

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Sita - Tarehe 20 Juni, 2012

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 44

Miundombinu Mibovu ya Barabara Tarime

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani ya uhakika kuhusu suala la miundombinu ya barabara katika Jimbo la Tarime?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime ina mtandao wa barabara wenyе urefu wa kilometa 763, ambapo kilometa 218.9 zinahudumiwa na Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Mara na kilometa 544.1 zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Kati ya hizo, kilometa 1.2 zimejengwa kwa kiwango cha lami, kilometa 118.5 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa 214 zimetengenezwa kwa kiwango cha udongo. Kilometa 406, sawa na aslimia 74 zinapitika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa kauli kwamba, itaendelea kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara nchini likiwemo Jimbo la Tarime. Hii inathibitishwa na ongezeko la bajeti ya matengenezo ya barabara kila mwaka, kwa lengo la kuzifanya ziweze kuitika mwaka mzima. Kwa mfano, katika Jimbo la Tarime, mwaka 2009/2010, Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 563.4 ambazo zilitumika kutengeneza barabara kilometa 133 na ujenzi wa daraja moja, *drift* moja na makaravati boksi tano.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011, Halmashauri ilipokea na kutumia jumla ya shilingi milioni 1,244.4 (sawa na ongezeko la asilimia 120), ambazo zilifanya matengenezo ya barabara zenyе jumla ya kilometa 210, ujenzi wa madaraja mawili na makaravati 25. Kwa mwaka huu wa 2011/2012, Halmashauri imetengewa jumla ya shilingi milioni 1,365.4 (sawa na ongezeko la asilimia kumi), ambazo mpaka sasa shilingi milioni 1,343, sawa na asilimia 98.4 zimeshapokelewa Halmashauri na utekelezaji wake unaendelea.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inajenga madaraja mawili; Daraja la Kiruba na Daraja la Mto Mori ambayo yamekuwa kero sana kwa Wakazi wa Tarime?

(ii) Kulingana na majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kwamba Barabara za Tarime ni kilometa 1.2 tu ndiyo zenyе kiwango cha lami. Je, Serikali inawaahidi nini Wananchi wa Tarime ili kuhakikisha kwamba Mji wa Tarime ambao una watalii wengi unapata barabara ya lami kuzunguka Mji wote wa Tarime?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kuhusu Madaraja ya Kiruba na Mori, gharama zake ni kubwa sana na nikisema hapa kwamba Halmashauri inaweza ikafanya hii hata *ceiling* yao hawataweza. Ushauri tunaoutoa sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu ni kwamba, tuone kwa pamoja namna mnavyopitisha jambo hili katika *RCC* na *DCC* na Halmashauri yenye ilii tumwombe Waziri mwenye dhamana ya ujenzi, yeze ndiye mwenye mamlaka ya kupandisha hadhi madaraja haya, tuweze kusaidiwa. *Otherwise*, tukisema kwamba Halmashauri tutajenga hapa itakuwa ni kitu ambacho kwa maoni yangu nadhani ni kigumu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu suala la kujenga barabara kwa kiwango cha lami, tumpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoiifanya katika Halmashauri yake ya Tarime. Hili ni suala la *priority*, ni suala la kuangalia anafanya nini, kwa sababu ukizungumza habari ya barabara ya lami, juzi juzi tulikuwa tunaambiwa barabara ya lami kilometa moja ni kama bilioni moja na *point*, wamepunguza punguza juzi imefika kama milioni 700 au 800. Nikijibu haraka haraka hapa nikamwambia Mheshimiwa Nyangwine kwamba, tutakwenda kujenga, watu watanishangaa kwamba sasa nasema inawezekana.

Nadhani kama ambavyo wamekuwa wanakwenda na wale wanaoangalia Mji wa Tarime na kama nilivyoeleza hapa, kuna hatua kubwa sana ambayo imepigwa pale. Ushauri wangu ni kwamba, twende tukaangalie fursa na vikwanzo

katika maendeleo. Sasa muiweke katika *priority* kuona kwamba mnaweka pale halafu ikiletwa kwenye Bajeti sisi hatuna tatizo.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa Barabara ya Rujewa - Madibila ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwemo kwenye bajeti mwaka uliopita lakini hadi ninavyozungumza haijakamilika. Je, mwaka huu Mheshimiwa Waziri ananihakikishia kwamba barabara hiyo itajengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Kilufi, lile swali lilikuwa ni la Barabara za kule Tarime. Sasa ukisema barabara zote mbona sisi wote tunaweza tukauliza barabara zetu zitajengwa. Waziri hakujandaa, lakini kama unalijua Mheshimiwa Naibu Waziri jibu. Yaani *specific question* haliwekwi kwenye nyongeza, ndiyo maana wakati mwingine maswali yenu hayapati majibu kwa sababu huyu alijiandaa Barabara za Tarime tena aende Mbarali kule, inakuwa ni tatizo.

Maswali ya nyongeza yawe yanaongeza katika swali la msingi au ni la kisera kwa ujumla wake. Swali la Kisera lazima Waziri ye yote ajibu, lakini *specific* hawezি.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Shekifu.

Na. 45

Mgogoro wa Viwanja Kati ya Wananchi na Halmashauri

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU aliuliza:-

Upo mgogoro wa viwanja kati ya Wananchi wa Mji wa Lushoto na Halmashauri hiyo ambapo mwaka 1998 Wananchi waliokuwa na viwanja karibu na eneo la Hospitali

walipokonywa viwanja na kuahidiwa kupewa viwanja katika eneo lingine. Hata hivyo, mwaka 2010 pamoja na viwanja vipyä kupimwa, Wananchi hao hawakupewa viwanja na hivyo kuamua kwenda Mahakamani:-

(a) Je, Serikal ina tamko gani kwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa kutowatendea haki Wananchi?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Watumishi wa Halmashauri hiyo ambao ushahidi uliopo unaonesha kuwa walitoa ushauri mbaya kwa Uongozi wa Wilaya kwa maslahi yao binafsi na hivyo kuleta chuki kati ya Wananchi na Serikali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Dafa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo linalolalamikiwa ni eneo ambalo awali lilikuwa Hifadhi ya Msitu likijulikana kama *Eucalyptus Territorial Forest Reserve Lushoto* chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Msitu huu ulikuwa Lushoto Mjini ambapo kwa sasa umefutwa na pamepimwa viwanja vyaa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, viwanja 36 vinavyopakana na Hospitali ya Wilaya ya Lushoto vilisitishwa kuendelezwa na kutwaliwa kutoka kwa wamiliki kwa lengo la kupata eneo la kutosha la upanuzi wa Hospitali hiyo. Maamuzi haya yalifanywa na Kikao cha Baraza la Madiwani kilichokutana tarehe 4 Februari, 1998. Uongozi wa Halmashauri ulifanya hivi ukiwa na mpango wa kuwapa Wananchi viwanja mbadala mahali pengine. Hata hivyo, baadhi ya Wananchi hawakukubaliana na uamuzi huu na waliamua kufungua kesi Mahakamani. Kwa vile Wananchi wamefungua kesi Mahakamani, suala hili

haliwezi kushughulikiwa hadi hapo hukumu itakapotolewa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuchukua hatua kwa Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya waliota ushauri mbaya ni kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma (Na. 8 ya 2002), Halmashauri ndiyo Mamlaka ya ajira, upandishaji vyeo na nidhamu kwa watumishi walioajiriwa kwenye Halmashauri husika isipokuwa Mkurugenzi. Hivyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira hadi hukumu ya Mahakama itakapotolewa. Baada ya hapo uamuzi wa kuwachukulia ama kutowachukulia hatua utatolewa na mamlaka za nidhamu za watumishi hao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Naibu Waziri. Mimi sijatosheka sana na swali ilivyojibiwa. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kero hii inajulikana wazi kwamba ni jeuri ya Watendaji na mwaka 2007/2008 Rais alitoa maagizo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuunda Kamati ya kusimamia kero za ardhi. Kipindi kile kero zilipungua. Je, hii ilikuwa nguvu ya soda kwa upande wa Serikali?

(ii) Kwa kuwa watumishi hawa walofanya hivi wanajua kabisa kwamba wamewapokonya wananchi haki na inawezekana kabisa kwamba kwa makusudi hayo Halmashauri ikashtakiwa na kama ilivyoshtakiwa ikabidi ilipe fidia. Je, kwa nini wafanyakazi hawa na wao wakijulikana kufanya kwa makusudi wasisimamishwe kazi na baadaye Mahakama kama itatoa adhabu ya kuiwajibisha Halmashauri na wao washtakiwe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, naomba nikueleze jambo hili na wala sina tatizo kabisa na mambo

ambayo anasema Mheshimiwa Shekifu. Suala hili lilitokea mwaka 1998, limekuwa *mis-handled* na limekuwa na matatizo hayo ambayo yamezungumzwa kama nilivyoeleza. Sasa kutoka mwaka 1998 mpaka leo tunavyozungumza hapa, hata ukimwuliza Mkurugenzi aliye pale, yule mwanamama, anajibu unamwona kabisa kwa kweli hana picha kamili huko nyuma nini kilichotokea lakini anakiri kwamba tatizo hili lipo. Sasa kilichotokea nikwamba, hawa wameondoka wamekwenda Mahakamani.

Mheshimiwa anazungumza kuhusu Tume ambayo iliundwa na Rais, walizunguka nchi nzima kuangalia matatizo haya na haya yote watakuwa wameyazungumza kama anavyosema Mheshimiwa Shekifu. *Problem* ninayopata hapa kwa upande kwa *administration*, mimi ningeweza kutoa maelekezo ni nini ikafanyike, lakini kesi hii ipo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kama hii habari ipo Mahakamani mimi nitasema nini; *unless*, Mheshimiwa Shekifu aniambie wanakwenda kutoa kesi ile Mahakamani ili sasa tukija hapa tutoe mawazo ya kiutawala. Kwa sasa hivi inakuwa vigumu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili; hawa watumishi inawezekana kabisa na mimi nakubaliana naye kwamba kuna watumishi watakuwa wame-*mis-handle* hili jambo. Katika Utawala Bora na wa haki na hapa wala sitaki kum-*defend* mtu yejote, ninachosimamia hapa ni Sheria. Kama wamefanya hivyo na kesi hii imekwenda Mahakamani, *verdict* yake itategemea na Mahakama imesema nini kuhusu jambo hili. Kwa hiyo, namwomba sana mjomba wangu Mheshimiwa Shekifu asubiri. Wakisema kwamba, watumishi hao ndiyo walihusika pale wala hatuna haja ya kuja kukaa hapa kuzungumza, wale ni *out* moja kwa moja.

SPIKA: Ila tu Mkurugenzi Mwanamama nadhani siyo sawa ni Mkurugenzi tu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona niulize swali moja la nyongeza.

Hivi karibuni kumekuwa na jithhada za Wizara ya Ardhi kusuluuhisha migogoro ya ardhi katika Mji wa Babati, maeneo ya Bagara, kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kutoka Wizara ya Ardhi kutembelea Wananchi wale. Cha kusikitisha, wiki moja baada ya ziara hiyo, TAMISEMI wakawahamisha Afisa Mipango Miji na Afisa Ardhi wa Halmashauri wakati migogoro hiyo haikuweza kupatiwa ufumbuzi.

Je, Serikali kwa kufanya hivyo siyo kwamba inawalinda Watumishi hao wakati wamesababisha migogoro hiyo? Kwa nini wanawahamisha badala ya kuwasimamisha kazi?

SPIKA: Wapi huko?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Babati.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri unajua habari za Babati? Yale yale mtu anaacha swali la msingi anakwenda kwingineko. Jaribu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu kuna Sera ya kuhamisha mtu baada ya kukosea mahali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mambo haya anayoyazungumza Mheshimiwa Gekul, amekuwa akiyasema mara kwa mara. Labda nisemee hili analolisema sasa; hapa ndani tumeambiwa na tunaendelea kusitisiza, mtumishi akifanya mambo ya ajabu ajabu, amevuruga kule, hela zimetumika vibaya au kuna migogoro na nini, msimamo uliopo ni kwamba, hakuna kumhamisha tena, atajibu yale mambo pale. Kwani huyu amekwenda Canada au Argentina? Tutamrudisha pale, kama kuna jambo la kujibu atakwenda kujibu tu. Tanzania hii ni nchi moja, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Gekul, njoo tukae tuzungumze vizuri tujue *issue* hii

ni nini. Upo mgogoro pale na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi alikwenda pale. Kwa hiyo ni jambo kubwa hili na mimi nasema *we welcome the idea* tushirikiane wote kwa pamoja katika jambo hili.

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASSIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa matatizo yaliyotokea kule Lushoto yanawiana sawia na yale yalipo Sobibo pale Kilole, Korogwe; na kwa kuwa yale yaliyoko Korogwe hayapo Mahakamani; nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala la Wananchi kunyang'anywa viwanja au mashamba yao na hatimaye kutokupewa fidia?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nikisema nitoe kauli ya Serikali haraka haraka kwenye maswali ya nyongeza nitapata matatizo. Mimi naomba atuletee katika hali ya kawaida, ambayo nitakuwa nimetulia *ni-study* jambo lenyewe. Najua amekuwa analizungumza lakini kusema kwamba, naweza kulitolea kauli hapa itakuwa vigumu kidogo. Namkaribisha Mheshimiwa Mbunge aje tuzungumze, anaweza akaleta kwa barua tuone namna ya kufanya.

SPIKA: Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani upo?

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, nipo.

SPIKA: Pole sana.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Ahsante sana. Naomba sasa swali langu namba 46 lipatiwe majibu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Huyu alikuwa mgonjwa alilazwa. Aliugua Bunge liliopita akapelekwa India, namwona yupo lakini ana bandeji sijui kwa sababu gani!

Mradi wa Maji wa Sakare – Bungu

MHE. STEPHEN H. NGONYANI aliuliza:-

Serikali iliahidi kumalizia Mradi wa Maji wa Sakare – Bunge ambao umekamilika kwa asilimia 60 hadi sasa:-

- (a) Je, Mradi huu utakamilika lini?
- (b) Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kukamilisha Mradi huu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wangu wa Siha, naomba kumpa pole Mheshimiwa Stephen Ngonyani na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba, amemrudisha tena Bungeni na anaendelea na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Sakare – Bungi ni Mradi wa Maji ya Mserereko kutoka chanzo cha Sakare ambapo ulianza kujengwa mwaka 2002. Gharama za awali zilikadiriwa kuwa shilingi milioni 500. Kazi zilizokuwa zimepangwa kufanyika ni ujenzi wa banio, matanki matatu ya kuhifadhia maji yenye jumla ya ujazo wa lita 270,000, ulazaji wa mtandao wa mabomba yenye vipenyo kuanzia inchi moja hadi sita, sawa na kilometra 43.21 na vituo 54 vya kuchotea maji. Mpaka sasa kazi zilizokamilika ni ujenzi wa banio (*intake*), utandazaji wa mabomba kilometra 7.83, ujenzi wa tanki moja la kuhifahia maji

na kituo kimoja cha kuchotea maji katika Kijiji cha Manka, ambazo zimegharimu jumla ya shilingi milioni 444.3. kutoka Shirika la *World Vision*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/12, Shirika la *World Vision* limepanga kutumia shilingi milioni 229.5 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Mradi huo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 187.7 zimepangwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa tenki moja na mtandao wa bomba katika Kijiji cha Bungu. Tayari Mkandarasi ambaye ni kampuni ya *Engineering Plus Tanzania Ltd* ya Dar es Salaam imesaini mkataba wa miezi minne kuanzia tarehe 15 Mei, 2012 hadi tarehe 14 Septemba, 2012. Aidha, shilingi milioni 41.25 zitatumika kukamilisha mtandao wa maji katika Kijiji cha Manka, wenye jumla ya kilomita 7.38. Kukamilika kwa Mradi huu kunategemea upatikanaji wa fedha zinazotengwa kila mwaka katika Bajeti ya Halmashauri.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe katika Bajeti yake ya Mwaka 2012/13, imetenga shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Sakale – Bungu.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, namshukuru mjomba wangu kwa majibu yake mazuri.

(i) Kwa kuwa Mradi huu umekaa zaidi ya miaka kumi na Miradi mingine mingi ambayo inakaa kwa muda mrefu huwa Serikali mnaingilia na kuitatua; ni tatizo gani linasababisha Serikali isinisaidie kumaliza kero hii ya maji ambayo imekaa pale zaidi ya miaka 20 na Wananchi wa Bungu wakiwa wanahangaika kwa miaka yote hiyo bila kupata maji?

(ii) Kwa kuwa nilikuwa nimeshaomba Mradi huu kwa Waziri wa Maji wa wakati huo na akaniahidi; Serikali inatamka ni lini Mradi huo utakuwa umeshakamilika? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ukiangalia swali lile lilivyoulizwa, Mbunge mwenyewe anakiri kwamba asilimia 60 ya Mradi huu imeshatekelezwa na ukiangalia *trend* na *pattern* ya Miradi yote ya Maji, hapa utaona kwamba mingine ipo chini ya asilimia sitini na vitu vingine vyaa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama anavyosema Mbunge, amekuwa anahangaika na Mradi huu, mara nyingi sana ametutaka twende tukauangalie; mimi nampongeza sana kwa kazi kubwa. Tulipokwenda kuangalia ni kiasi gani kimetengwa na Halmashauri acha hawa wanaowasaidia ambao ni *World Vision*, tukakuta wametenga milioni sitini tu, kwa maana ya *priority* yao pale. Kwa hiyo, kama Mbunge anadhani kwamba huu Mradi ni *priority, then* kuna maana ya kwamba, kurudi tena nyuma na kwenda kuangalia kipaumbele hiki kiwekwe kule. Kwa hapa tulipofika, *position* ya Serikali katika Bajeti yake *is already established*, wiki ijayo tunaanza kuisoma hapa; atakachofanya sasa labda ni kwenda kuomba kibali *wa-rearrange priorities* zao tena ili waiweke katika sura hii inayozungumzwa.

La pili, amezungumza kuhusu ahadi ya Waziri wa Maji; sasa Waziri wa Maji ni huyu aliyeo nyuma yangu hapa ambaye ndiyo ameingia, tutataka kujua kutoka kwake ni nini kilichoahidiwa na kiasi gani kilichoahidiwa. Waziri wa Maji bado yupo anasikia yeye mwenyewe hapa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, nitawasilisha ile ahadi ya Waziri wa Maji kwake ili iweze kutekelezwa kama alivyokuwa ameahidi.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile Mradi huu wa Maji wa Kitaifa ambao unachangiwa kwa sehemu kubwa na Benki ya Dunia unaonekana kusuasua katika utekelezaji; na kwa kuwa hata

pesa ambazo wananchi wanachanga zingine zinaibiwa kama ilivyotokea Serengeti, Kijiji cha Nata, Wananchi walichanga shilingi milioni 21 lakini shilingi milioni 14 zikaibiwa kwa kushirikiana na Benki ya *CRDB*:-

Je, Serikali ina mpango gani kutazama upya utekelezaji wa Mradi huu mkubwa ili pale ambapo Wananchi wanalazimika kuchangia fedha basi wachangie nguvu zao ikiwemo kuchimba mitaro, kuchanga kokoto, mawe na vitu kadhaa ambavyo vinasaidia utekelezaji wa Mradi huu?

SPIKA: Miradi ya Benki ya Dunia; Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita wa fedha, kuna shilingi sabini bilioni ambazo zipo kwenye Wilaya mbalimbali zikingojea utekelezaji wa Mradi huu. Katika Bajeti ya Serikali itakayosomwa na Waziri Mkuu wiki ijayo, zipo fedha zingine shilingi themanini na moja bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo. Kwa hiyo, kwa mwaka ujao wa fedha Miradi mitatu kwenye kila Wilaya itatekelezwa kwa fedha ambazo zimetengwa. Aidha, tumekuwa na mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Ujerumanu na *DFID* na yapo matumaini ya kupata fedha zingine shilingi ishirini na saba bilioni kwa ajili ya Miradi hiyo. Tunategemea kwa fedha hizo ambazo zimeongezeka, vijiji vingine viwili katika kila Wilaya Tanzania nzima vitatekelezwa. Kwa hiyo, jumla ya vijiji vitano vitatekelezwa. Baada ya hapo ni vizuri tuzungumze na tuangalie ni jinsi gani tunakwenda mbele na Miradi hii, ikiwa ni pamoja na kufikiria mawazo mazuri ambayo yamependekezwa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Matatizo yaliyopo Serengeti hayana tofauti na

yaliyopo Wilaya Chemba na nimekuwa mara nyingi nikiuliza ndani ya Bunge hili.

SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia, hili swali lilikuwa la Tanga huyu Mheshimiwa Dkt. Kebwe, nimemkubalia kwa sababu Miradi ya Benki ya Dunia ni ya Kisera.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, labda kwa sababu ipo jirani yangu hapa.

SPIKA: Haya.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nilitaka kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na Mama Maria, walilala siku saba katika Wilaya ya Kondoa hususan katika Jimbo la Kondoa Kusini, kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Ntomoko. Leo Wananchi wa Wilaya ya Nchemba wanalazimika kubadilisha debe la mahindi kwa debe la maji.

Je, Waziri yupo tayari kuongozana na mimi Jumamosi hii kwenda kuangalia adha wanayoipata Wananchi wa Jimbo lile na yupo tayari ule Mradi sasa uingie Serikali Kuu kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa haina uwezo tena wa kuhudumia Mradi ule? Ahsante.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Juma Nkamia, utajadili wakati wa Wizara ya Maji, hilo halikuwa suala la msingi. Tunaendelea na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed atauliza swali linalofuata.

Juhudi za Kunusuru Mlima Kilimanjaro

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED aliuliza:-

Mlima Kilimanjaro ni kati ya maajabu makubwa Duniani na moja kati ya alama kubwa tatu zitokanazo na athari ya mabadiliko ya tabianchi:-

(a) Je, Serikali ya Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa zimechukua hatua gani za kimkakati kunusuru Mlima huo na maeneo ya vijiji jirani?

(b) Je, tathmini inaonesha ni kiasi gani cha theluji kilichopungua kutokana na athari ya mabadiliko ya tabianchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mlima Kilimanjaro ni moja ya maeneo muhimu yaliyoathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Athari za kupungua kwa theluji zimethibitishwa na Toleo la Nne la Ripoti ya Jopo la Wanasyansi wa Mabadiliko ya Tabianchi Duniani ya Mwaka 2007. Kufuatia kupungua kwa theluji, jitihada mbalimbali za Kimataifa na Kitaifa zimeanza kuchukuliwa kama ifuatavyo:-

(i) Kundelea kuzibana nchi zinazoendelea kupunguza uzalishaji wa gesi joto duniani kwa asilimia 5.8 kuitia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*UNFCCC*) na Mkataba wa Kyoto (*The Kyoto Protocol*);

(ii) Kutekelezwa kwa Mradi wa Maendeleo Endelevu ya Ardhî Mkoani Kilimanjaro chini ya Mpango Maalum wa Afrika wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*Terra Africa*). Mradi huu unafadhiliwa na *UNDP* kwa miaka minne (2011 - 2015), kwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni tatu. Ofisi za Mradi zipo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro;

(iii) Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (*EU*), imedhamiria kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Kitaaluma cha Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kilimanjaro ili kufanya utafiti na kutoa elimu. Tayari upembuzi yakinifu umefanyika;

(iv) Kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *KINAPA*, juhudî mbalimbali zinaendelea kufanya za kupanda miti na kudhibiti uchomaji moto. Vile vile Uongozi wa Mkoa umezuia kabisa uvunaji wa miti ya mbaô na kuni kutoka maeneo ya Mlima huo; na

(v) Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira kwa Wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro, kwa kupitia Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa, yaani MKUHUMI. Programu hii ilianza mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Jopo la Wanasayansi wa Mabadiliko ya Tabianchi Duniani, Toleo la Nne la Mwaka 2007 inaonesha kuwa, theluji ya Mlima Kilimanjaro imepungua kwa asilimia 80 katika karne ya ishirini. Aidha, Ripoti hii inaonesha kuwa, iwapo mabadiliko ya tabianchi yataendelea, kiasi cha theluji kilichobaki juu ya Mlima huu kinaweza kutoweka kati ya mwaka 2015 na 2020. Hivyo, nachukua fursa hii kuhimiza Uongozi na Wananchi wote wa Mkoa kuongeza jitihada za kutunza mazingira ya Mlima huo.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante.

(i) Kwa kuwa *data* zote zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi zinatoka Ulaya na Marekani na hakuna Taasisi yoyote ya Kisayansi katika Afrika ambayo inakusanya *data* hizi; na kwa kuwa kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri ni kwamba EU imeonesha dhamira ya kuisaidia Tanzania kujenga kituo hiki: Je, ni lini kituo hiki kitaanza kujengwa?

(ii) Narudi katika Kisiwa changu cha Pemba; mabadiliko ya tabianchi yanaathiriwa zaidi na bahari. Najua katika Wizara yako una Mfuko wa *Global Fund*. Je, Mfuko huu umesaidiaje Kisiwa cha Pemba katika kuhifadhi mazingira?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anauliza ni lini kituo kitaanza kujengwa. Kama nilivyojibu katika swali la msingi, upembuzi yakinifu tayari umeshafanyika, pesa za ujenzi zipo, lakini hatuwezi kuanza kujenga mpaka *detail design* itakapokuwa imekamilika. Tusubiri na nimwombe Mbunge na Wananchi wa Kilimanjaro wawe na subira kidogo, pale ambapo *detailed design* itakapokuwa imekamilika na *Project Plan* kuwa imetolewa, basi tutaweza kuwaeleza *exactly* tarehe ya kuanza ni lini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ambalo amezungumzia *Global Fund* katika eneo la Zanzibar; ni kweli *GEF* ina Miradi mbalimbali ikiwepo Mradi ambao unahusisha kuhakikisha maeneo ya Pwani na Zanzibar yanawekwa katika hali yake ya kawaida. Kwa upande wa Zanzibar maeneo ya Ukere, katika kisiwa cha Pemba na eneo la Bwawani katika Kisiwa cha Unguja, vile vile katika maeneo ya Tumbe upande wa Mashariki na Tumbe upande wa Magharibi yote yatafanyiwa na yanahusishwa. Jumla ya Dola za Kimarekani laki tatu na sitini na tano zitatumika katika maeneo hayo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Grace Kiwelu, Kiongozi wako amesimama, kwa hiyo namwita Kiongozi wako; Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro unachangia kwenye Pato la Taifa zaidi ya shilingi bilioni themanini kwa mwaka. Hiki ni kiwango kikubwa sana na kupotea kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro siyo jambo la dharura ni jambo ambalo limekuwa linaendelea kwa miaka mingi na mara nyingi kupitia Bunge hili, Serikali imetambua tatizo hilo.

(i) Swali ambalo napenda kumwuliza Waziri kwa niaba ya Serikali; kwa kutambua umuhimu wa Mlima huu kwa biashara ya utalii na kwa biashara ya mazingira na kwa kipato ambacho kinaingizwa kwenye Pato la Taifa. Serikali ina mpango gani wa makusudi kwa sababu Miradi yote ambayo imeelezwa hapa inafadhiliwa na watu wa nchi za nje lakini hatuna mpango wetu wa ndani wa kuu-*sustain* Mlima huu. Kauli aliyoitoa Waziri anatuambia kwamba theluji katika Mlima huu amba ni kivutio kikubwa cha utalii inakaribia kwisha katika kipindi cha miaka mitatu ijayo?

(ii) Mwaka 2015 ni karibu mno; Serikali ukiacha Mipango mingine ya Kimataifa ina mpango gani wa makusudi wa ndani kuona kwamba inasaidia Mkoa wa Kilimanjaro kutunza mazingira ya Mlima huu ili theluji hii angalau tuweze kurefusha uwepo wake?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Spika, labda kwanza nieleze umuhimu na nini hasa kinasababisha hii theluji kuondoka, watu wanasema inayeyuka, theluji haiyeyuki. Sote tunafahamu kwamba, Mlima Kilimanjaro kilele chake ni mita 5,895 *above sea level*. Wote tunaruka na ndege, ukivuka mita elfu tano, *temperature* katika *level* hiyo ipo *below zero*, kwa vyovvye vile ile theluji kule kwa sababu *temperature* ipo *below zero* haiwezekani ikayeyuka hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, nini kinasababisha? Katika Ripoti nilioisema ya Tabianchi ambayo imetolewa mwaka 2007, inaonesha kwamba, asilimia themanini ya mabadiliko katika dunia yanababishwa na wenyewe viwanda vikubwa kwa kuongeza hewa joto katika dunia. Sisi kwa kukata miti kwa uharibifu wa mazingira, asilimia 20 hiyo tunaisababisha. Sasa tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, kinachosababisha theluji iondoke katika kilele cha Mlima Kilimanjaro ni kukosekana kwa maji mengi au unyevunyevu utakaopanda kule juu na utakapofika katika kilele yaweze kuganda kuendelea kutengeneza barafu. Sasa kama hatutatunza mazingira yetu, hilo haliwezekani kwa sababu tukilima, tukikata miti, sisi kama Serikali, tumechukua juhudhi maalum, ndiyo sababu Mkoa wa Kilimanjaro mwaka huu umepata zawadi ya upandaji miti. Vile vile tumeeleza kuititia kwa Mkuu wa Mkao, wamepiga marufuku ukataji wa miti kwa ajili ya mbao, hata miti kwa ajili ya kuni.

Vile vile tunaendelea kuhamasisha Wananchi waendelee kupanda miti na waendelee kuyatunza mazingira yaliyopo katika Mlima Kilimanjaro. Namna hiyo tutawezesha hali ya kawaida ya kuwezesha Mlima Kilimanjaro uendelee kupata unyevunyevu wake na hali ya kawaida ya mvua na unyevunyevu utaendelea kawaida na ile theluji itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba ndugu zangu na yeze kama Mbunge kutoka Mkao wa Kilimanjaro, tushirikiane pamoja. (*Makofi*)

SPIKA: Naona jibu lilikuwa linatosha kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Cecilia Paresso, atauliza swali hilo. (*Kicheko*)

Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Karatu

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Mahakama ya Karatu inakabiliwa na upungufu mwingi ikiwemo jengo kutokamilika, ukosefu wa Mahakama ya wazi, mashimo ya choo na ukosefu wa rasilimali watu, hali inayosababisha ucheleweshaji mkubwa wa kesi:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Karatu?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya kuongeza rasilimali watu ili kuondoa ucheleweshaji wa kesi mahakamani?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, jengo linalotumika na Mahakama ya Wilaya ya Karatu ni la Mahakama ya Mwanzo ya Karatu, ambalo lilibadilishwa matumizi yake baada ya kuona umuhimu wa kuanzisha Mahakama hii ya Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, jengo hilo halijakamilika kwa kukosa vizimba kwa ajili ya washtakiwa, vizimba kwa ajili ya mashahidi na sehemu ya kukaa Hakimu anaposikiliza kesi. Kuhusiana na ukosefu wa mashimo ya choo,

Mahakama hiyo inayo vyoo vya nje vinavyotumia maji kwa ajili ya kutumika na Wananchi wanaofika katika Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, licha ya upungufu uliopo, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Mahakama ya Wazi (*Open Court*) ipo na katika mwaka ujao wa fedha, Mahakama itajenga vizimba, sehemu ya kukaa Hakimu anaposikiliza kesi na vyoo vya nje vya mashimo, kwa ajili ya matumizi ya Wananchi wanaofika katika Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, jumla ya watumishi wote waliopo katika Mahakama ya Wilaya ya Karatu ni watano, ambao ni pamoja na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya, Karani mmoja, mpiga chapa mmoja, Mhudumu mmoja na Mlinzi mmoja. Kutokana na upungufu huo, Mahakama inakusudia nyongeza watumishi zaidi katika Mahakama hii katika mwaka ujao wa fedha.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kufika Karatu na kujionea hali halisi. Kwa kuwa upungufu huu umekuwa kero katika Mahakama nyingi na kwamba mambo haya yanapelekea kudorora katika utendaji na kutokuleta ufanisi unaokusudiwa. Je, Serikali ipo tayari kukamilisha upungufu huu katika Mahakama ya Wilaya ya Karatu ndani ya miezi mitatu ya mwaka wa fedha unaoanza? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kuhusiana na upungufu ambao umekuwa kero na kwamba endapo Serikali ipo tayari kukamilisha upungufu huo ndani ya miezi mitatu. Nadhani Mheshimiwa Mbunge, anajua taratibu za kibajeti na bajeti ijayo ya fedha itaanza tarehe 1 mwezi Julai. Zipo taratibu mbalimbali ambazo zinahitaji kukamilishwa kabla haijatekeleza upungufu huo. Napenda kumuahidi kwamba atuamini, ndani ya mwaka ujao wa fedha haraka iwezekanavyo tutajitahidi upungufu huu

uweze kurekebisha. Hata hivi sasa nilifanya ziara tarehe 4 mwezi Juni kama ambavyo ameeleza na nilikuta upungufu kama vile nyufa mbalimbali zilikuwa pale na tayari nilishaagiza mkandarasi na Jumapili hii alishafika *site* kwa ajili ya kurekebisha marekebishiyo hayo. Ahsante.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa swali la msingi linaongelea jinsi ambavyo huduma za mahakama zimekuwa hazipatikani; na kwa kuwa swali hili la msingi linaihusu Wilaya ya Kalambo ambayo haina hata Mahakama moja inayofanya kazi kwa kuwa hakuna Mahakimu:-

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutoa ahadi lini Mahakimu watapelekwa Kalambo ili Wananchi wapate haki yao bila usumbufu?

SPIKA: Wewe swali lako ungeuliza hivi; kutokana na upungufu wa Mahakimu Serikali ina mpango gani? Kijumla, siyo habari ya kwenu huko. Naomba ujibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Suala la upungufu wa Mahakimu wote tunafahamu lipo katika Mahakama zote nchini. Tunazo Mahakama za Wilaya takriban 116, lakini Serikali tunajitahidi kwa kadiri inavyowezekana, tumeshasaili Mahakimu 300 na muda wowote kuanzia tarehe 22 Mwezi huu wa Juni, Kikao cha Menejimenti kitakaa kwa ajili ya kuwapangia kazi Mahakimu mbalimbali ili waweze kuripoti kazini. Vile vile tunatarajia kuwapandisha vyeo Mahakimu 73 wa Mahakama za Mwanzo ili waweze kusambazwa katika Mahakama zote nchini. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea; *time*.

Uharibifu wa Mazingira Mkoani Kilimanjaro

MHE. BETTY E. MACHANGU aliuliza:-

Kuanguka kwa uzalishaji wa Zao la Kahawa Mkoani Kilimanjaro kumesababisha Wananchi kuvamia rasilimali za misitu na kupelekea Mkoa huo kukabiliwa na janga la uharibifu wa mazingira na uoto wa asili:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wananchi juu ya janga hili na inasaidiaje Wananchi hao kujikwamua na tatizo hilo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuongeza Watumishi wa Idara ya Misitu na vitendea kazi ili kupambana na uharibifu wa mazingira?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya uharibifu wa misitu nchini ukiwepo Mkoa wa Kilimanjaro ni mbaya na ya kutisha. Katika Mkoa wa Kilimanjaro pekee, jumla ya hekta 30 za Misitu ya Kindoroko, Minja, Kamwala na Chambogo, imeteketea kwa majanga ya moto hadi kufikia mwezi Mei, 2012. Aidha, hekta 15 za Hifadhi ya Misitu wa Rau zimevamiwa kwa shughuli za kilimo na ukataji miti kinyume na sheria na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira karibu kabisa na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatahadharisha Maafisa Misitu ya Mikoa na Wilaya kote nchini na kwa Mameneja wa Hifadhi zote za Misitu, kuzingatia Sheria na Taratibu za Kazi katika maeneo yao. Aidha, Wizara yangu itafanya tathmini katika maeneo yao pale itakapobainika kumetokea uharibifu huku wahusika wakiangalia kwa macho yao, Serikali itawachukulia hatua za kinidhamu na Bunge lako Tukufu litatarifiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri aliyetangulia, kupitia kikao chake cha *RCC* cha tarehe 29 Februari, 2012, amepiga marufuku kwa muda uvunaji wa miti ya asili isipokuwa mashamba ya kupandwa ya Rongai na Kilimanjaro Magharibi. Hatua hii ina lengo la kupunguza kasi ya kutoweka kwa misitu ya asili na kupambana na ongezeko la uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, mnamo Julai, 2011, Serikali ilianzisha Wakala wa Huduma za Misitu (*Tanzania Forest Services - TFS*) ili kusimamia na kuendeleza misitu kote nchini. Wakala utafanya tathmini ya mahitaji ya Watumishi kwenye Sekta ya Misitu na Nyuki katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13. Baada ya zoezi hilo kukamilika, Wakala utaaajiri Watumishi wa Kada ya Misitu hususan Walinzi wa Misitu (*Forest Rangers*), ikiwa ni pamoja na kuongeza vitendea kazi kama magari na pikipiki ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji.

SPIKA: Mimi naona kuna wengine wamejisahau wanafikiri wapo nje, tupo kwenye kikao, maana wanaongea mpaka wana-*disturb* tunashindwa kusikiliza.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Utafiti uliofanywa na *Oversee Development Institute* ya Uingereza ukigharamiwa na *Netherlands Development*

Organisation ya Mwaka 2011 uligundua kwamba mapato yanayotokana na Hifadhi ya Mlima huu ni takriban dola milioni 50 kwa mwaka, yaani bilioni 80. Sera ya Nchi hii wawekezaji popote pale walipo wanalipa kwenye Halmashauri kodi inayoitwa *service levy*, wengine wanalipa kiasi cha dola 200 kwa mwaka. Je, ni lini Wawekezaji wa Utalii katika Hifadhi ya Mlima wa Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa watalipa *service levy* kwa zile Halmashauri zinazowazunguka kwa ajili ya kuendelea kulinda Hifadhi hii?

(ii) Kwa umuhimu wa pato linalopatikana; Serikali ipo tayari sasa ku-*declare* uhalibifu wa mazingira kama Janga la Taifa ili kunusuru misitu yetu na utalii?

Hapa naomba nieleze kidogo; ukitoka Kigoma mpaka Ruvu ni mkaa, Ukitoka Manyara mpaka Ruvu ni mkaa, sijaenda huko Kusini lakini nina-*imagine* kwamba ni hivyo. Ipo siku miti itakatwa mpaka tutakosa oksijeni ya kuvuta. Naomba Serikali itoe tamko; ipo tayari ku-*declare* uharibifu wa mazingira kama Janga la Taifa? (*Makofi*)

SPIKA: Ule mrabaha siyo 200 ni 200,000. Nadhani umesema 200, nafikiri ni 200,000.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Betty Machangu, kama ifuatavyo:-

Kwanza, namshukuru sana yeye na Waheshimiwa Wabunge wa Kilimanjaro, akiwemo Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni, kwa kulisimamia vizuri hili suala la hatari tunayoipata katika kutoweka kwa vyanzo vyta maji, vyanzo vyta miti na theluji katika Mlima wetu wa Kilimanjaro.

La pili, nakubaliana sana na Mheshimiwa Betty Machangu kwamba, kipato kinachotokana na Mlima Kilimanjaro na niseme tu kwamba, Mlima Kilimanjaro ndiyo

unaoongoza kwa kuingiza pato katika Hifadhi zetu zote za Taifa ukifuaatiwa na Hifadhi yetu ya Serengeti. Hivyo, katika sehemu ya uwajibikaji ya *TANAPA*, tunaendelea kuhakikisha kwamba wanashirikiana na Mkoa wa Kilimanjaro na mawazo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa akiwepo Mheshimiwa Betty, tutaendelea kuyasikiliza na kuangalia yanawekwa vipi katika utaratibu wetu wa kawaida. Niseme mwaka jana tu, *TANAPA* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Mkoa wa Kilimanjaro, waliweza kufanikiwa kupanda miti milioni saba katika Mkoa wa Kilimanjaro peke yake.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu katika Mkoa wa Kilimanjaro peke yake na lile eneo linalozunguka Mlima, tunapanda miti milioni 8.2. Hizi ni jitihada tu za Serikali kwa kushirikiana na wadau na Wananchi wa Kilimanjaro kuhakikisha kwamba, tunarudisha hali ya Mlima Kilimanjaro kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

La pili, nakubaliana sana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hali ya kupotea kwa miti ni Janga la Taifa. Tunapotembea nchi hii kila mahali unaona miti imekatwa na taratibu hizi kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, tunaagiza kila Afisa Misitu nchini, Mikoa, Wilaya na wale *rangers* ambaو huwa wanalinda, wanafanya kazi zao na tunahakikisha kwamba, wale watu wote ambaو tutagundua, kwa mfano, pale *RAU*, pale *RAU* tumekuta hekta 15 za msitu ambaو umekuwa hifadhi siku nyingi umegeuzwa kuwa mashamba, umegeuzwa kuwa sehemu ya watu kukata mbao.

Tunaamini kwamba, kuna watu walikuwepo na Serikali sasa itahakikisha kwamba, tunaliangalia siyo tu *RAU*, lakini nchi nzima ili kila anayehusika aweze kuwa *responsible* na tutahakikisha kwamba, taarifa hiyo ya uchunguzi wetu tunailleta hapa Bungeni.

SPIKA: Majibu marefu, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi.

Na. 50

Uchakavu wa Meli – Ziwa Nyasa

MHE. CYNTHIA H. NGOYE aliuliza:-

Meli ndogondogo za Usafiri wa Wananchi waishio kandokando ya Ziwa Nyasa zimechakaa sana hali inayosababisha matatizo kwa wananchi hao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma ya usafiri wa abiria na mizigo katika Ziwa Nyasa hutolewa na meli mbili za Serikali zinazoendeshwa na Kampuni ya Huduma za Meli (*MSCL*). Meli hizo ni MV Songea, yenyewe uwezo wa kuchukua abiria 200 na kubeba tani 40 za mizigo na MV Iringa inayobeba abiria 125 na tani tano za mizigo. Meli hizo zimekuwa zikikabiliwa na uchakavu na hivyo kuhitaji matengenezo ambayo yatakapokamilika yataziwezesha kuendelea kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo ya Ziwa Nyasa.

Kampuni ya Huduma za Meli imekamilisha taratibu za kuifanyia matengenezo makubwa Meli ya MV Songea yatakayofanyika nchini Malawi, ambapo kuna chelezo kinachowenza kufanya kazi hiyo.

Gharama za matengenezo hayo ni shilingi 134,000,000. Fedha za matengenezo hayo zipo. Malipo ya awali ya shilingi milioni 30 yamelipwa. Meli hiyo imeondoka jana tarehe 19 Juni,

2012, alfajiri saa 11.00. Matengenezo hayo yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2012.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali katika kipindi cha miaka 2012 hadi 2015 ni kuzifanyia matengenezo makubwa meli za MV Songea na MV Iringa zilizoko katika Ziwa Nyasa.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninamshukuru kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba meli zote mbili; MV Songea na MV Iringa zimechakaa sana na zinahitaji matengenezo ya mara kwa mara huko Nchini Malawi; jambo ambalo kwa maoni yangu naona ni hasara kubwa sana na inachelewesha muda kwa wasafiri. Je, Serikali ipo tayari sasa kuamua na kuwekeza kwa kununua chelezo yetu sisi wenyewe ili iweze kuwekwa upande wa Tanzania badala kila siku kusafirisha meli kwenda nchini Malawi?

(ii) Hivi karibuni tulisikia kupitia vyombo vya habari kwamba zile meli tatu ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba zitajengwa kwa ajili ya Maziwa matatu zimeanza kutengenezwa. Je, Wizara hii ipo tayari kuhakikisha kwamba meli ya kwanza itakayokamilika itapelekwa huko kwenye meli chakavu kwanza ili iweze kufanya kazi kuwasaldia Wananchi wa Kata za Matema Wilayani Kyela na Wananchi wote waishio katika Mwambao wa Ziwa Nyasa hadi kufikia Mbamba Bay? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cynthia Ngoye, kama ifuatavyo:-

Ni kweli meli hizi mbili zinazofanya kazi katika Ziwa Nyasa zimechakaa na meli zote zipo katika programu ya matengenezo makubwa. Matengenezo ya awali kwa hii MV

Songea ni haya ambayo yataigharimu Serikali shilingi 134,000,000. Tayari shilingi milioni 30 zimekwishalipwa kule na shilingi 134,000,000 zitalipwa.

Suala la kununua chelezo kwa maana ya kuwa tayari kuhudumia meli sisi wenyewe nchini, nadhani ni wazo zuri na mimi nalichukua hili tuweze kuona uwezekano wa kufanya hivyo badala ya kutegemea kwenda Malawi.

Swali la pili, ni kweli taratibu za ujenzi wa meli tatu, moja katika Ziwa Victoria, nyingine katika Ziwa Tanganyika na moja katika Ziwa Nyasa zinaendelea. Wadau wetu wa Maendeleo (*DANIDA*), tarehe 7 Juni, 2012 wamekamilisha upembezi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa hizi meli tatu.

Programu hii itagharimu *Euro* milioni 45. Sasa ombi la Mheshimiwa Ngoye kwamba, meli ya kwanza itakayokamilika ipelekwe Ziwa Nyasa; mimi sina tatizo nalo.

Wajenzi watakapokamilisha meli hiyo, ikipatikana itapelekwa Ziwa Nyasa. Naamini kwamba, ujenzi huu utakwenda *simultaneously*, siyo kwamba itaanza moja baada ya nyingine. Kwa hiyo, tuwe na matumaini kwamba tutapeleka meli hiyo pindi itakapokuwa imekamilika.

Na. 51

Ndoa za Jinsia Moja Mkakati wa Nchi za Magharibi

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Kumekuwa na msimamo mkali wa kimkakati wa Nchi za Magharibi wa kuzitaka Nchi rafiki ya zile zinazopokea misaada kutoka kwao kuhalalisha ndoa za jinsia moja:-

Je, Tanzania ikiwa ni moja kati ya nchi hizo zinazopata misaada mbalimbali kutoka kwa Mataifa hayo imejiandaa vipi

kukabiliana na janga hilo hasa pale nchi hizo wahisani watakapokatisha misaada yao kwa nchi yetu?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali namba 51, la Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Msimamo wa Tanzania wa kuheshimu utamaduni, mila na desturi zake, unazingatia pamoja na mambo mengine, ndoa za jinsia mbili, yaani mke na mume. Utamaduni huo haujabadilika na wala hauwezi kubadilishwa na shinikizo la aina yoyote ile ikiwemo kukatiwa misaada kwani utamaduni ni uhai wa taifa letu na tutaendelea kuulinda daima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, kipengele cha 9(a) kinasema, ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke, wenyе lengo la kudumu katika maisha ya wawili hawa. Hivyo, suala la msingi hapa ni kuwa kulingana na matakwa ya Sheria ya Tanzania ili kuwepo na ndoa inayotambulika kisheria ni lazima kuwepo na pande mbili za jinsia tofauti, yaani mwanamume na mwanamke. Aidha, dini zetu zote za hapa nchini hazikubaliani na uwepo wa ndoa za jinsia moja na viongozi wake wapo kwenye mstari wa mbele kukemea jambo hilli. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo, utamaduni wetu, sheria zetu na dini zetu, hazitambui ndoa ya jinsia moja. Muungano kati ya watu wa jinsi moja, yaani mwanamume na mwanamume au mwanamke na mwanamke mwengine, hautambuliki kabisa kama ndoa kisheria hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi marafiki duniani zikiwemo zile za Magharibi zimeendelea kutuheshimu kutokana na msimamo wetu huo thabiti na usio teteleka kwa kuendelea kutoa misaada ya ushirikiano wa kiuchumi kwa Serikali ya Tanzania.

Nasi tutaendelea kupokea misaada ile tu ambayo haina masharti ya kubadili sera, utamaduni na sheria zetu kuhusu ndoa za jinsia moja.

Mheshimiwa Spika, itakapotokea wahisani wanasitisha misaada kwa sababu ya msimamo wetu, tupo tayari kujifunga mikanda na kujibeba wenyewe badala ya kukubali kudhalilisha utu na utamaduni wetu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Waziri katika jibu lake mwisho amemalizia kwa kusema kwamba, Watanzania tutakuwa tayari kufunga mikanda ili kujinusuru na janga hilo. Nilichotaka kujua, kwa sababu hili jambo linaonekana lipo na linanyemelea, Malawi tayari hapo, wataoana watakuja *honeymoon* Dar es Salaam. Je, ni mikakati gani kama Taifa ya kiuchumi na kwa kutumia rasilimali zetu tutaanza kufikiria kujinusuru na janga hili badala ya kutegemea misaada ambayo inaonekana dhahiri hawa watu wamekusudia?

(ii) Kuna mshairi mahiri aliwahi kughani na akasema: "Fadhila kitu cha maana usiniambie si kitu. Kama huwezi kulipa, usile kitu cha mtu." Je, leo Waziri yuko tayari na kwa ujasiri wa Serikali mahiri ya CCM; kuwaambia Mataifa makubwa ikiwemo Marekani wafikirie kwanza kuondoa misaada yao kwa Tanzania kuliko kufikiria kutuambia tuingie ndoa ya jinsia moja? Tanzania bila ushoga inawezekana. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa ni swali au hotuba tena! Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, naomba ujibu kwa kifupi sana tafadhali.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatib, kama ifuatavyo:-

Tumesema tutajifunga mikanda, katika upande wa uchumi, tutaimarisha uchumi kama ulivyoelezwa kwenye bajeti iliyotolewa mwaka huu, ambayo inaweka kipaumbele katika kukuza nyanda mbalimbali za uchumi. Watanzania wanafurahi kwamba sasa hivi tuna rasilimali kama gesi ambayo imevumbuliwa. Nashukuru sana kwamba, kwa Mkoa wa Lindi tumepata sasa karibu trillioni tatu za gesi ambayo itawasaidia sana Watanzania. Pia ni matumaini yangu kwamba, rasilimali hizi tukiziweka vizuri, hatuwezi kuchezewa na Taifa lolote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, suala hili ni la kisiasa pia. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwaomba marafiki wa watu ambao wanashughulikia na kushabikia sana suala hili, wazungumze nao na waache kuitaniatania Tanzania katika jambo la aina hii.

Na. 52

Hitaji la Ofisi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

MHE. BAHATI ALI ABEID aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kule Zanzibar ikizingatia kuwa Wizara hii ni ya Muungano?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo sasa ni kuwa upande wa Tanzania Zanzibar, masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

yakiwa sehemu ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa, yanaratibiwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa shughuli za Wazanzibari waliopo nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuhuisha Muundo wa Wizara na *job list* kuangalia uwezekano wa kuingiza nafasi za vituo vyta nje ya Makao Makuu ya Wizara, ikiwemo Ofisi Ndogo huko Zanzibar. Baada ya hatua hiyo kukamilika na hali ya fedha kuruhusu, Wizara itaanzisha ofisi hiyo na pia kuangalia namna ya kutekeleza utaratibu huu kwa pamoja Tanzania Bara na Zanzibar.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(i) Kwa kuwa Ofisi hii aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ipo katika maeneo ya Ikulu kule Zanzibar; na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wanajua mazingira ya Ikulu. Je, Serikali sasa haioni haja ya kuiondoa Ofisi hii Ikulu na kuiweka nje ya Ikulu ili Wananchi waweze kupata taarifa muhimu pale ambapo wanazihitaji?

(ii) Ofisi ni pamoja na jengo, wananchi na vitendea kazi, hata kama jengo halipo. Je, wafanyakazi wanaofanya kazi Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki wameajiriwa na Wizara hii?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli ofisi hii inayoratibu mambo ya Afrika Mashariki kule Zanzibar ipo Ikulu na suala hili lilitibainisha kwamba ni tatizo wakati tulipokuwa tunafanya ziara ya kuhamasisha Wananchi baina ya Wafanyabiashara na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Bahati na Watanzania na Wazanzibari kwa ujumla kwamba, jambo hili limefikiriwa na Wizara yetu na tumeshakaa pamoja katika ule mchakato ambao tumeuainisha wa kutengeneza *integration centres* na Ofisi Kuu kule Zanzibar. Wizara yetu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais itatafuta Ofisi nje ya Ikulu ili iwe rahisi kwa Wazanzibari kwenda kutafuta ushauri na kutumia fursa ya mtangamano wa Afrika Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli wafanyakazi wa pale wanaohusika na utaratibu na uratibu wa mambo ya Afrika Mashariki katika Ofisi ya Rais wote ni waajiriwa wa SMZ; lakini kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba sasa hivi Wizara yetu ipo katika mkakati wa kuhuisha muundo wa kuwa na vituo nje ya Makao Mkuu, ambayo ni *integration centre* na Ofisi ya Zanzibar, *job lists* na wafanyakazi. Namhakikishia Mheshimiwa Bahati kwamba, utaratibu huu ukishamalizika, walau wafanyakazi wawili watakaokuwa wameajiriwa na Ofisi ya Afrika Mashariki, watashirikiana na wafanyakazi wenzao pale SMZ kwa ushirikiano wa pamoja ili kutoa faida kwa Wananchi wa Zanzibar.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge si mnaona muda umekwisha tena umepita sana?

Leo wageni wetu walioko katika Ukumbi huu ni wanafunzi 60 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Kinyerezi ya Dar es Salaam. Naomba walimu na wanafunzi wote wasimame walipo; ahsanteni sana. Tunawakaribisheni sana, muendelee kusoma vizuri na wakati mkiwa hapa mtaelekezwa mambo yalioko hapa. Karibuni sana walimu na wanafunzi wote.

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama - Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa tano asubuhi, kutakuwa na Kikao cha Kamati, katika Ukumbi Na. 231. Ningependekeza iwe saa saba, *unless* kama ni saa tano lazima muwe mmeniarifu ni kwa sababu gani. Vinginevyo, vikao vyote vinakuwa saa saba, *otherwise*, ukumbi utakuwa hauna watu. Kwa hiyo, mtakuwa na kikao saa saba, Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana na yeye pia anasema saa tano, hapana. Anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na kikao leo Chumba Namba 227. Yeye pia amesema saa tano, naomba iwe saa saba, ndiyo utaratibu tunaofanya; sikupata maombi maalum kwa hiyo ni saa saba.

Mheshimiwa David Ernest Silinde, Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo saa saba mchana, kutakuwa na kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Halafu, Katibu wa Wabunge wanaotoka Majimbo yanayolima pamba, huyu ni Dkt. Titus Kamani anasema, anawafahamisha Wabunge wote wanaotoka Majimbo yanayolima pamba, watakuwa na kikao leo saa saba katika Ukumbi wa Msekwa B kujadili changamoto zinazokabili msimu wa ununuzi unaotegemea kuanza hivi karibuni. Kwa hiyo, ni wale wa Mikoa inayolima pamba. Wale wenyeviti wa Kamati zile mbili mnaanza saa saba siyo saa hizi, kwa sababu tukienda kwenye Kamati basi Ukumbi utakuwa hauna watu.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mengine mafupi.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwafahamisha kuwa, Kamati ya Uongozi ya Bunge katika kikao cha dharura kilichofanyika Siku ya Jumatatu, tarehe 18 Juni, 2012, iliazimia kufanya mabadiliko ya upitishwaji wa Muswada wa Sheria ya Fedha (*The Finance Bill*) kwamba; badala ya Muswada huo kupitishwa mara baada ya Hotuba ya Bajeti na bajeti kupitishwa, sasa upitishwe mwishoni kabisa mwa Mkutano wa Bajeti wakati Bajeti za Wizara zote zitakapokuwa zimepitishwa. (*Makofi*)

Itakumbukwa kuwa, kwa nia njema utaratibu wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha, mapema ulianzishwa wakati wa Bunge la Tisa ili kuruhusu mchakato wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali uanze kuanzia Julai mosi, badala ya kutegemea Sheria inayoruhusu mapato yakusanywe hata kama Sheria ya Fedha haijapita (*Provisional Collection Tax*).

Hata hivyo, utafiti unaonesha kuwa Mabunge mengi ya Jumuiya ya Madola (*Commonwealth*), yana utaratibu wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha (*The Finance Bill*) na Muswada wa Sheria ya Matumizi (*Appropriation Bill*), mwishoni kabisa mwa mjadala wa Bajeti. Tumefuatilia na kubaini kuwa, mchakato wa kupitia Bajeti unaanza mapema na kumalizika kabla ya Mwaka wa Fedha mpya kuanza. Mathalani Bunge letu lingepaswa liwe linakutana na kuanza mchakato wa kupitia Bajeti ya Serikali mapema na inapofikia Juni 30, Mkutano wa Bajeti uwe umemalizika na Muswada wa Sheria ya Fedha kuanza kutumika ifikapo Julai Mosi, ambapo mwaka mpya wa Fedha unaanza.

Hivyo basi, kwa kuzingatia ombi la Serikali na Waheshimiwa Wabunge walio wengi na maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na kwamba hata pasipo kupitisha Sheria hii bado Serikali inaweza kukusanya mapato; na kwa kuwa Kanuni ya 106 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, bado haikufanyiwa mabadiliko na kwamba utaratibu wa kupitisha Muswada huu mwishoni utatoa fursa kwa Wabunge kushauri

vyanzo vingine vya mapato kama wataweza kushauri kutokana na michango ya Wabunge wakati wa mjadala wa Bajeti; na kwa kuwa kwa kujadili Muswada wa Fedha mwishoni tutatoa muda mzuri kwa Kamati na Waziri wa Fedha kujadiliana kwa undani kuhusu Muswada huu kabla ya kuletwa rasmi Bungeni. Vile vile utaratibu huu ulikuwa unatumika zamani na unaendelea kutumiwa na Mabunge mengi ya Nchi za Jumuiya ya Madola kama nilivyoeleza hapo juu; tumeona ni vyema tuendelee na utaratibu wa zamani unaotamkwa na Kanuni za Kudumu za Bunge ili mawazo ya Wabunge wakati wa mjadala wa Bajeti nzima yaweze kuboresha Muswada huo wa Sheria ya Fedha.

Kutokana na mabadiliko hayo basi, mjadala wa Hotuba ya Bajeti utakuwa wa siku tano badala ya siku nne, ambapo utahitimishwa Siku ya Ijumaa, tarehe 22 Juni, 2012 na Bajeti itapitishwa siku hiyo. Kwa hiyo, naomba Wabunge wote wafike siku hiyo tarehe 22 Juni, 2012 kwa sababu ndiyo tutapitisha Bajeti kwa majina. Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2012 badala ya kupitishwa tarehe 22 Juni, 2012 sasa utapitishwa mwishoni mwa Mkutano wa Nane wa Bunge. Aidha, Kanuni za Bunge zitaendelea kufanyiwa mabadiliko ambayo hatimaye yatawezesha Bunge letu lifuate utaratibu wa nchi nyingine, kwa Mkutano wa Bunge wa Bajeti kufanyika mapema na kumalizika kabla ya Mwaka wa Fedha mpya kuanza. Hii itawezesha Mkutano wa Bajeti uwe umeisha kufikia Juni, 30.

Haya mabadiliko tunaendelea kuyafanyia kazi, pamoja na kuunda na Kamati ya Bajeti na Ofisi ya Bajeti. Sasa hii kuongeza muda kwamba Muswada wa Fedha ujadiliwe mwishoni itategemea. Waheshimiwa Wabunge, mnajadili Bajeti, mnachokifanya sasa mnajadili sijui kulumbana na bahati nzuri nina simu nyingi mno wanazozileta Wananchi wanaeleza masikitiko yao kwamba Waheshimiwa hamjadili Bajeti mnajadili kitu kingine mnachokijua ninyi. Sasa tukiongeza muda kufikiria *Finance Bill* wakati ninyi mnajadili malumbano, hamjaisaidia

Serikali. Jadilini Bajeti; tuongeze mapato vipi, tupunguze matumizi vipi, wapi tufanye vitu kama hivyo na siyo matusi wala kuonesha ufundi wenu wa kisiasa humu ndani; siyo mahali pake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, rudisheni heshima ya Bunge. Nimewaambia mara zote, mnaposimama hapa Wananchi wanawaona mmoja mmoja na waliwachagua wao muwawakilishe, ninyi hamzunguzii shida zao mnazungumzia habari ya kugombana ninyi wenyewe! Nomba mrudishe heshima ya Bunge; jadilini hoja na hoja zimeandikwa vizuri. Bajeti siyo kwamba inakwenda inafukuzwa, siyo *point, discuss* Bajeti hapa halafu wanaosikiliza hapa waende kufanya marekebisho. Naombeni sana mtambue kuwa kila anayesimama hapa Wananchi wake wanamwangalia. Sasa wanaanza kusikitika; huyu tulimchagua wa kazi gani huyu? Jamani hebu jihurumieni wenyewe.

Tunaendelea na shughuli inayofuata.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. PAULINE P.GEKUL: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Mwongozo wa Spika kuhusu maneno niliyosema mimi? Haya! (*Kicheko*)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 68(7), inayosema kwamba, Mbunge yeoyote anaweza akasimama na akaomba Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako...

SPIKA: Halafu soma mpaka mwisho hilo neno, maana tunatumia Mwongozo wa Spika, kumbe haisemi hivyo mpaka mwisho.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, naomba nisome: "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako katika Kanuni ya 64(a) inayosema: "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Naomba mwongozo pia katika Kanuni ya 114(8) inayosomeka hivi: "Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, kila Kamati itajiwekea utaratibu wake na Kamati inaweza kuwaruhusu Wabunge ambao siyo Wajumbe wa Kamati au watu ambao siyo Wabunge kuhudhuria na kushiriki katika shughuli za Kamati, lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura."

Jana wakati mjadala wa Bajeti unaendelea humu ndani, Mjumbe mmoja wa Kamati alilipotosha Bunge kwamba, Kamati ya Huduma za Jamii, haijawahi kukataa Bajeti ya Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu. Pia, aliweza kuzungumza kwamba, hawa Wapinzani wanaingia kwenye Kamati ambazo siyo zao wakati Kanuni inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba mwongozo wako ni kwa jinsi gani ambavyo Mjumbe huyu analipotosha Bunge hili, wakati vielelezo vinaonesha na mpaka magazeti ya jana na vyombo vyahabari vimeripoti kwamba, Mheshimiwa Sitta afichua siri ya Bajeti ya Wizara ya Afya. Imeelezwa ni kwa jinsi gani ambavyo Kamati illieleza Serikali kwamba, wamalize

mazungumzo na Madaktari kuhusu migogoro hii ya Madaktari na migomo ili kuwanusuru wananchi wasiendelee kufariki.

Mheshimiwa Spika, hii imesababisha Mjumbe mwenzetu kutoa maneno ya uwongo wakati Kamati ikieleza msimamo huu tukiwa Mlandizi, Siku ya Jumamosi, Dar es Salaam. Mjumbe huyu alikuwa kwenye Mkutano wa Hadhara wa CCM, wala hakuwa kwenye Kamati, lakini humu ndani anasema kwamba, Kamati haijawahi kukataa bajeti hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Ukiomba Mwongozo wa Spika, halafu ikawa hotuba; nasema mwongozo unatakiwa uwe *very specific*, sasa ninyi mnaanza kutoa hotuba. Kwa kweli ni lazima nikiri, mahali ambapo tunatumia vibaya kifungu hiki ni kwenye mwongozo na tunakula wakati mzuri sana wa kufanya majadiliano. (*Makofi*)

Sasa, ukweli ni kwamba, mimi mwenyewe katika kubadilisha Kanuni tutaangalia, Mawaziri Vivuli, wasiwe Wajumbe wa Kamati zinazohusika; hili tutaliangalia. Pia ni kweli kwamba, Mbunge ye yeyote anaweza kuhudhuria Vikao vya Kamati zingine. Kwa hiyo, ile kusema kwamba tumesema maneno ya Kamati msiyaweke *public*, mtakuja kutuambia sisi. Sasa kama mlikuballana kukataa bajeti, sisi kule haituhusu kabisa; ndiyo mtaendelea kufanya hizo Kamati na mtaleta hapa Bungeni. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana tuwe waangalifu kutumia kifungu cha mwongozo, tunakula muda wa kazi. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba, Mbunge ye yeyote anaweza kuhudhuria Kamati yoyote. Baadaye katika Kanuni tutaangalia, Kanuni za sasa hazisemi hivyo, lakini baadaye tutaangalia Mawaziri Vivuli wasiwe Wajumbe wa Kamati zile kwa sababu anakuwa mmoja wa waamuzi. Kanuni inasema Kamati

itakubaliana kutoa maamuzi yake Bungeni iwapo mbili ya tatu ya Wabunge wamekubaliana na hiyo hotuba.

Sasa anakuja hapa Mjumbe mmoja ambaye ni Mjumbe wa Kamati, anatoa kinyume na vile alivyokubaliana na wenzake, siyo sahihi. Hivyo ndiyo tunavyosema na hamuwezi ku-*challenge* kwa sababu hiyo ni kweli.

Tulipoamua kuunda Kamati zile, nilikuwa mimi nimeshaunda Kamati, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, akawateua watu wake, tusingeweza kumzuia kwa sababu hakuna kifungu kinachomzuia kufanya hivyo, lakini *in future* ni lazima hili tuliangalie.

Tunaendelea na hatua inayofuata; Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Deo Filikunjombé, atafuatiwa na Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, atafuatiwa na Mheshimiwa Salvatory Machemli, hawapo wote? Atafuatiwa na Mheshimiwa Henry Shekifu. Mheshimiwa Shekifu naye hayupo? Atafuatiwa na Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran; yupo?

Tuanze na Mheshimiwa Nassir, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shekifu halafu Mheshimiwa Machemli.

MHE. YUSUPH A. NASSIR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Inawezekana nina rangi ya kufifia kidogo, ndiyo maana hukuniona.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nataka kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha kwenye hatima hii ya ku-*discuss* au ya kuchangia hoja hii ya Bajeti yetu. Napenda kuishukuru Wizara ya Fedha, hasa pale walipofanya jambo la makini kabisa la kutoa mafao ya watu wa mikongeni. Naomba kuipongeza sana Wizara ya Fedha na Serikali. Nimepata taarifa kutoka mashamba ya Mgombezi na mashamba ya karibu ya kwamba, sasa karibu asilimia 80 ya mchakato ule imekamilika na watu wameanza kupokea pesa zao. Nazishukuru sana Wizara ya Fedha, Waziri aliyeidhinisha na Uongozi mzima wa Wizara na Mashirika yanayohusika. Kilio cha watu wa mikongeni kilikuwa kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafao ya watu wa mikongeni, yalicheleweshwa kwa miaka mingi. Ushauri wangu kwa wana Mgombezi na watu wa mashamba ya karibu, pokeeni kile mllichopewa na mkihisi kwamba, ipo haja ya kudai *time value* kwa pesa zilizocheleweshwa, basi msisite kuandika na kuomba nyongeza kwa ucheleweshaji uliotokea.

Mheshimiwa Spika, ningependa niende moja kwa moja kwenye Bajeti yetu. Kuna mahali ambapo tumekuwa tukikaa kwenye Halmashauri zetu na kujadili Bajeti; imedhihirika karibu asilimia 90 ya kile ambacho tunakiomba, huwa hakiendi. Halmashauri ya Mji wa Korogwe, imepata kiasi kidogo sana cha pesa mwaka huu. Tumeshindwa hata kuendesha maeneo muhimu kabisa ya huduma za jamii, kwa mtindo uleule ambao tunapewa *ceiling* wa kuambiwa kwamba msifikie. Tatizo kubwa linalokuja kujitokeza hapa ni mahitaji makubwa yaliyoko katika Halmashauri zetu. Badaye tunakuja kuambiwa kuwa, mahitaji yote mengine ya ziada tupeleke *special request*.

Mheshimiwa Spika, ningependa niishauri Wizara ya Fedha kuwa, kuweka *ceiling* ni sawa, lakini suala la kupeleka mahitaji mengine ya msingi na changamoto zinazoibuka siku baada ya siku kwenye Halmashauri zetu. Kwa mfumo huu wa kupeleka *special request*, unatufanya turudi tena kwenda kupiga magoti *Treasury*. Sasa tunakuwa na Bajeti ambayo tumeipitisha ndani ya Bunge, lakini inakuwa haikidhi mahitaji ya Halmashauri zetu. Tunalazimika tena kwenda *Treasury* kupiga magoti na kuomba gari la taka na gari la maji taka. Amekuwa akisimama hapa Mheshimiwa Mwanri, kwa muda mrefu, akitoa macho anapokumbana na maswali ya Wabunge yanayohusisha maendeleo kwenye Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, sasa hii huwa haitoshi; kutoa macho pekee hakutoshi, inabidi atoke na aende akawaambie *Treasury*, tusimame pamoja ndani ya Bajeti hizi tuone kwamba, kile kinachopangwa hakikidhi. Hivi juzi tu haina hata mwezi mmoja, Wananchi wa Korogwe Mjini, walitaka kumkamata kumpeleka sokoni, akashuhudie rundo la takataka na maombi yao yaliyokaa kwenye Wizara ya Fedha zaidi ya miaka mitano na mpaka sasa gari la takataka halikupatikana.

Mheshimiwa Spika, hii siyo sahihi, tuambiwe yale yaliyo ya kweli. Bajeti za Halmashauri na mahitaji na changamoto zinazokuwa siku baada ya siku ni lazima ziwe *addressed*.

Mheshimiwa Spika, tunakaa tunajadili Bajeti hapa. Kuna maeneo mengi ya kukuza kipato, kuna maeneo mengi ya kuongeza tija, lakini pia kuna pesa za Serikali ambazo zimekaa tu mikononi mwa watu. Nitatoa mfano wa dola milioni 28 ambazo zimekaliwa tu na Kampuni ya *Pan Africa Energy*; zile zingeweza kutoa msaada mkubwa kabisa, lakini majibu ya Serikali wakati wa kufuatilia suala lile, kilichotokea ni kwamba, tumeambiwa inaitwa *Government Negotiation Team*. Huyu alipaswa atulipe juzi, jana na leo; *negotiations* ni za nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni haki ya Serikali; kwa nini tumeamua kuunda timu kuongeza ukiritimba mbele yetu? Wizara ya Fedha, mmekuwa mkiitumia *TRA* kwa ajili ya kukusanya mapato. Mmekuwa mkiitumia *TRA* kwa ajili ya kudai haki za Serikali. Itumieni iende ikachukue milioni 28 zilizoko *Pan Africa Energy*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, tuna maeneo mengi mengine ya kuangalia. Nimejaribu kufungua Kitabu cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nikaangalia Sekta ya Ardhi. Tumekuwa na changamoto ya Miji na Vitongoji vinavyokua hasa kwenye maeneo ya zamani niyaite maeneo ya kikoloni, yaliyokuwa yakilima mazao ya mkonge. Tunahitaji tuone kumetengwa pesa za kutosha za kufanya *survey* iliyo sawa, Vitongoji vya katikati na pembezoni viweze kupata ardhi stahiki na vitambulike vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *Inland Container Depot (ICD)*. Ukiingalia Dar es Salaam ya leo, imekuwa na *out burst* ya *congestion* ya *ICD*. Kwa taarifa iliyofanywa na *study* iliyofanywa na *World Bank, USAID* na wadau wengine, wameelekeza kabisa kwamba, *ICD* zote ni vyema zikawa si chini ya kilometra 100 kutoka maeneo ya bandari. Sasa basi, tujaze *ICD* kwenye ukanda wa bandari ambao hatimaye unalazimisha msongamano mkubwa wa magari na hata kazi za kijamii na za Kiserikali hazifanyiki vizuri; ni vyema sasa tuangalie upya kuzisogeza maeneo ya Chalinze au hata kupita Kibaha. Hii itatusaidia sana kupunguza msongamano uliopo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, kupata na maeneo makubwa ambayo tutaweza kusema sasa tuna-*designate* mzigo wote unaokwenda Zambia ukae mahali hapa. Chalinze ni mahali *ideal*, wanaotaka kupeleka Zambia, wataanzia pale, kilometra 100 nje ya Mji ili kuwafanya wakazi na wanafunzi, akina mama na wazee wa Mkoa ule, waweze kufanya kazi zao kiurahisi na hata Serikali kufanya kazi za kiutendaji mapema. Sisi

ambao tunakuwa na fursa na kazi za pale mjini, ukitaka kuwahi kabla ya saa mbili ni lazima uamke baada ya swala ya alfajiri (saa 11.00) ndiyo utaweza kufanya kazi zako. Hata kwenda Ofisi za Bunge wakati wa Kamati, inabidi lazima utoke nyumbani kwako kuanzia saa 11.30 au saa 12.00 kwa wale ambao tuko maeneo ya karibu kwa sababu msongamano ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hayo ni ya kuyaangalia. Pia tungeweza hata kuisaidia reli kwa sababu *Intergrated Program* ya *ICDs* na *Port Authorities*, kwa *study* iliyofanywa, inatueleza kwa kina kabisa, wafadhili wale wapo, tuweze kuona basi tunawezaje kuitumia reli hiyo ya Dar es Salaam mpaka Ruvu. Vilevile tutengeneze *side line* kuelekea Chalinze kwa ajili tu ya *transit goods* peke yake ili kuufanya Mji wa Dar es Salaam uwe wazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, suala la kupanda kwa bei ya vyakula katika baadhi ya maeneo nchini mwetu kunatokana pia na kufa kwa reli; ni vyema Wizara ya Mawasiliano, ikaongezewa fedha kwa ajili ya kufufua reli ambayo imekufa. Mathalani, ilikuwa tukikaa pale llala tunaona mizigo mingi ya vyakula ikitoka kwa madebe mawili mawili, matatu, manne au hata matano na hata mizigo mikubwa kwa sababu ya *goods*, sasa hivi hilo halipo. Ujisikia mabehewa tuliyokuwanayo utaambiwa haya ni *designated* na ni machache. Tuangalie ni jinsi gani kwa *program* za Kiserikali zilizopo *under Public Private Partnership*, tutaweza kuongeza nguvu ili walau basi hata wale wakulima wadogowadogo ambao sasa hivi magari hayafiki kwao, lakini kuna reli ya zamani, waweze kutoa mchango na hata kupata nguvu ili kilimo kiweze kupata tija kwao na hatimaye kupunguza mfumko wa bei za vyakula katika Miji na Vitongoji mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la jinsi gani Bajeti yetu ya sasa itawezekana kuangalia uwezekano wa mapato

yatakayotokana na rasilimali zetu kama madini na hasa gesi ukizingatia kwamba na sisi tumeingia kwenye Programu ya *Extractive Industry Association (EIATA)*. Katika mambo makubwa ambayo tumeweza kujifunza kwa kipindi kifupi ni kuona kwamba, mapato haya yanayotokana na rasilimali zetu, hayataingia kwenda ku-cover matumizi yetu moja kwa moja. Mapato haya ni lazima kwanza yatumike kujenga miundombinu kwa ajili ya maendeleo yetu. Haya ni mambo ambayo tumejifunza katika maeneo mbalimbali na hatuna budi kuishauri Bajeti ya sasa na Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii. (*Makof*)

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Watanzania wanachotaka kuona sasa hivi ni maisha bora na mabadiliko makubwa ya maisha yao. Falsafa kubwa ya Chama kilichoko madarakani ni Maisha Bora kwa Kila Mtanzania, lakini tunachokishuhudia leo ni kuchana Bajeti na kuzitupa huku hatulengi kuwasaidia Watanzania. Falsafa hii haina mashiko kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kokote, nigusie wananchi wangu wa Jimbo la Ukerewe. Wamenitura nisikubaliane na bajeti hii na wamenitura kwa sababu katika Bajeti, uvuvi na mifugo imetengewa shilingi bilioni 192. Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hilli, sasa kama uti wa mgongo unaumwa *meningitis*, utabakije salama? Kilimo kinaumwa, uvuvi unaumwa uti wa mgongo. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Ukerewe leo hawana pa kushika kwa sababu wamegoma kutokana na mwanguko wa bei ya samaki. Ninavyosema hapa leo Bungeni, wavuvi hawavui sangara kwa sababu wale Wahindi wenye viwanda wameamua wao wenyewe binafsi kugoma, wakashusha bei ya sangara kutoka shilingi 5,000 mpaka shilingi 2,500. Kwa wale wanaonunua sangara kule Ziwani, wameshusha kutoka shilingi 3,000 mpaka shilingi 1,500; ni anguko la asilimia 50. Sasa

nitaungaje mkono Bajeti wakati wananchi wangu wanakufa na njaa?

Mheshimiwa Spika, sina zao lingine, silimi pamba wala kahawa, mimi ninavua. Sasa kama uvuvi wenyewe umeanguka kwa asilimia hizo na Serikali ilikuwa inategemea Bajeti kubwa, ilikuwa inategemea sana zao la samaki, tulikuwa tunasafirisha sangara kwenda Ulaya; leo wavuvi wamegoma hawaingii majini, Serikali imenyamaza kimya; hivi siyo kuumwa huko? Hiyo siyo *meningitis*? Siyo uti wa mgongo huo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kukubaliana; Kimsingi, tunakaa hapa ndani tunajadili mambo mengine ambayo hayana mashiko. Tunaanza kuchanana ovyoovyo wakati tunaiangalia nchi hii inakwenda pabaya. Wabunge tunasimama tunaanza kuongea mambo ambayo hayana mashiko. Naiomba Serikali itoe tamko kuhusiana na wavuvi wa Sangara katika Ziwa Victoria kwamba tunawasaidiae. Tunaisaidiae Serikali kukosa pesa za kigeni kwa sababu ilikuwa inasafirisha sangara kwenda Ulaya. Ninawaomba Wabunge wengine tunaotoka Kanda ya Ziwa, akiwemo Mheshimiwa Wasira, tuungane kutetea hili suala, tusiwe tunaleta bajeti nyininge ambazo hazitusaidii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Kusini, walijadiliana kuhusu kahawa, wenzetu wa Kaskazini walijadiliana kuhusu mazao yanayowasaidia. Sisi Kanda ya Ziwa tumenyamaza kimya, wakati watu hawaingii majini, hawavui samaki kwa sababu Wahindi wameamua. Serikali gani hii ambayo Wahindi wanajadili tu wenyewe leo tunaamua tufanye hivi, wanafanya wanavyotaka, halafu Serikali imenyamaza kimya, imelala usingizi inakoroma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, nikiachilia mbali zao la sangara, uvuvi, sambamba na wale wanaolima pamba, Wabunge wanaotoka kwenye Kanda inayolima pamba, wamepiga kelele sana hapa Bungeni, wanalamika pamba

inashuka kwa shilingi 1,000 tu. Wanaiomba Serikali iwaongezee angalau wananchi wale wapate maisha bora kwa kila Mtanzania yanayopigiwa kelele na ninyi wa Chama hicho. Bahati mbaya zaidi, hakuna anayewasemea.

Nchi gani inaweza kuendelea bila kuwa na viwanda wala bila kuzalisha? Tulikuwa tunategemea viwanda nya pamba hapa nchini, tulikuwa na viwanda Mwanza (*MWATEX*), Musoma (*MUTEX*) na Morogoro, vyote sasa hivi havipo hatuzalishi; ni nchi gani ambayo haizalishi halafu ikapata maendeleo? Ni mufilisi. Serikali mufilisi haiwezi kuendelea kwa kuagiza vitu kutoka nje, haiwezekani, hatuwezi kuendelea kama tutakuwa tunaagiza vitu kila siku kutoka nje, viwanda vyetu tumeuza, halafu watu wanavibadilisha. Morogoro pale kulikuwa na kiwanda cha ... tumempa Mheshimiwa mmoja yuko hapa ndani ana fugia mbuzi, halafu Serikali imenyamaza kimya haimgusi! Tunatafuta kinga ya Bunge, wanaingia Bungeni kwa ajili ya kujificha. (*Makof!*)

Hatuwezi kuendelea kwa staili hiyo; tuwe wazi tufufue viwanda vyetu, tupate maendeleo. Jimboni kwangu kuna kiwanda kilikuwa kinazalisha mafuta ya pamba, leo kiwanda kile kwa sababu hatulimi pamba kimekaa *idle*. Kibadilisheni basi, kama kuna uwezekano Serikali ibadilishe kile kiwanda baada ya kusindika mafuta basi kiweze kusindika mazao ya matunda. Ukerewe tunalima matunda mengi, kuna machungwa na mananasi. Ukerewe kuna kila aina ya matunda, badilisheni kile kiwanda basi kiweze kusindika matunda, maana kimekaa pale popo wanazaliana mle, mijusi ndiyo kibao halafu Serikali tunasema kilimo ni uti wa mgongo; uti wa mgongo gani? *Meningitis*, uti wa mgongo unaumwa huu hatuwezi kuendelea kwa msingi huu.

Mheshimiwa Spika, elimu; kwa kuwa tumepanua wigo wa *skill development levy* wa kuwahusisha Wafanyakazi wa Serikali na Mashirika ya Umma; ni vyema suala la mikopo likafutwa na Serikali kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa sababu watakuwa

wanasoma kwa kodi. Kwa nini kodi iwe *involving* kama mikopo? Hapo ndipo hoja ya elimu bure inapokuwa na mashiko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, juzi wakati Mheshimiwa Zitto anasoma Bajeti, kuna Mheshimiwa mmoja alifikia hatua akaichana chana ile Bajeti wakaitupa mbali. Naomba ninukuu; kama wanafunzi wetu wasoma kwa kodi basi tuangalie upya mfumo wa wanafunzi wa elimu ya juu, fedha inayopatikana kwenye kodi hii itumike kusomesha kwa *grant*, wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi darasani na kupunguziwa mzigo wa mkopo. Vilevile tunaangalia kama tunaweza kukopesha wanafunzi malazi na chakula tu na kutoa bure ada na mafunzo kwa vitendo pamoja na vitabu.

Mheshimiwa Spika, kama wanafunzi wetu wanaosoma elimu ya juu wanaweza kulipiwa kwa kodi ya wafanyakazi wa Serikali ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

SPIKA: Haya ahsante.

MHE. SALVATORY N. MACHEMLI: Mmmh!

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru na ninakuomba radhi kwa sababu jana na juzi nimetafutwa lakini nilikwenda mazikoni nilifiwa na dada yangu.

Nianze kwa kumshukuru Mungu na pengine nianze na utani kidogo kwa sababu nazungumza ...

SPIKA: Unazungumza kwa dakika kumi.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Dakika kumi?

SPIKA: Ndiyo.

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mimi nitazungumza kwa kifupi tu, niseme kwamba, pengine kwa sababu saa nyingine tunazungumza, lakini ni mchezo ambao jana nilimsikiliza Baba wa Taifa katika mawazo yake akizungumzia demokrasi na alikuwa anazungumza na waandishi wa habari mwaka 1992. Ninakubali demokrasi, lakini ni lazima tuwe na demokrasi inayozingatia mazingira yetu. Kwa hiyo, nawaomba wenzetu walioko upande wa pili, wanazungumza vizuri na mimi nakubaliana nao, lakini tunaposema kwa mfano maisha bora kwa kila Mtanzania, hatusemi kutoa fedha kumgawia kila mtu. Hakuna Bajeti duniani ambayo utaitengeneza umpe kila Mtanzania fedha; haipo, hata Marekani ambao ni matajiri hawana. (*Makofi*)

Tunaposema maisha bora kwa kila Mtanzania ni kufikisha zile nyezo za kumletea maendeleo Mtanzania. Leo ni nani anapinga kwamba Serikali iliyoko madarakani inachimba barabara nchi nzima, inasambaza maji nchi nzima, inajitahidi kutengeneza Bajeti kama hii ambayo amesema Waziri? Waziri ame-*address* matatizo yaliyoko ya changamoto tulizonazo sasa na akazitaja vizuri sana. Amezungumzia mfumko wa bei, amezungumzia umeme, amezungumzia usafirishaji na uchukuzi, amezungumzia maji safi na salama, amezungumzia mawasiliano mazuri. Nani asiyekubali leo Tanzania ni nchi ya kwanza katika mawasiliano katika Afrika? *Data* zipo, unakwenda mahali popote unazungumza. Hata Ulaya tunawashinda, mimi nimekaa Uhlanzi ni maeneo machache unaweza ukazungumza na simu unaonekana *luxury*, lakini sisi kwa uchumi wetu tumeweza kuwasiliana.

Ninamshukuru Waziri wa Fedha na nianze kumhakikishia kwamba, Bajeti yake inapita asipate *pressure*. (*Makofi*)

Afanye mema makubwa kiasi gani; ame-*address* matatizo tuliyokuwa nayo, ametoa majibu ili tutakavyoweza

kuendelea tuweze kuyatatua haya tuweze kusonga mbele, tuongeze fursa za umeme. Napenda kusema pengine mimi nimshauri Waziri na sikuwa na *figures* na bahati nzuri wenzangu wamezungumza vizuri, nimshauri Waziri katika mambo yafuatayo ili kuboresha bajeti:-

Kwanza, nimwombe kuwepo na mambo yafuatayo na ayasimamie vizuri:-

Nidhamu ya matumizi ya Bajeti; ni lazima kuwe na nidhamu katika Bajeti. Tunachobajeti humu ndani kitoke tukitumie. Nikuombe Mheshimiwa Spika, mapema sana tuunde ile Kamati yetu ya Bajeti ifuatialie fedha tunazoidhinisha hapa na zionekane zinatumika na kama hazitumiki tupate sababu, ndiyo kazi ya Bunge. Maneno yasiwepo jamani, tutawaingiza kwenye mchezo mtashindwa na uzee huu au yejote hapo aingie kwenye mchezo wa mpira, ukiwa huko nje unashabikia kweli, ingia pale uone utakavyoanguka anguka. (*Makof!*)

Nimwombe Mheshimiwa Waziri, matumizi yetu yaendane na ukweli katika maeneo. Juzi juzi sisi tulikwenda kutembelea barabara, kwa kweli taarifa tulizopata hazilingani na ukweli uliopo katika maeneo. Kwa hiyo, tunaomba Waziri wa Fedha, ahakikishe kwamba, kama fedha za barabara zimebekwa, basi barabara ifikie viwango vinavyotakiwa. Nidhamu kama nilliyosema, matumizi ya Bajeti tusiingize matumizi yasiyokuwepo, hata ikiwa ni dharura kiasi gani tusikate fedha za maendeleo. (*Makof!*)

Kwa sababu maendeleo ndiyo kichocheo, leo tunakopa tutalipaje kama hatutengenezi reli maana reli ndiyo chombo cha uzalishaji? Leo ukiwa na treni tano kwa siku zinakwenda Kigoma, Mwanza, zinatoka Bandari ya Dar es Salaam, utapata fedha nyingi mno. Katika nchi zote ukubwa kama Tanzania, ukienda India reli ndiyo uti wa mgongo, Serikali imesema wameweka bajeti kufufua. Sasa tunaanza kuuliza huko nyuma reli, samaki, ndiyo tutauliza tulikuwa tumebadilisha sera tulikuwa

katika sera ya kuongoza kwa umma. Sasa tunasema tuwakaribishe wawekezaji binafsi, hawa hawaji kama maji ni lazima tukawatafute, tujenge mazingira mazuri ndiyo watakuja. Tukilaumu hatuna majibu ya msingi.

Mimi nakushukuru Mheshimiwa Waziri, umepunguza viwango vya kodi kwa wale wanaotengeneza *juice*, matunda, kwa viwanda vya nchini shilingi nane, kwa viwanda vya nje wanaoleta matunda watachajiwa shilingi 83. Mimi ninayetengeneza *juice* hapa Tanzania nitachajiwa shilingi nane kulipia Mfuko wa Kodi ya Serikali; hayo ndiyo mazingira mazuri. Kwa hiyo, nitatafuta wawekezaji waje Lushoto, wayaweke matunda yale waya-*process*; ni rahisi kuwapata kwa sababu tutawaambia tumeponguzza kodi watakuja na ndiyo mazingira ya bajeti tunapaswa kuipongeza Serikali. (*Makof!*)

Nimwombe Waziri, *Private Sector* bado katika Bajeti haijapewa nafasi ya kutosha; vivutio hakuna, bado hatujaweka vivutio, unajua mwekezaji ni mtu ambaye anataka umpe mazingira ya kuja. Leo tuna bia za kumwaga, tulikuwa tunagombana, mimi nilikuwa mtu mkubwa sana katika biashara ya ndani, ilikuwa ni masikitiko; nilikuwa kiongozi ndiyo lakini leo bia ni za kumwaga. Tuliweka mazingira, tuka-*privatize* na tukafanikiwa kama tulivyofanikiwa leo.

Kwa hiyo, naomba Waziri aongeze mazingira ya kuwakaribisha wawekezaji na Watanzania tujifunze kukaa na wawekezaji duniani kote ndiyo tutafanikiwa. (*Makof!*)

Of course, hatupendi kuwakaribisha wawekezaji wa kuja kutudhalilisha. Hiyo lazima tukubali, siasa zetu na sera zetu lazima tuheshimu kanuni na desturi za kuheshimu Watanzania. Huyu anayekuja na akaheshimu desturi zetu tumkaribishe. (*Makof!*)

Namwomba Waziri wa Ardhi kuwa tuwe na *Land Bank*. Mwekezaji leo akija atakuuliza ardhi kama huna hatakuja.

Sasa hizi ndiyo sera ambazo tunazzungumza, tuweke akiba wananchi wetu wasinyanyaswe. Tuweke maeneo ya uwekezaji ijulikane wakija tunawapeleka huko, hatuwezi kujenga ajira bila kujenga mazingira ya ajira na ajira kwa leo usidanganyike, hata kama Serikali ikitaka kuajiri, ajira itatoka *private sector* na itatoka kwenye viwanda; si vinginevyo. (*Makofi*)

Sasa leo mtu anakuja hapa anasema kuna eneo moja lilisemwa kwamba Bajeti haikuzingatia ajira, ndiyo sasa kuzingatia ajira ni kujenga mazingira ya kuleta ajira. Kilimo ndiyo mwajiri mkuu. Kuna aliyetania kwamba *meningitis* sasa *meningitis* ukiwa nayo si lazima utibiwe; hivi tukunyonge kwa sababu una *meningitis*? Tunaimarisha kilimo kwa kuleta matrekta, yako pale kanunueni tumeshusha bei; unataka tukupe dawa gani? (*Makofi*)

Mmoja alikuwa anasema jana *power tiller* zilikuwa hazifanyi kazi, Waziri amemruhusu Waziri Mkuu kama kwenu *power tillers* hazifanyi kazi, basi acheni nunueni mnachoona kitawasaidia katika kilimo, ndiyo uongozi na hakuna aliyelazimisha katika hili. Ninasema ndugu zangu Upinzani ni mchezo hata mimi ningekuwa kule ningesema haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Masoor Shanif, naona hayupo. Nitamwita Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Vilevile niseme kuwa, sikuwepo baada ya kufiwa na bibi yangu Kija Luhaga na Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya kipenzi bibi yangu; Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema la kwanza kabisa siungi mkono Bajeti hii iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, kwa sababu kuu zifuatazo:-

La kwanza, mapato yetu ya ndani kufikia mwezi wa tatu yalikuwa asilimia 98, mapato yanayotokana na mikopo na misaada yalifikia asilimia 62 kwa mwaka, lakini matumizi yetu yalifikia asilimia 87 kwa kipindi hicho. Halmashauri zilikuwa chini ya asilimia 30 kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi zilikuwa chini. Sasa haya matumizi yanayozungumzwa ya asilimia 87 hayawiani na matumizi yalivyo fedha zinakopelekwa. Kwa hiyo, Serikali kama Serikali ilitakiwa kuondoa utata huu. (*Makofii*)

Yaletwe maelezo ya kutosha Bungeni ili lithibishe kama fedha zilizokuwa zimetengwa kwa matumizi ya mwaka jana zimeenda kwenye maeneo gani na kama hazikuenda katika maeneo ambayo tulikubaliana kwenye Bajeti ziko wapi na kwa idhini ya nani? (*Makofii*)

Sababu ya pili ya kutokubaliana na Bajeti hii ni kwamba, Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi na Mkuu wa Hesabu za Serikali mpaka tunaingia za mwaka 2009/2010 na mpaka tunaingia kujadili Bajeti hivi leo, Bunge lako halijaona majibu ya Serikali dhidi ya Hoja hizo za Ukaguzi za mwaka 2009/2010. Hiki ni kinyume cha sheria ya nchi ambayo tulipitisha, *The Public Audit Act* ya 2008, kifungu cha 40, ambapo Kifungu cha 40(1) kinasema; *the Accounting Officers shall respond to the Controller and Auditor General's Annual Audit Reports and prepare Action Plan of the intended remedial action for submission to the Pay Master General.*

Kifungu kinachofuata cha pili kinasema; *on receipt of the responses and actions, the Pay Master General shall submit to (a) Minister who shall lay it before the National Assembly in the next session. (b) Controller and Auditor General, a copy of consolidated response and Action Plan.* Haya yote hayajafanywa na Serikali; kwa hiyo, siyo halali Bunge hili kuanza

kujadili Bajeti mpya wakati hoja zilizozungumzwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hazijajibwa kwa kufuata Sheria yetu ya Ukaguzi ya Mwaka 2008, kifungu cha 40, ukisoma (i) mpaka (iii).

Kwa hiyo, Serikali imevunja sheria kwa kutolitendea haki Bunge hili ili lijiridhishe kwamba, fedha za Watanzania ambazo tumezigawa zimefanyaje kazi tulikozipeleka; na kama kuna malalamiko ambayo yalioneshw na Mkaguzi, Serikali imeyajibu vipi ili Bunge hili linapoingia kwenye Bajeti leo liwe na uhakika kwamba kule linakotaka kuziidhinisha tena fedha za Watanzania zitaenda kufanya kazi. Kwa kuvunja Sheria namani hii Serikali ingekuwa imeshapelekwa Mahakamani kwa sababu ukivunja Sheria na Sheria hii inasema unapoivunja unatakiwa ufanye nini.

La tatu, umbile la Bajeti na matarajio ya Watanzania. Bajeti hii tuliyowasilishiwa siyo sahihi kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo na kwa mujibu wa Bunge tulivyokubaliana mwaka 2011, mwezi wa sita. Umbile la Bajeti tulikubaliana mambo ya msingi; la kwanza katika Mpango wetu wa Maendeleo tutautekeleza vipi. Tulikubaliana Bajeti yetu kila mwaka wa fedha tutahakikisha tunatenga fedha zetu za ndani shilingi trillioni mbili nukta saba kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, fedha za ndani. Vilevile tukasema walau asilimia 35 ya fedha zetu za Bajeti ziende kwenye Miradi ya Maendeleo.

La tatu, fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo zisitumike kwa kitu kingine chochote. Sasa nasema Bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, imekiuka Azimio la Bunge kwa sababu haikuzingatia hayo yote; badala ya kutenga shilingi trillioni mbili nukta saba kwa ajili ya shughuli za maendeleo, Bajeti ya Serikali imewasilishwa ikiwa na shilingi trillioni mbili nukta mbili kwa ajili ya shughuli za maendeleo. (*Makof*)

Vilevile uwiano wa 35 kwa 65 haukuzingatiwa. Asilimia iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, matumizi ya kawaida ni asilimia 70 na matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni asilimia 30, kinyume na Maazimio ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi ni kwamba, katika mwaka huu wa fedha, mapato yetu ya ndani yameongezeka kwa shilingi trillioni moja nukta tano. Matumizi ya Serikali yakapanda kwa shilingi trillioni moja nukta tisa, wakati Miradi ya Maendeleo ikipunguziwa fedha katika Bajeti shilingi bilioni 397.8. (*Makof!*)

Hii siyo haki na ndiyo maana nasisitiza kwamba, bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha imekinzana na Azimio la Bunge na imekinzana na yale tuliyokubaliana katika Mpango wetu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukifanya utafiti utagundua kwamba, katika matumizi yetu ya kawaida, shilingi trillioni 3.6 ndiyo fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, yaani shilingi trillioni 3.6, lakini katika shilingi trillioni 3.6 yapo matumizi ambayo hayaepukiki na mimi nakubaliana nayo, yapo shilingi trillioni mbili. Shilingi trillioni 1.6 inaweza kabisa ukai-*adjust* ukapata fedha ukapeleka kwenye Miradi ya Maendeleo. Kinachokosekana ni nia ya dhati tu, wakati Watanzania wakisubiri tuongeze utoaji kasi ya utoaji wa huduma, tuongeze uwekezaji, lakini leo hii tunakusanya mapato yasiyolingana na mahitaji ya Taifa hili. Tumekuwa na Mipango yetu ya namna hii ya siku nyingi na Serikali ilituletea Mpango huu, Baraza la Mawaziri liliupitisha Mpango huu, lakini leo tunaingia kuu-*deny* sisi wenyewe. Kama Mheshimiwa Rais amekosa watu wa kumsaidia Serikalini, basi Bunge hili limsaidie kwa kuikataa bajeti hii mpaka pale watakopokubaliana na maazimio tuliyokubaliana na shilingi trillioni 2.7 kupangwa kwenye shughuli za maendeleo. Hatuwezi kuendelea na mzaha wa namna hii.

Nina Kitabu cha Dira ya Maendeleo, soma ukurasa wa 13; Watanzania wamejijengea sifa ya kutayarisha na kujitangazia

Mipango, Programu na Malengo, ambayo mara nyingi yamekuwa hayana mpangilio mzuri wa utekelezaji. Uratibu na taratibu za tathmini, matokeo yake utekelezaji umekuwa dhaifu, hali hii imesababisha kupungua kwa imani na matumaini ya wananchi kwa viongozi wao; ni dhahiri kwamba, wananchi hivi sasa hawana hamasa ya kushiriki katika Mipango ya Kitaifa bali wamekata tamaa. Hiki ni Kitabu ambacho kimefanyiwa *research* na wataalamu wetu. Tunaleta mzaha leo wa kutekeleza Mpango wa Maendeleo ambao tuliukubali.

Mimi naomba Bunge hili limsaidie Mheshimiwa Rais; Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alikuwa na nia ya dhati kabisa kutuletea Mpango huu, lakini leo pesa za kwenda Benki tulikubaliana kwamba Benki ya Kilimo, leo tunazungumzia bilioni mia moja lakini Benki hiyo tulizungumzia kuanzia mwaka jana na mwaka huu kwenye bajeti hii tunazungumza shilingi bilioni 40 za kupeleka kwenye Benki hiyo. *TIB* tulizungumza shilingi bilioni 30 badala ya shilingi billioni 70.

SPIKA: Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Ntabaliba na Mheshimiwa Vita Kawawa ajiandae pia.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ili niweze kuchangia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nitoe *a fatherly advice* kwa wenzetu upande wa pili. Nasema *a fatherly advice* kwa sababu kubwa ambayo Watanzania wametupa kuingia katika jengo hili. Lugha ya matusi haina tija kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachokuumba kwa mamlaka uliyopewa, ufundwaji ambao umelifunda Bunge hili haujaka sawa, naomba urudie ili Bunge hili lifundwe upya. Wale ambao walipata dozi nusu basi ikamilike kwa sababu kuna

Parliamentary Language ambayo katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola inatumika; ni hoja kwa hoja siyo matusi.

Mheshimiwa Spika, hii inatupeleka mbali hata kuvunja utamaduni wetu watu weusi na hususan Watanzania. Watanzania tunaheshimika dunia nzima na ndiyo sababu hata Mataifa mengine ambayo wanafanya ufedhuli, wanatumia jina la Tanzania hata *ku-forge Passport* ya Tanzania kwa heshima ambayo tunayo Kimataifa. Kwa hiyo, suala hili la matusi naomba Kanuni ziandaliwe upya ili yule anayekwenda pembedi na majadiliano na heshima ya Tanzania achukuliwe hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la ushauri kwa upande wa Mipango ni kwamba, kwa uzoefu wangu, naona jinsi tunavyoandaa Mipango tunakwenda kinyume na utaratibu wa kuandaa Mipango. Kama Bajeti hii tunayoizungumza tumejadili Mpango wakati tayari Wizara, Mikoa na Halmashauri, wameshakamilisha Mipango; sasa je, wametumia mwongozo upi wakati hata Halmahauri nyingine wametengeneza ile Mipango bila hata *ceiling*? Siyo utaratibu wa namna ya kutengeneza Mpango.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kingine cha msingi ni kwamba, hii ndiyo inachochea kikundi kidogo cha ile timu ya Halmashauri au Wizara, wanatengeneza Bajeti ambayo wanajipangia bajeti zao. Baadaye katika utekelezaji, CAG anakuja juu anasema mmetumia vibaya hiki kimekwenda vipi, kwa sababu hawakupata baraka za Mikoa wala Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri ambalo amelifanya juzi, kwa heshima ya Watanzania. Ninachowaomba Watanzania, tufanye kazi la sivyo itakuwa kila leo ni mchezo wa kuigiza; Mawaziri hawa wanaingia na kutoka lakini utendaji sisi Watanzania wengine ndiyo tunaosababisha udhaifu wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuwasilisha Bajeti, Mheshimiwa Waziri alianza na neno nidhamu; nidhamu hii ni lazima izingatiwe katika matumizi na kufanya kazi, mbona nchi nyine tunatembea duniani tunakuta watu wanavyofanya kazi, unaona kweli huyu mtu yuko *serious* anafanya kazi. Sisi ni ujanjaujanja, sehemu nyine mtu anaingia kazini saa tatu, lakini kwenye kitabu cha kusaini kuingia kazini anaandika saa moja na nusu. Hili lazima lifanyiwe kazi kwa sababu anakaa ofisini na kazi ya kusoma magazeti, ofisi zimekuwa ni sehemu ya kufanya mijadala ya kisiasa, nchi haiwezi kwenda kwa utaratibu huo. Ninachoomba, kama mtu anakwenda sehemu aombe ruhusa kwa utaratibu.

Katika Kitabu hiki cha Bajeti limezungumzwa suala la *Management Audit*, lifanyike kikamilifu. Miaka ya 2000 utaratibu wa OPRAS ulianzishwa; je, umezaa tija gani? Mfanyakazi kama sehemu ya sekta binafsi au Mtumishi wa Umma, ufanyaji kazi wake ufuatiliwe ili tija ijulikane anavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi katika vyanzo vya kupandisha mapato katika nchi ni lazima tuwe na *priorities* ambazo zipo makundi mawili. Kundi moja liwe na vipaumbele katika kuinua kipato na kundi lingine lazima liwe na vipaumbele katika kutoa huduma. Katika kupandisha mapato hata suala la utalii halikukaa vizuri katika Bajeti ya mwaka huu, ambapo sisi tuna fursa kubwa katika dunia hii, yaani tunaongoza katika fursa za utalii, lakini utalii leo hii unasaidia Tanzania kiuchumi kwa kuongeza pato la asilimia 17; haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ulipotokea mfumko wa kwenda Loliondo kwa Babu, tunaomba Wizara ya Utalii chini ya TANAPA, watupe takwimu. Watu wengi walikwenda na walitozwa fedha na fedha zile zikaongeza pato la nchi. Hii ni sehemu ya kuimarisha utalii wa ndani. Utalii wa ndani

hatujaufanya kazi vizuri, hiki ni kielelezo dhahiri. Katika nchi nyingine kama Japani, Mjapani anapozaliwa ni Sheria ya Japan kwamba ni lazima kama amezaliwa Kusini atembelee Kaskazini mwa Japan na kama kazaliwa Magharibi ni lazima atembelee sehemu nyingine za Japani. Sisi tulete sheria ya kuhakikisha Watanzania tunafanya utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, katika utalii nashukuru wenzetu Zanzibar, asilimia 47 ya mapato ya Serikali ya Zanzibar inatokana na utalii, kwa sababu wamejipanga vizuri katika kunyanya utalii. Haya ndiyo mazingira ambayo inabidi tuyaaangalie, si kodi kwani kodi zimekuwa ni kodi kila siku, lakini kodi hizi zitazamwe upya. Hivi unavyomtoza bodaboda kodi; ye ye mwenyewe amekimbilia ni sehemu ya kujificha na wote tunaona mfumko wa bodaboda kila sehemu; hivi bodaboda ndiyo nchi tunaleta kwamba ni sehemu ya kuajiri vijana? Hapana ni lazima tuwe na mazingira mazuri ya kuboresha mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hiyo ya utalii kwa nini Wilaya ya Serengeti tunanyanyaswa kiasi hicho? Nasema hivyo kwa sababu asilimia 70 ya *National Park* ya Serengeti ipo Wilaya ya Serengeti. Takwimu hizi ni lazima zizae tija kwa Wilaya ya Serengeti.

Kuimarisha ulinzi kwa Hifadhi hili si kupeleka bunduki wala kupeleka Maaskari, lakini unalinda utalii na uchumi kwa njia ifuatavyo:-

Kwa mfano, Wilaya ya Serengeti ukiboresha miundombinu mizuri kwa ajili ya umeme utaajiri vijana, nani atakwenda Mbugani kwa sababu kule ni *risk*. Ukiweka kilimo kitazaa tija nani atakwenda Mbugani?

Mheshimiwa Spika, Wilaya hizi ambazo tuna maeneo ya Hifadhi ni lazima kuwe na Mkakati Maalum wa Kitaifa utakaosaidia kuinua uchumi.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ni kwamba, makusanyo ni kidogo, nikijaribu kuangalia makusanyo kwa nchi nyingine kama Kenya yaani *KRA*, wanakusanya mara 30 ya Tanzania. Hawa ni wenzetu, tupo nao jirani na hii ndiyo imewawezesha baada ya kubanwa na hao tunaowategemea kuleta fedha katika nchi. Wao wameweza kujinasua katika Bajeti yao ya Maendeleo kwani asilimia 95 ni makusanyo ya ndani. Inakuwaje sisi; kwa mfano afya ni hatari, afya za Watanzania tumeziweka rehani kwa wafadhili kwani asilimia 97 tunategemea fedha za wafadhili. Hii ni hatari, naomba tujipange tuandae mikakati mizuri ambayo itatusaidia kuinua mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, katika *power generation* lazima kuwe na *generation mix* kama *high breed* ya kuchanganya upepo na jua. Ujerumani wamekuwa *super powers* wa *solar energy in the World*. Hii ni fursa ambayo tunaipoteza bure, kwani jua tunalo la kutosha, upepo upo mwangi; hivi tatizo liko wapi kwa wataalamu wetu? Wataalamu wetu nao wanageuka kuwa wanasiasa, ndiyo matatizo. Tengenezeni mawazo mazuri yaje ili sisi tubariki. Tunachotaka ni kusonga mbele, lakini haya masuala ya malumbano na kadhalika hayatatusaidia.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi fursa ambazo zipo katika maeneo ...

(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, mengine nitachangia kwa maandishi, nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana, nashukuru pia. Sasa tuendelee na Mheshimiwa Albert Obama na Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Bajeti yetu.

Kwanza, tumshukuru Mungu kwamba, wote tuna afya njema. Pili, niwapongeze Wananchi wote wa Jimbo la Manyovu kwa kuniamini na nitaendelea kuwatumikia. Niwapongeze Wananchi wote wa Wilaya ya Kasulu kwa uvumilivu wao na hatimaye kutulea sisi wa Jimbo la Manyovu na hatimaye kutupatia Wilaya yetu mpya ya Buhigwe. Kwa hiyo, pongezi ziende kwao. (*Makofi*)

Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kukubali kutupa Wilaya yetu na kutupa Mkuu wetu wa Wilaya. Mwisho, nawapongeza Mawaziri wote waliochaguliwa kwenye nafasi zao. (*Makofi*)

Tunayo kazi moja tu ya kuchambua Bajeti zilizowasilishwa. Nimejaribu kupitia Bajeti ya Kambi ya Upinzani ili kuona kama ina vigezo ambavyo vinaweza vikashawishi jamii kwamba ni bajeti ambayo imekidhi lakini nimeona ina udhaifu ufuatao:-

Moja, kima cha chini cha mshahara kilichotajwa ni kiwango ambacho kimekopwa ambacho kililetwa na watu wa *TUCTA* na wao wanachukua ile *figure* wanaweka bila kufanya utafiti na hii kwenye Bajeti halwezi kuonesha kwamba ni kiasi gani kitatumika. Wameendelea kusisitiza kwamba, wanataka kuweka *pension* ya wazee ambayo kwenye Bajeti yao haioneshi sasa ni kasi gani kitatumika, kwa hiyo, inaendelea kuonesha kwamba bado ni Bajeti dhaifu.

Inaendelea kusema kwamba, Bajeti ya Serikali haikutenga mapato ya ndani huku Serikali imepanga *2.2 trillion* kwa ajili ya maeneo hayo. Kwa hiyo, inaendelea kuonesha kwamba bado ni dhaifu.

Wakati wa kujinadi vyama hivi vimekuwa vikisema kwamba, vitatoa elimu bure kwenye maeneo ya Kigoma, watatoa sementi nusu bei, lakini sasa kwenye Bajeti yao hawaoneshi hizo fedha zitakazotumika zipo namna gani. Kwa hiyo, hii ni kwamba, unakuwa unawahadaa Watanzania bila kuwa na uwezo navyo.

Vilevile wamekwenda mbali zaidi kwenye vijiji vyetu hasa vya Mkoa wetu wa Kigoma, kwa kuwashawishi Madiwani wawaambie wananchi wao wasijitolee. Hii imerudisha *morale* ya Watanzania, lakini kwenye bajeti yao sioni mahali ambapo wameonesha kwamba wangeweza kuzipeleka fedha. Kwa hiyo, wasiwadanganye Watanzania.

Wamezidi kuonesha kwamba, kodi ya mtu wa kima cha chini, Serikali inasema mtu wa kima cha chini aanzie shilingi 170,000 bila kukatwa kodi, lakini wao wanazidi kumgandamiza Mtanzania kwamba eti iwe shilingi 150,000. Kilichonisikitisha ni kwamba, Bajeti ya Serikali ambayo ni shilingi trilioni 15 kwa ujumla wao na wao wameendelea kuikopi hiyo hiyo huku Serikali yao itakuwa ndogo. Kwa hiyo, Bajeti ya Upinzani inaonekana kwamba haikukidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, iendelee kuiona Barabara ya Kasulu - Manyovu kama ni kitu muhimu na ni ombi lao. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Ujenzi iendelee kuona kama Obama anaendelea kuipigania barabara ile.

Lipo Zao la Michikichi kwenye *speech* zote, ninaomba Waziri wa Kilimo atakapokuja ku-*wind up* atuambie kwani sioni likipewa umuhimu na msukumo na huku mafuta ya mawese watu wanayatumia sana lakini sioni zao hili likitajwa kama nalo litasamehewa kodi.

Wakulima wetu wa Manyovu wanaomba ruzuku ya kahawa, kwa hiyo, ningeomba nayo ifikiriwe. Vilevile mashine

ndogo za kukoboa kahawa katika vijiji vyetu ni muhimu sana zikawekwa kwenye Mpango wa Bajeti yetu. Bajeti ya Serikali imeendelea kunifurahisha kweli kweli; kwanza, kwa kutenga shilingi bilioni 70 kwa ajili ya Mikoa na Wilaya mpya, ni kitu ambacho Serikali ipo makini imekifanya. Imenifurahisha zaidi kuweka fedha za JKT, sasa kwa mtu yeyote ambaye anasema kwamba hiyo ni Serikali gani na huku inataka kuimarisha vijana wetu, sielewi wanakuwa na maana gani!

Msukumo wa reli umewekwa vizuri lakini tulipokuwa kwenye Kamati, Wizara ya Elimu na Mafunzo ilitutangazia ikasema ifikapo tarehe 30 Juni, 2012 madai ya Waalimu madai yatakuwa yamelipwa. Kwa hiyo, tunaomba Walimu waendelee kulipwa haki zao kwa sababu ni kilio kinachowasumbua.

Mapendekezo ya Serikali ya kupandisha ushuru wa mawasiliano kwenye simu zetu siyo kitu kinachokubalika. Mawasiliano ni Sekta ambayo imeendelea kukuza uchumi na kuongea kwetu tunaendelea kupata adhabu. Ninapenda kupendekeza yafuatayo:-

Tunayo maeneo mengi ambayo minara ya simu haijafika, ningeomba Wizara inayoshughulika na mawasiliano, waweke minara mingi ili mapato yaweze kuwa mengi zaidi.

Kodi kwa bodaboda ambayo imepunguzwa ni faraja kwao na ninaomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninapenda nishauri kwamba ili kupunguza matumizi ya Serikali, tunayo mafunzo ambayo watu wanajifunza wakiwa wameshaajiriwa, aidha wengine wanakwenda kuchukua *Masters* au wengine wanakwenda kuchukua *PhD*. Kuliko Serikali kuendelea kuwagharamia kwa nini hii Bodi ya Mikopo isipanuliwe mpaka isiwe na mwisho? Yeyote anayetaka kwenda kuchukua *PhD* aende akakope fedha halafu atazilipa baadaye kuliko Serikali kuendelea kubeba watu waliokwishaelimika huku hatuwezi?

Mimi ninashauri kwamba, ile Bodi ya Mikopo ipanuliwe na ipewe meno zaidi na fedha. Zile training courses zote zinazofanyika ziweze kuwa *taken care* na Bodi ya Mikopo na mtu yeyote anayetaka kwenda kusoma *Masters* au *PhD* aweze kuhudumiwa na Bodi.

Bunge liliopita tuliongelea kwa masikitiko makubwa sana kuhusu mishahara ya Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Madiwani. Sioni kwenye Bajeti hii wameweka wapi kuonesha kwamba watalipwa mishahara hii. Bunge liliopita tuliongea kwa uchungu na kila Mbunge aliongea kwamba, Diwani na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji waweze kulipwa lakini kwenye Bajeti hii labda Waziri atakuja kutufafanulia.

Mheshimiwa Spika, ni hakika kwamba, mikopo kwenye benki zetu tunazidi kuweka mitaji. Nakubaliana, lakini mazingira ya watu wetu wa vijijini kuwafanya waweze ku-access hii mikopo siyaoni, kwa sababu kupima viwanja ili watu wawe na hati hakufanyiki na kupima mashamba hakufanyiki. Sasa watu watapataje mikopo wakati hawana dhamana? Kwa hiyo, nimeona nishauri hayo yote yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, wale wote ambao hawaungi mkono hoja na ambao hawataki fedha, Obama ninazihitaji kwenye Jimbo langu. Mimi naunga mkono mia kwa mia fedha zije Jimbo la Manyovu. (*Makof!*)

SPIKA: Yaani zije zote kabisa kabisa. (*Kicheko*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata fursa hii ya kuchagia Bajeti ya 2012/2013.

Kwanza, naomba niwapongeze Waziri na Naibu Mawaziri wote wawili na Waziri wa Uhusiano na Uratibu, Mheshimiwa

Wasira na Dkt. Mgimwa, kwa kuwasilisha vizuri Hotuba zao Bungeni. Pia naomba niwashukuru sana Serikali, maana usiposhukuru kibaba, Waswahili wanasema hata ukipewa pishi huwezi kushukuru. Katika Jimbo letu la Namtumbo, kwa mwono wangu Serikali imenipa gunia zima la mpunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani hizi kwa Serikali kwanza kwa kutujengea barabara ya kutoka Songea - Namtumbo kwa kiwango cha lami. Natoa shukrani kwa Serikali pia Mradi unaendelea kutoka Namtumbo - Tunduru kwa kiwango cha lami. Natoa shukrani kwa Serikali kwa kutuletea Mradi wa Umeme ambao nguzo na nyaya zake zimeshawekwa tayari, tunasubiri umeme uwashwe. Naishukuru Serikali kwa kutuletea fedha za kukarabati barabara zetu, sasa hivi Namtumbo nzima zinafikika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba nijielekeze kwenye Bajeti. Kwenye Bajeti kuna baadhi ya wenzetu wamezungumzia kuhusiana na Deni la Taifa, lakini wakati wanazungumzia hawakuzungumzia Pato la Taifa. Huwezi kuzungumzia deni bila kuzungumzia pato.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa la Tanzania ni shilingi trilioni 37.5 na aya ya 47 ya Hotuba ya Waziri wa Fedha inatuambia wastani wa pato la Mtanzania ni shilingi 869,436.30, lakini Deni la Taifa kwa Mtanzania ni shilingi 455,640.40 kwa kila Mtanzania, ndiyo deni lake. Sasa ukitazama kwa haraka haraka pato la laki nane na deni la laki nne linahimiliwa, lakini halijaelezwa vizuri. Ukienda vizuri ndani zaidi, ukifanya hesabu zake sisi tunalipa Deni la Taifa asilimia tano ya mapato ya ndani. Mapato ya ndani ni karibu trilioni 5.6. Mapato haya ya ndani ukiyagawanya kwa Watanzania 44,500,000 ni sawa sawa kwa siku moja Mtanzania anatakiwa alipe shilingi 17.50, maana yake inatakiwa lazima Watanzania waelewe hivyo. Kwa mwaka Mtanzania analipa shilingi 6,387.

Sasa mtu anapozungumzia Deni la Taifa kuna uzito sana, lazima ufanye hesabu ili Mtanzania aelewe. Kwa siku Mtanzania anatafutiwa kulipiwa shilingi 17.50. Kwanza, tuangalie hapo kuhusiana na Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na malalamiko kwa nini tunakopa sana deni letu ni kubwa. Deni letu tumesema tunalipa asilimia tano ya mapato ya ndani na kigezo cha Kimataifa ni asilimia 35. Ukifikia hapo wewe uko hatarini. Sisi ni asilimia tano ya mapato yetu ya ndani. Kwa hiyo, tuko sawasawa na tunakopesheka. (*Makofi*)

Kuna malalamiko kwamba, tusikope mikopo ya kibiashara. Nimefanya utafiti mdogo, mikopo ya kibiashara tuliyokopa hapa ni kwa ajili ya kulipia barabara na tunalalamika hapa tuongeze *infrastructure*. Tumelipia umeme wa MW 60 kule Nyakato Mwanza. Tumekopa pia mkopo wa miaka 40 kulipia ujenzi wa Daraja la Malagarasi. Mikopo hii ni ya muda mrefu, kwa hiyo, lazima tusipotoshe wananchi hapa kwamba tuna mzigo mkubwa sana; hapana, hauwezi kuendesha Serikali bila kukopa. Marekani wana mkopo wao. Sisi deni letu ni asilimia 54, Marekani mkopo wao ni asilimia 108 ya Pato la Taifa. Japani ambao ni matajiri, sisi ukitutoa wote nje pale tuna magari ya Japani, lakini wana deni la asilimia 205 ya pato lake la Taifa, sisi ni asilimia 54 tu. Kwa hiyo, lazima tuangalie tusiwapotoshe wananchi kwamba tuna mzigo mkubwa; hatuna mzigo huo mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bidhaa za asilia katika mwaka 2011 ziliongeza mauzo yake kwa asilimia 16.8 kutoka dola milioni 572 hadi kufikia dola milioni 668. Ongezeko hili la mauzo mazuri ya nje limetokana pia na kuongeza thamani ya tumbaku na kahawa. Sasa hapa nataka kuzungumzia tumbaku na naomba *ku-declare interest*, mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeuza tumbaku nje yenye thamani ya dola milioni 281.2 mwaka 2011. Mwaka 2007 tuliiza dola milioni 89.9, sasa kumekuwa na ongezeko la mwaka hadi mwaka la uzalishaji na mauzo ya tumbaku nje. Pia tumbaku imekuwa ikilipa kodi ya pato la ndani la Taifa. Kutoka mwaka 2007 ilikuwa inalipa shilingi bilioni 89, mwaka 2008 shilingi bilioni 106, mwaka 2009 shilingi bilioni 118, mwaka 2010 shilingi bilioni 134 na mwaka jana shilingi bilioni 156.7. Sasa hiki ni chanzo kizuri sana cha mapato ya nchi yetu. Tunaomba mkiangalie na mkienzi. Watu wanaogopa sana kuzungumzia hili eti kwa sababu sigara inaathiri watu, lakini hiki ni chanzo cha mapato, tukiangalie tusikiache. Tunapokuja tunaosimamia tumbaku tunapoomba mtuongezee rasilimali watu na vitendea kazi ili tuwasaidie wakulima waweze kuzalisha vizuri wasikate tamaa, tuwasaidie matatizo yao, tunaomba Serikali mtusikilize na mtusaidie. Hili Ni eneo ambalo linasaidia sana katika Pato la Taifa (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la kilimo, pia naishaukuru sana Serikali kwa kubadilisha mfumo wa wakala wa pembejeo. Sasa hivi tumesikia kwamba, wakulima watapelekewa moja kwa moja pembejeo zile. Nawapongeza sana, kwa sababu mfumo huu ulikuwa unawatajirisha wachache. Kwanza, walikuwa wanachelewesha kuleta pembejeo, hawaleti kwa wakati halafu mwisho wanaleta pembejeo za kukuzia, wakulima wanakuwa wamekosa pembejeo za kupandia na mbegu bora. Sasa nashukuru sana kwa kubadilisha muundo huo. Ninachoiomba Serikali, tuwahi mapema kupeleka mbegu na pembejeo zake ili wakulima waweze kuzipata mapema na waongeze mapato yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakulima wa nchi hii hasa wa Mkoa wa Ruvuma, wengi wao wamekuwa wakitumia kilimo cha mkono. Mkoa wa Ruvuma tunapongeza sana Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Said Mwambungu, kwa kuja na mawazo ya kubadilisha kilimo kutoka kuwa cha mkono kwenda cha

matrekta. Mpaka sasa hivi ameishaingiza matrekta 50 katika Mkoa wetu wa Ruvuma. Tunaomba na ninyi Serikali mtusaidie, eneo lile ndilo linalozalisha chakula kwa maeneo mengine ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba sana mtuunge mkono katika uzalishaji wa mahindi, lakini pia masoko yake. Tunaomba masoko ya mahindi yawahi mapema. Mwaka jana walichelewa mpaka mvua ikaanza kunyesha na mahindi mengine yalinyeshewa yakaoza. Kwa hiyo, tusiwakatishe tamaa wakulima. Tunaomba sana Serikali mnapogawa fedha za ununuzi wa mahindi, basi tunaomba sana wawahi kule kununua mahindi ili wakulima wetu waweze kunufaika na kile wanachokiingiza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi ya kuchangia Bajeti hii. Mimi pia naomba niungane na wenzangu wanaouna mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nitangulize kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa jitihada kubwa ambayo ametufanya kutufungua katika suala zima la miundombinu ya barabara. Barabara yetu ya Tunduma inaenda vizuri na ina lengo la kufungua Ukanda mzima ule. Ninaomba kasi lendelee katika barabara inayotoka Sumbawanga - Mpanda Kibaoni. Barabara hizi ni matarajio makubwa sana kwa Wanarukwa kuwa zitaleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, hizi barabara pia zitaweza kutuunganisha na masoko mbalimbali ya nje. Ukiangalia barabara inayotoka Sumbawanga kwenda Namanye, bado kidogo tu itafika Kirando ambako ni mpakani na Zaire (Kongo DRC). Tutakuwa tumeunganishwa vizuri na nchi jirani. Tunaomba *speed longezeke*.

Mheshimiwa Spika, barabara inayotoka Sumbawanga - Kibaoni utekelezaji wake unasua sua. Barabara hizi hazitakuwa na maana sana kama barabara zinazoenda pembezoni kwenye maeneo ya uzalishaji hazitakuwa zinaboreshw. Maeneo ya uzalishaji pia yanatakiwa yatazamwe, tumeziachia mzigo mkubwa sana Halmashauri za Wilaya. Mwaka jana nilikuwa napiga hesabu kwa kilomita zinazohudumiwa na Wilaya ya Nkasi, nikakuta inatengewa chini ya shilingi 700 kwa kilomita. Sasa kama hizo ndizo fedha zinazotengwa kwa Halmashauri utegeme mabadiliko gani?

Tumekuwa mara kadhaa tunaiomba Serikali barabara hizo zisaidiwe kwani ndiyo zinazowasaidia wakulima wetu na wapiga kura wetu ambao wako kule hasa tutakapoingia Ofisi ya Waziri Mkuu hizo barabara zitazamwe. Zipo Barabara za Wampembe - Kitosi, Wampembe - Nkanakala, Nkasi - Uchoka mpaka pale Myula ni barabara ambazo zinapita katika maeneo makubwa ya uzalishaji ambayo kama zingeunganishwa na hizi zinazotengezwa kwa kiwango cha lami, maana yake chakula kinachozaishwa kingeweza kuongezwa thamani mara mbili kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, ni ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningedhani kwamba, tufike wakati tubadili mtindo wa utekelezaji wa barabara za vijiji kwa kuanzisha *agency* itakayoshughulikia barabara za vijiji. *Agency* hiyo inaweza ikatusaidia sana. Tumeona kwenye Wakala wa Umeme (*REA*), wanafanya vizuri. Tumeona kwenye Mamlaka ya Majitaka na Majisafi wanafanya vizuri, lakini kwenye barabara tu ndiyo tunaona vijiji kule hakuna kasi nzuri ya ufanyaji kazi. Kwa hiyo, ingeanzishwa *agency* inayojitegemea, wahandisi wale wangejisikia pia kama wasomi walioandaliwa kufanya kazi. Sasa hivi wako *idle*, mwisho wanatembelewa na shetani, unakuta mtu anaanza kujihusisha na mambo ya kuchakachua kwa sababu hana kazi za kutosha, hatujampa kazi za kutosha. Kwa hiyo, hilo nafikiri

Serikali tuliangalie, vinginevyo, tutapiga kelele siku hadi suku lakini barabara za vijijini zitabaki hazina msaada wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu kilimo kimetengewa shilingi bilioni 192.2. Maoni yangu fedha hii iongezwe. Kilimo kinaajiri asilimia 80 ya Watanzania. Ukuaji wa kilimo kutokana na takwimu za mwaka jana inaonesha kwamba, tumeanguka. Mwaka jana ukuaji wa kilimo ulikuwa asilimia 4.2, sasa ni asilimia 3.6, maana yake ni kwamba, kilimo hakisongi mbele huku kimebeba mzigo mkubwa zaidi. Kama tunataka kujinasua na kuleta maendeleo ya haraka ni kuwekeza zaidi katika kilimo. Nazikubali jitahada za Serikali, lakini bado hazitoshelezi. Tunatakiwa bei za pembejeo zipungue na zifike mapema. Kila siku tunasema ni vizuri zifike wakati wa mavuno. Mwezi wa Saba ndiyo wakati mwafaka wa kufikisha pembejeo kwa wakulima na utawanyaji pia uwe mzuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ubora wa pembejeo, mwaka huu nina wasiwasi na wataalam wetu. Jambo ambalo halikuwepo kabisa, mbolea mwaka huu haikuleta tija kama ya mwaka jana. Kadhalika mbegu. Haya maeneo yanayofanya tafiti wanatakiwa waangalie jambo hili. Ukimhujumu mkulima maskini huyu kwa kiwango hicho ni dhambi kubwa. Sasa ni wataalam peke yake, pengine suala la kuongeza kufanya biashara na hawa mawakala limeanza kupotosha dhana hallisi ya utafiti wa kuleta mbegu bora kwa wakulima. Ningeshauri hapa tupafanyie kazi zaidi ili mkulima asipate hasara.

Mheshimiwa Spika, tunaomba itolewe mikopo kwa wakulima. Kwenye Bajeti hii tumeona kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni 30 zimetengwa kwa Benki ya Wakulima. Mimi natoka maeneo ya wakulima, sijaona nani amekopeshwa kule. Mkoa wa Rukwa ni maarufu lakini sijaona nani amekopeshwa, labda mtueleze hata mmoja. Mikopo hii angalieni inaweza ikawa inaelekezwa kwa watu ambao siyo wakulima, halafu tukawa tunadanganyana.

Mheshimiwa Spika, matrekta yamejaa bei ni kubwa. Tunaomba bei ipunguzwe lakini pia pawe na mfumo wa kukopesha matrekta kwa watu binafsi, wakulima kwa *SACCOS* na watu wote wanaoshughulika na kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la uvuvi katika Ziwa Tanganyika halijaendelezwa vya kutosha. Ningombas katika Bajeti hii litazamwe kwa namna ya pekee. Ukanda ule hautembelewani Viongozi hasa kwa sababu hakuna hata barabara na kwa maana hiyo watu wanaishi katika umaskini mkubwa huku wakizungukwa na rasilimali kubwa sana ya mali inayotokana na Ziwa lile. Hatujawa na uwezo wa kusimua kwa sababu ya zana duni tunazozitumia. Ningombas katika Bajeti hii, hili litiliwe mkazo mkubwa sana ili tuweze kuwakomboa. Hatuwezi kuondokana na umaskini katika maeneo yetu kama tumewafunga; mawasiliano ya simu hakuna, barabara hakuna, lakini pia bado hatujawawezesha kwa kuwapa zana nzuri za uvuvi na usafiri wa maji katika Ziwa Tanganyika; ni shida kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni umeme. Umeme ni kitu muhimu. Gridi ya Taifa inayotoka Nyakanazi – Kigoma – Sumbawanga na kuunganisha Mbeya – Iringa, ingetusaidia sana katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo katika Ukanda ule kwa sababu ile ingeleta wawekezaji kwa haraka, kwa sababu watu wote wanatafuta nishati hiyo katika kuwekeza. Vilevile Ziwa Tanganyika lingeweza kutumiwa katika uwekezaji wa kusindika minofu ya samaki; ingetusaidia sana. Kwa hiyo, hilo nalo mtusaidie. Pale kwenye Jimbo langu, Kijiji cha Nkomoro II, kuna makaa ya mawe yanaendelezwa na mwekezaji mmoja wa kwetu pale. Tungemsaidia hapo ndiyo tungeweza kutumia *PPP* katika kuhakikisha kwamba, makaa ya mawe yale yanatumika ili yaweze kuchangia katika Gridi ya Taifa ambayo inaweza ikapita hapo kama tulivyokuwa tunasema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. DUSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia Bajeti yetu. Awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana kaka yangu Waziri wa Fedha, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi kifupi hiki tangu amepewa jukumu hilo. Amefanya kazi kubwa ya kusikiliza ushauri makini na wa kina uliotolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi. Mengi ya mambo ambayo tuliyashauri katika Kamati yetu, ameyachukua na ameyafanya kazi; tunakupongeza sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ndiyo inayojenga matumaini kwa Watanzania. Nilisema ubora wa Bajeti hii mwaka jana wakati nachangia kuwa, ubora wa Bajeti ni katika utekelezaji wake. Tulivyotekeleza Bajeti ya mwaka jana wote tunajua, sasa tunayo Bajeti nyingine, Watanzania wana matumaini makubwa kwamba tutaitekeleza vizuri ili iwaondolee kero. Naipongeza Serikali kwa kukaribia kukamilisha Mradi mkubwa wa Barabara ya Tanga - Horohoro. Mradi huu kwa uhakika utafungua fursa za kiuchumi kwa Mkoa wetu lakini vilevile kwa Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa jambo lile, watu wa Tanga wana kilio cha fidia kwa wale ambao walipata athari ya kubomolewa nyumba zao au kwa hiari yao waliobomoa nyumba zao. Mheshimiwa Rais na katika hili tunamshukuru sana, alipokuja akaona kwamba wapo watu walioheshimu taratibu wakabomoa wenyewe, aliahidi kwamba watu wale watalipwa. Watu wa Tanga wamekuwa na subira wakiamini Serikali yao itatekeleza ahadi lile. Tunaomba Serikali itekeleze ahadi yake. Hii ndiyo kero ya Watu wa Tanga, Horohoro, mkitekeleza hili hatuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, kama tuna jambo ambalo tuna changamoto nalo kubwa katika nchi yetu ni maji. Tusipokuwa waangalifu wa jambo hili, litailetea matatizo Serikali yangu ya

Chama cha Mapinduzi. Kuna tatizo kubwa sana la upatikanaji wa maji salama. Mradi ule wa Vijiji Kumi wa Benki ya Dunia, utekelezaji wake umekuwa na matatizo. Tuongeze kasi katika kutekeleza Mradi ule. Nilikuwa napitia *document* ya *Water Sector Development Programme*, ambayo tumejikita kutekeleza Programu hii kuanzia mwaka 2006 mpaka mwaka 2025. Tumesema kutekeleza Programu hizi tunahitaji dola 3,366.38 milioni na katika hizo zinazoelekezwa vijijini ni dola 1,643 milioni. Ninachotaka kusema hapa ni nini? Kiasi cha fedha tunazopanga kwenda kwenye Sekta ya Maji Vijiini ni nje ya *projection* hizi tulizojiwekea. Kwa mwendo huu, hatuwezi kuondoa tatizo la maji.

Mkinga tuna tatizo kubwa la maji. Makao Makuu ya Wilaya sasa hayajengeki kwa sababu hatuna maji. Nilikuwa nawaambia wataalamu wangu wa maji pale Wilayani kwamba, zile *data* za upatikanaji wa maji ni asilimia 53 siyo sahihi; kwa hiyo, naomba tuongeze nguvu katika kuelekea kwenye upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo ambalo tunapaswa kuliangalia kwa makini. Tulipitisha Sheria hapa miaka minne iliyopita kama sikosei kwamba, Mamlaka zetu za Maji zitozwe kodi ya VAT kwa madawa yanayotumika kutibu maji. Sasa kama madawa ya binadamu hatutozi VAT vipi madawa tunayoyaelekeza kwenda kutibu maji ambayo yanatumika kwa binadamu tutoze VAT? Hapa nina takwimu za mamlaka sita katika nchi yetu. Mamlaka ya Maji Tanga gharama zake kwa mwaka ni shilingi milioni 400, wao wamekuwa wakipata msamaha, lakini nitaeleza baadaye shaka yangu au hofu yangu ni nini. Mbeya gharama zake ni shilingi milioni 600, nao wamekuwa wakipata msamaha. Iringa gharama zao ni shilingi milioni 200, wao wanatozwa kwa mwaka VAT wanalipa shilingi milioni 35. Mwanza gharama shilingi milioni 400 wanalipa shilingi milioni 72. Morogoro gharama shilingi bilioni moja wanalipa shilingi milioni 180. Tabora gharama shilingi milioni 315 wanalipa shilingi milioni 56. Baadhi ya mikoa ambayo

imesamehewa kama Morogoro sasa hivi wamefuatwa tena wanaambiwa walipe; wametakiwa kulipa shilingi milioni 180, lakini wanatakiwa kulipa na fedha ambazo walikuwa wamesamehewa shilingi milioni 223. Wasiwasi wetu Watu wa Tanga unakuja hapo kwamba, pamoja na kwamba tunapewa msamaha, inawezekana kesho asubuhi mtu mmoja akakurupuka huko ofisini akasema tulipe na zile fedha ambazo tulikuwa tumewasamehe.

Mheshimiwa Spika, nasema hii siyo sahihi. Lazima tuangalie upya uamuzi wetu, tusilipe VAT kwenye maji.

SPIKA: Ahsante umemaliza vizuri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Meshack Opulukwa na Mheshimiwa Kidawa Saleh ajiandae, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani pia ajiandae na Mheshimiwa Cecilia Pareoso naye ajiandae.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia Bajeti yetu. Kwa kuwa mambo mengi yameongelewa na wazungumzaji waliotangulia, nitajitahidi sana kujaribu kugusia maeneo ambayo aidha wameyasahau au waliyaacha kwa ajili ya kuchangia kwa wakati mwengine.

Mheshimiwa Spika, wakati naanza kukua nikiwa mdogo, nillanza darasa la kwanza nikamaliza darasa la saba, nikaenda Kidato cha Kwanza nikamaliza na nilipokuwa nikiendelea kusoma shule na hata nilipokuwa nikijaribu kuongea na watu wengine mtaani, wote walikuwa na kauli moja kama ambayo imekuwa ni kauli ya Chama cha Mapinduzi kwa muda mrefu na ni kauli ya Taifa kwamba Kilimo ni Utu wa mgongo wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii ambayo imewasilishwa kwetu, nilikuwa najaribu kuisoma kwa makini *between the lines*, nikadhani kwamba nilikuwa nakosea, nikajaribu kuuliza wale wenzangu niliokuwa nao karibu kama *figures* ambazo nilikuwa

nazisoma nazo zilikuwa haziko sahihi. Nikaja baadaye nikagundua kwamba, kumbe kilimo siyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Baada ya kusoma tena zaidi nikagundua kwamba, uti wa mgongo wa Taifa hili ni miundombinu na wala siyo kilimo. Niajuliza mara nyingi nataka niweze kusaidiwa Taifa hili tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kama miundombinu ilitengewa zaidi ya shilingi trillioni tatu, ukijumlisha umeme, maji, usafirishaji na mambo mengine halafu kilimo kikawa na 192.2 bilioni, halafu tunasema kilimo ni uti wa mgongo; mimi ilikuwa hainiingii akilini vizuri. Nilikuwa naishauri Serikali angalau sasa iangalie vizuri maneno yake. Watanzania zaidi ya asilimia 75 mpaka 80 walioko vijiji ni wakulima. Sisi tunaotoka kwenye Majimbo yanayolima pamba, ukichukua kwa mfano Mkoa Mpya wa Mkoa wa Simiyu na ukichukulia Wilaya ya Meatu ndiyo inayolima pamba nyingi kuliko Wilaya nyingine yoyote ile katika Mkoa Mpya wa Simiyu; kama bei ya pamba ambayo inakusudiwa na Bodi ya Pamba na Serikali ya shilingi 520 kwa kilo moja wakati mwaka jana bei ya pamba ilikuwa ni shilingi 800 na ikapanda mpaka shilingi 1,200 na 1,300 katika maeneo ya Jimbo langu; Wananchi watakata tamaa na mwisho wake wataamua kuacha kabisa kilimo cha pamba ili waweze kwenda kwenye kilimo cha mazao mengine yenye faida na tija.

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana Serikali inaanza kuwasahau wakulima wa pamba. Inawasahau sana sana, inajikita zaidi kwa wafanyabiashara. Wakati wa mdororo wa uchumi mwaka 2008/2009, Serikali iliji-*commit* na ikatoa *around 1.7 trillions Tanzania Shillings* kwa ajili ya kusaidia mdororo wa kiuchumi. Leo hii wakulima walio wengi, zaidi ya 14,000,000 ya Watanzania hawana mategemeo mengine isipokuwa pamba kama zao la biashara. Ninamwomba sana Waziri mwenye dhamana, kama wakulima hawa hawatawatendea haki kwa bei, ningependa kuongea kwa niaba ya Wananchi wangu, hawa wanunuzi amba wanajiandaa kununua kwa bei ya

shilingi 500 kwa kilo moja ni bora wasubiri mpaka hapo bei itakapopanda iwe zaidi ya shilingi 1,000 kwa kilo na si chini ya hapo.

Wananchi wa Meatu kupitia Bunge hili, ningewashauri wasiwe na haraka ya kuuza pamba yao kwa sababu najua bei itapanda. Kwa uzoefu uliopo, kwa miaka mitatu mfululizo bei ya pamba ilikuwa ikitajwa ya chini sana lakini baada ya msimu kuanza bei imekuwa ikipanda. Hii ndiyo rai yangu kwa wakulima wa zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Mikoa Mipyä ikiwa ni pamoja na Mkoa wangu wa Simiyu. Ni Sera ya Taifa kwamba, mikoa yote angalau iunganishwe kwa barabara ya lami. Nashukuru kwamba, daraja linalounganisha Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Singida ambalo ni Daraja la Sibiti, lipo kwenye utaratibu wa kuanza kujengwa na fedha naamini imekwishatengwa. Sasa basi naomba tunapokuwa tunaendelea na mchakato huu wa Bajeti kama itashindikana hata kwa mwaka unaokuja, Mkoa wa Simiyu uunganishwe kutoka Bariadi mpaka Singida kwa barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mabingwa wa kukopa, lakini kukopa siyo kitu kibaya, mimi mwenyewe nimekopa nalipa madeni. Sasa tunaomba Serikali yetu inapokopa vilevile ilipe madeni inayoyakopa. Ninashindwa kuelewa tunakopa kwa ajili ya kufanya nini. Wakati wa uhai wa Baba wa Taifa, tulikopa tukajenga viwanda vyा nguo, kwa mfano, *MWATEX*, tukajenga viwanda vyा nyama, kwa mfano, *Tanganyika Packers*, leo hii nashindwa kuelewa tunakopa kwa ajili ya kufanya nini! Naishauri Serikali, mikopo ambayo tunaikopa kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania walio wengi ambao wanaitegemea Serikali yao hii, iwasaidie basi iende kwenye maeneo ambayo yana tija kwao na wala siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongelea pia suala la madeni ya ndani. Katika Bajeti hii, Serikali imesema kwamba

wataendelea kuajiri, ajira mpya zitatoka na tunaamini kuwa tutaendelea kupata walimu wapya. Kwa bahati mbaya sana, kuna walimu walioanza kazi mwaka huu, mwezi wa pili, mpaka leo tunapoongea hawajawahi kulipwa hata shilingi moja ya mshahara wao. Leo tunasema tunataka kuwaajiri walimu wengine wakati tuna madeni ya nyuma tangu mwezi wa pili! Nilikuwa naomba hebu tulipe madeni ya watumishi wetu ambao tumewaaajiri ili waweze kuwa na *morale* ya kufanya kazi na kuweza kulitumika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninatoa ushauri kwa Bunge hili kwamba, sisi kama Wabunge tumekuwa na matatizo ya kutokujua labda majukumu yetu, tunatakiwa kufanya nini katika Bunge hili Tukufu. Naamini kazi ya Mbunge pamoja na mambo mengine ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Kinachoonekana katika Bunge hili, Wabunge ndiyo watakuwa Wasemaji Wakuu wa Serikali na wala siyo Washauri wa Serikali. Anasimama Mheshimiwa Mbunge anasema.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge naona muda umeisha.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja iliyokuwa Mezani. Naanza kwa kumpongeza au kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Mgimwa na Mheshimiwa Wasira na Naibu Mawaziri, kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuweza kutuletea bajeti ambayo sasa tunaijadili.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutoa mchango wangu wa jumla tu katika Bajeti hii na nianze kwa kuelezea sura ya Bajeti. Ukiangalia sura ya Bajeti, mapato yetu ya ndani yale ya kodi na yasiyo ya kodi na ya Halmashauri yanashindwa *ku-finance* matumizi ya kawaida. Kwa kuangalia haraka haraka tu sura hii siyo nzuri kwa Taifa. Hii inaonesha hata katika

familia, mfano baba ameshindwa kulisha vyema familia yake, inabidi aende kwa wenzie wa karibu wamsaidie kulisha familia.

Ukienda katika uchambuzi wa ndani kama walivyozungumza wenzangu, kuna matumizi ambayo hayaepukiki na katika *recurrent expenditure* vilevile kuna *element* za matumizi ya maendeleo. Vilevile ukienda kwenye kwenye matumizi ya maendeleo ni lazima utakutana na matumizi ambayo yana *recurrent nature*. Hilo kwenye Bajeti haliwezi kuepukika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kuna matumizi ambayo ni lazima yafanyike na yakifanyika yanaondoka, kwa mfano yale ya sensa. Kuna matumizi mengine ni lazima yafanyike ili kusaidia matumizi ya maendeleo au maendeleo ya nchi. Kwa mfano, tuna Miradi mbalimbali mipya ambayo Watanzania hatuna utaalam nao ni lazima ipatiwe fedha ifanyike ili kusaidia maendeleo. Mfano, mafunzo, kuendeleza rasilimali watu, tuna Miradi ya Gesi, tuna Miradi ya *Uranium* inakuja, watu wote hawana utaalam. Lazima zipatikane fedha za kufundisha hawa watu waweze kusaidia kuleta maendeleo katika Miradi hiyo. Vilevile kuna mambo ya utafiti lazima yafanyike. Hakuna nchi inayoendelea bila utafiti, kwa hiyo, mambo ya utafiti yameingizwa hapa. Sisi tunakubaliana na sura hii lakini tumeishauri Serikali katika Kamati kuwa iwe sura ya mpito, isiwe kila mwaka tunakuja na sura hii hii. Mara hii sura hii iko *justifiable* kutokana na haya yaliyojitokeza, lakini kipindi kinachokuja kwa mwaka ujao sura hii ibadilike.

Vilevile ukiangalia vipaumbele; kwa kweli vipaumbele vilivyowekwa ni vya uhakika vya kuchochoea maendeleo ya nchi yetu. Watu wanaofikiwa na huduma ya umeme ni chini ya asilimia 20 katika nchi hii.

Tunazungumzia umeme vijijini; tunasema watu wanalalamika kuwa uchumi unakua lakini Watanzania walio

wengi wanalamikia umaskini kwa kuwa maendeleo hayajawafikia kule waliko na wengi wapo katika Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, tunasema suala la umeme vijiji ni lipewe kipaumbele, vinginevyo itakuwa malalamiko ya kila siku.

Suala la barabara vijiji ni kwa maana ya *feeder roads* vilevile liangaliwe, kwa sababu wakulima wetu wanahamasishwa wanalima kwelikweli. Utakuta mazao yao yanaozea mashambani hakuna uwezekano wa kuyaondoa kuyapeleka sokoni. Hili jambo ni la muhimu kabisa. Huduma za jamii ni kitu cha msingi, lazima Watanzania wapatiwe. Kwa hiyo, sisi tunakubaliana na vipaumbele hivi, vimeteuliwa kwa umakini kabisa na ndivyo vitakavyochochea ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo tunaloliona hapa ni moja kuwa, malalamiko haya yasingetokea kama tungekuwa na uwezo mkubwa wa kukusanya mapato. Kwa hiyo, la msingi hapa ni *TRA* kujitahidi kukusanya mapato kwa kadiri ya uwezo wa vianzio vyta mapato. Tunawashukuru na tunawapongeza wamekusanya zaidi ya lengo, zaidi ya asilimia 104, lakini je, huo ndiyo uwezo wa vyanzo vyetu vyta mapato tu au wanaweza wakaenda mbele zaidi?

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo vyta Wizara mbalimbali na Taasisi za Serikali havikufanya vizuri. Kwa hiyo, kila Waziri hapa na Taasisi zake, achukulie kuwa wana jukumu la kukusanya kodi siyo tu kuwaachia *TRA* kwa sababu wengine wanaweza kukusanya lakini wakakaa wakisema *TRA* ipo inakusanya, kwa hiyo sisi tutapata hela tu. Haiwezekani, kila mmoja abebe hili jukumu liwe jukumu la Taifa. Vilevile hela nyingi zinapelekwa kwenye Halmashauri, naona hela zinakwenda wao hawajishughulishi kufanya utafiti kuangalia vyanzo vyta mapato vipyta ili kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi imetoa mapendekezo mazuri ya kupanua wigo. Kambi ya Upinzani pia imetoa mapendekezo mazuri, kama Taifa mzichukue Ripoti zote hizi mbili mzifanyie kazi, mwone tutaongeza vipi katika nchi yetu. Tuna tatizo moja la ongezeko wa Watanzania; Watanzania tunaongezeka kwa wingi sana; asilimia tatu ya *growth rate* ya *population* katika nchi yetu. Ukiangalia wastani wa ukuaji wa uchumi ni asilimia 6.5. Ukichukua 6.5 ukitoa tatu tunazokula wenyewe kama Watanzania, zinabakia asilimia 3.5 ambazo ni asilimia ndogo sana kuleta maendeleo yanayotarajiwa. Tujitahidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye mambo yanayohusiana na Muungano. Tume ya Pamoja ya Fedha: Katika hotuba za miaka ya nyuma ninayo hapa ya 2007, angalau kipengele kimetajwa kutueleza nini kinaendelea, lakini mara hii Mheshimiwa Waziri ameamua kunyamaza kimya. Labda niseme ni ya Mheshimiwa Meghji ya mwaka 2007. Naomba kunukuu:-

"Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Tume ya Pamoja imewasilisha mapendekezo yake kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Mawaziri wa Fedha wa Serikali za Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wamekutana na kukubaliana kwamba kila upande ukamilishe uchambuzi wa mapendekezo ya Tume kuwasilisha maoni kwa Kamati ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar kwa Waziri Mkuu Kiongozi."

Nyingine ni ya Mheshimiwa Mustapha Mkulo, amezungumzia yaleyale. *"Mheshimiwa Spika Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zinaendelea na zoezi la kupitia uchambuzi wa Ripoti ya Tume na vigezo mbalimbali vitatolewa."* Hivyo hivyo, lakini ye ye

ameona hawezi kurudia *statement* hiyo ameamua kukaa kimya kabisa anaogopa labda atakuja kuulizwa hapa kwamba haya mambo yamekwendaje kila siku *statement* ni hizo hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu kwa Taifa letu. Kabla sijaendelea kuchangia, ningependa kuwasilisha salamu za Wananchi wa Jimbo langu la Busega kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuwapatia utawala wa kuwa na Wilaya Mpya ya Busega na Mkoa Mpya wa Simiyu katika dhima nzima ya kusogeza huduma karibu na wananchi. Lengo hilo limefikiwa na naomba Serikali iendelee kutoa msaada kwa sababu unapoanzisha Wilaya mpya ni vizuri kuziangalia changamoto kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama Mbunge na Mwakilishi wa Wananchi, natakiwa kujua Bajeti za Mikoa yetu na Wilaya yetu zipo katika fungu lipi ili niweze kufanya kazi yangu ya kufuatilia kwa karibu. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwani ni mwezi mmoja tu tangu ameteuliwa lakini ameweza kuwasilsha Bajeti nzuri ambayo ina mwelekeo.

Napenda kuipongeza Serikali kwa uwekezaji wa kimkakati kwa kujenga Barabara ya Ramadi - Mwigumbi kwa kiwango cha lami. Naomba wakandarasi waweze kupatiwa fedha kwa wakati ili ujenzi wa barabara hii uweze kukamilika kwa wakati. Napenda kushukuru sana kwa Miradi mitatu ya Umeme inayoendelea ya Nyashimo - Kalemela, Mwanangi - Badugu - Busami na Lamadi - Mkula. Jana nilikuwa naongea na Meneja wa *TANESCO* Mwanza, amesema kwamba, Miradi hii ratiba

yake inaendelea vizuri. Kwa hiyo, naomba kazi hii iendelee vizuri, Wananchi wa Busega waweze kutumia umeme huu kwa manufaa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuna utata mkubwa wa bei ya pamba na juzi katika kikao cha wadau wa pamba kule Mwanza, wameshindwa kuafikiana katika bei ya pamba kwa mwaka huu na hivyo msimu wa pamba umeshindwa kuanza. Mwaka jana pamba imenunuliwa zaidi ya shilingi 1,000 na sasa bei elekezi ni kwenye shilingi 500. Hili ni tatizo kubwa na limeleta hofu kubwa kwa wakulima. Pamoja na kwamba inaanjiri Watanzania wengi sana, takriban Wilaya 42 zinalima pamba kama zao la biashara, yaani Watanzania milioni 14. Tatizo la kutegemea bei ya Soko la Dunia, mimi nalionna limeendelea kuwa kubwa na sielewi kwa nini kama Tanzania tuendelee kutegemea bei ya Soko la Dunia. Namna gani tunaweza kubadilisha hali hii? Bei ya pamba inaweza kupangwa kutoka Tanzania kama tutawekeza kwenye viwanda vya pamba, viwanda vya nguo au vya nyazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaambiwa kwa utafiti wa haraka haraka, tunahitaji viwanda vya nyazi vinne ambavyo vinakadiriwa kati ya dola milioni 25 mpaka 40 kwa kiwanda na wafanyabiashara wapo tayari kuwekeza iwapo Serikali itatoa *guarantee* ili waweze kuwekeza. Viwanda vya nguo ambavyo vina uwezo wa kusindika takriban asilimia 30 ya pamba yote bado vinatozwa kodi. Kwa nini kodi hii haiondolewi?

Nashauri kodi hii iondolewe na Serikali ichukue dhamana ya kuwekeza katika viwanda vya nyazi. Mkoa wa Simiyu tupo tayari kuanza kujenga na maeneo yameshatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipokuwa akizindua kiwanda cha kuchambua pamba cha kule Bariadi aliahidi kwamba, angesaidia katika hili. Wananchi bado wanaikumbuka ahadi yake, tunaomba itekelezwe. Nimesikia

pembeni baadhi ya Watendaji wanamtia hofu Mheshimiwa Waziri kwamba, kuondoa VAT ni suala gumu na lina utata. Hivi inakuwaje rahisi kuondoa kodi kwenye mafuta yanayoingizwa kutoka nje, sukari kutoka nje, nyama na kuku kutoka Brazil, maziwa kutoka nje na inakuwa vigumu kuondoa kodi kwa mwekezaji wa Tanzania. Naomba hili Waziri uwe imara na usiyumbishwe. Unaweza ukakuta kuna Wafanyakazi wa Serikali wananaufaika na *syndicate* ya kuingiza bidhaa hizi kutoka nje. Nimeona kuna mpango mzuri sana wa kuendeleza zao la pamba na ningeomba Wilaya yangu ya Busega iwe Wilaya ya mfano na huu ni mpango wa Serikali na moja ya eneo ni kuimarisha viwanda vyta kusindika pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina utajiri isioutambua. hii ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa idadi kubwa ya mifugo. Tuna ng'ombe milioni 19.2, mbuzi milioni 13.7, kondoo milioni 3.6, kitimoto, samahani, nguruwe milioni 1.9 na kuku milioni 58. (*Kicheko*)

Pamoja na hayo, Bajeti hii haijajielekeza namna ya kufanya Sekta hii iweze kuliingizia Taifa mapato. Sijaona maji, sijaona mpango thabiti kuhusu majosho, viwanda vyta nyama, viwanda vyta maziwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ili wafugaji wasiendelee kusumbuliwa. Hii ni ajira tele; kwa mfano, mfugaji wa kawaida tu wa Kisukuma au wa Kibarabaig ama Mmasai, anaweza kuwa na ng'ombe 3,000. Ng'ombe 3,000 kwa hesabu ya bei ya chini kwa sababu Dar es Salaam ng'ombe anaenda mpaka shilingi laki nane, kwa bei ya chini nimekadiria shilingi laki tatu; mfugaji wa ng'ombe 3,000 anatembea na shilingi milioni 900,000. Shilingi milioni 900,000 ni uwekezaji mkubwa sana na wafugaji wa namna hii wapo wengi katika nchi hii. Hawa ndiyo wanasumbuliwa kutoka kule Ihefu, wanahama na ng'ombe kutoka Kaskazini na Magharibi ya Tanzania, wanapita Lindi, ng'ombe wanachakatwa mapanga kule Rufiji. Bilioni inachakatwa mapanga, Watanzania hatujitambui.

Mheshimiwa Spika, nchi za Uarabuni na nchi nyingi tu za Afrika zinatamani kuwa na utajiri huu. Sisi tunao tunauchezea. Nina wasiwasi dhamira na nia njema ya Rais ya kuanzisha Wizara hii inataka kupotea. Tunavyo vituo vya kuzalisha mitamba kama kule Mwanza Mabuki, lakini unakuta mfugaji wa jirani ng'ombe wake ni duni; yule anayezaa baada ya miaka mitatu, wakati kumbe kungeweza kuwa na ng'ombe wa mwaka mmoja na nusu ambaye ana uwezo wa kuzaa, anaweza kuwa na kilo 400 au 500 na akaleta nyama nzuri. Kwa kweli naona Serikali ni vizuri katika hili ijielekeze vizuri.

Mheshimiwa Spika, ningependa sana katika kuhitimisha au katika Hotuba ya Waziri wa Mifugo, Mabwawa ya Rwangwa, Chubutwa, Nyamigongwa na Mwabayanda ambako kwa sasa kuna msongamano mkubwa wa mifugo, yawekwe kwenye Bajeti. Tuna taasisi pekee ya kuendeleza suala la mifugo inaitwa *National Ranching Company (NARCO)*; Shirika hili lilitaka kubinafsishwa, liliwekwa kwenye receiver kwa zaidi ya miaka kumi. Kwa busara ya Rais, akasema kwamba, Shirika hili lisibinafsishwe ili liweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Cha kushangaza ni kwamba, Serikali haitaki kuweka fedha kule ili kulifanya Shirika hili liamke. Tunapeleka mabilioni ya pesa *TRL* zinaliwa tunapeleka tena, tunapeleka *ATCL* zinaliwa tunapeleka tena. Hili Shirika la *NARCO* linataka billioni kumi tu. Mheshimiwa Spika, lisaidiwe na nashukuru sana. (*Makof*)

MHE. CECILIA D. PARRESO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Waziri kama ilivyowasilishwa. Nianze kwa kuchangia suala la Pato la Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa, Uchumi wa Taifa umeshuka kutoka asilimia saba mwaka 2010 hadi asilimia 6.4 mwaka 2011. Sababu zinazotolewa na Serikali ni kwamba, kulikuwa na ukame, upungufu wa nishati na m dororo wa uchumi duniani. Serikali ni lazima iwe na mkakati thabiti wa

kuona hali hii haitokei tena na uchumi uweze kupanda mwaka hadi mwaka kuliko ambavyo sasa hivi uchumi unaonesha kwamba unashuka. Hii ni sambamba na kuwepo na nidhamu ya kazi kwa Watumishi wa Umma. Lazima tuhakikishe Watumishi wa Umma wanafanya kazi kwa muda unaotakiwa, matokeo ya kazi yanayofanywa yanapimwa na yamekuwa na ufanisi kiasi gani kwa nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia ni lazima Serikali ione ni namna gani ya kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima. Hili limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi; ni lazima Serikali ione namna gani tunapunguza matumizi hasa suala la *administrative cost* ni namna gani inapungua. Je, ni lazima Mkurugenzi fulani wa Wizara au Halmashauri aendeshe V8? Je, lazima Wakuu wa Idara wawe na magari fulani kulingana na mazingira yao? Sasa ni vyema Serikali iangalie kulingana na mazingira na jiografia ya nchi hii, tupunguze vitu au matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, ni lazima pia Serikali ione namna gani watu wake wanaweza kumiliki uchumi. Hii ni sambamba na kila mtu kuweza kumiliki ardhi, kumiliki nyumba, kumiliki maduka na hata biashara ndogondogo. Hapa ndipo tunaweza kupima kwamba, uchumi wa nchi sasa unapanda kwa kiasi gani, mwananchi mmoja mmoja anaweza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Pato la Taifa kwa mwaka 2011. Takwimu zinaonesha kwamba, kwa mwaka 2011 Uchumi au *GDP* kwa kila mwananchi ilikuwa asilimia 12, yaani shilingi 770,000 kwa mwaka 2010 na shilingi 800,000 kwa mwaka 2011. Kule mwanzoni takwimu zinaonesha uchumi umeshuka, hapa zinaonesha kwamba, kipato cha mwanachi kimekua. Je, huku siyo kuwadanganya wananchi? Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unapochukua au unapotaka kuangalia *GDP per capita* ya kila mtu unawaweza wananchi wote maskini na tajiri katika kapu moja, unakokotoa hizo hesabu kama wachumi wanavyofanya, ndiyo unapata mwananchi wa Tanzania kwa mwaka anaweza kuwa na kipato cha namna gani. Ni lazima Serikali iweke makundi tofauti. Huwezi kumlinganisha au leo tuseme tufanye tathmini: Je, yule mama yangu wa kule Karatu ambaye hata mlo ni shida, anakunywa uji. Ni kweli aliweza kwa mwaka 2011 kuwa na kipato cha Sh.469,000/=? Ni lazima Serikali ione kwamba hii *GDP per capita*, yaani pato la mwananchi kwa mwaka, inawekwa katika makundi tofauti.

Kuna makundi ya wananchi wa kipato cha chini waliopo vijijini, kuna makundi ya wananchi wa pato la kati ambao leo wanaweza kubadilisha mboga; anaweza kununua nyama, kesho akanunua samaki; na kuna mwananchi wa kipato cha juu ambaye yeye leo atafikiri aendeshe gari gani, aina gani ya gari imetoka, haya mambo mengine hayataweza kumgusa. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iangalie na kuona namna gani inatatau tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, wachumi wanasema kwamba unapoangalia viashiria vya ukaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja, kuna mambo kadhaa ambayo yanaweza yakaainishwa. Moja, ni ukuaji wa ajira, lakini kunakuwepo na *price stability* ya bidhaa na huduma, lakini kunakuwa na kutokubadilika badilika kwa *exchange rate* kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri haya ni mambo sahihi ambayo yanaweza yakatupelekea tukaona kwamba ni namna gani uchumi wa mwananchi wa Tanzania unaweza kukua. Lakini haya yote bado ni kitendawili, wananchi bado hawana matumaini. Wananchi wamekosa matumaini! Serikali inapaswa iangalie ni namna gani wananchi wa Tanzania wanaweza kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika naomba niongolee suala la mfumuko wa bei. Takwimu zinaonyesha kwamba, mfumuko wa bei uliopo sasa hivi upo katika *double digit*, yaani mfumuko wa bei umechangiwa sana na bei ya bidhaa ya vyakula. Kulingana na takwimu, inaonyesha asilimia 25.3 kwa mwaka 2012, hii ilichangiwa na bei ya vyakula.

SPIKA: Wenzio wanalamika kwamba unasoma.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, sisomi, nime-*note point* ndiyo naziangalia na takwimu.

SPIKA: Endelea.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa nanukuu takwimu hapa kwamba, mfumuko wa bei upo katika *double digit* kwa sasa kulingana na takwimu na kwa mwaka huu, April, 2012 takwimu zinaonyesha kwamba mfumuko wa bei ya vyakula upo asilimia 25.3. Sasa mfumuko huu wa bei usipimwe tu kwa bei za bidhaa bali upimwe kwa kuangalia ni namna gani mtu mmoja mmoja anaweza kumudu kununua vifaa hivi au bidhaa hizi za vyakula.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee pia kwenye suala la deni la Taifa. kulingana na Muhtasari wa sera ya Benki Kuu, deni la Taifa linaonekana kuwa ni Dola za Kimarekani elfu kumi na mbili mia tano themanini na tano milioni. Hii ni sawa na asilimia 79 kwa madeni ya nje, na madeni ya ndani ni sawa sawa na asilimia 21.

Mheshimiwa Spika, tunajiuliza, kama Tanzania tuna raslimali nyingi kiasi hiki: Je, tumeshindwa kutumia raslimali hizi? Kwanini tunaendelea kukopa, na kukopa huku ndiko ambako kunakuja kutuathiri katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii? Kama tunaendelea kukopa na tuna hizi raslimali, tunashindwa kuzitumia, ndivyo ambavyo nchi za nje zinaweza kuja kutuwekea masharti ya wanayoyataka wao. Ina maana

kwamba tutashindwa kuamua, tutashindwa kusimamia tulichonacho, tutaendelea kuwa wategemezi mpaka lini? Ni lazima Serikali ituambie, ni lini inaacha utegemezi huu? Ni lini haitaendelea kukopa? Ni kwa namna gani wananchi wa Tanzania wanafaidika na rasilimali zao?

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kueleza kidogo kuhusu ukuaji wa kisekta. Takwimu zinaonyesha kwamba, ukuaji wa kisekta kwa mwaka 2011 hasa kilimo, ilikuwa asilimia 3.6 dhidi ya asilimia 4.4 mwaka 2010. Kwa hiyo, utaona mwaka 2010 kwenye suala la kilimo angalau sekta hii ilikua lakini mwaka 2011 sekta hii ilishuka. Kama tunasema kilimo ni uti wa mgongo na bado tunaona kwamba suala hili linashuka, Serikali ina mkakati gani? Je, haioni upo umuhimu wa kuwekeza katika maeneo ambayo wanaweza wakalima, kukawepo na mifumo mizuri ya umwagiliaji hata kama kuna mvua, hakuna mvua, kuna ukame, lakini kama kuna *irrigation system* nzuri, wananchi wataendelea kulima na kupata mazao.

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali ni vema ikayasimamia haya na wananchi wakanufaika kulingana na rasilimali walizonazo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kidogo mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2011/2012. Taarifa inaonyesha kwamba, ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa ilishuka na kuwa asilimia 57 ya lengo lilllokusudiwa. Sababu kubwa inayotolewa na Serikali hapa ni kwamba ilichelewesha kutoa agizo kwa Serikali za Mitaa kuweza kukusanya tozo ya ada za leseni.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri atuambie ni kwanini walichelewa na hatua gani zilichukuliwa? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Mariam Kisangi, na Mheshimiwa Christowaja, ameomba achangie baadaye, anaumwa. Atafuatia Mheshimiwa Dokta Limbu.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Kikao hiki cha Sita, napenda kukipongeza Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dar es Salaam na Jumuiya zake kwa kazi kubwa waliyoifanya.

SPIKA: Hiki Kikao ni cha Nane.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, Kikao cha Tano.

SPIKA: Cha Nane!

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Nane.

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwapongeze Waziri wa Fedha na Manaibu wake na Watendaji wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa waliyoifanya kuandaa bajeti yetu nzuri.

Baada ya hapo, napenda niipongeze Jumuiya yangu ya UWT Mkoa wa Dar es Salaam hususan Wilaya ya Temeke na leo natambua mpo kwenye shughuli kubwa ya Baraza la UWT, nawatakia kila la kheri, huo ni mgawanyiko tu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza bajeti binafsi, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na sababu ninazo. Nikiwa kama Mbunge wa Mkoa wa Dar es Salaam katika Bunge hili na katika bajeti hii ya Serikali iliyopita, nimeweza kuongelea masuala mbalimbali ya umeme katika Mkoa wangu na kweli mipango ile ya maendeleo katika Mkoa wa Dar es Salaam imetekelzeza na mpaka sasa hivi Kandarasi wako *site*.

Mheshimiwa Spika, niliomba msongo wa umeme uangaliwe. Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam walikuwa

wanapata kero kubwa ya kukatikakatika kwa umeme. Juzi *TANESCO* walikabidhi mtambo wa umeme wa Kisitu na tayari mtambo wa Mbagala upo tayari, siku yoyote utakwenda kufungwa pale na mtambo wa umeme wa Ubungo pia upo tayari. Lakini pia wa Kijitonyama upo tayari. Hayo yote niliyasema kupitia Bunge hili na Kamati yangu ya Nishati na Madini. Hayo si madogo na sina sababu ya kutounga mkono bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, katika bajeti yetu nitachangia katika maeneo yafuatayo. Nitachangia mfumuko wa bei, nitachangia pia vyanzo vya mapato pia kodi za pikipiki na magari. Nikianza na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, suala la mfumuko wa bei ni suala zito sana kwa Serikali yetu. Pamoja na bajeti hii nzuri, kila kilicho kizuri hakikosi changamoto zake. Hakuna mwanadamu timilifu, wala hakuna jambo timilifu, hilo ni lazima tulikubali. Lakini tuangalie katika suala zima la mfumuko wa bei na hasa katika Miji Mikuu na Jiji la Dar es Salaam. Wananchi wamekuwa wakipata shida sana ya maisha kwa kupandishwa kwa bei za vyakula; naishauri Serikali yangu sikivu ya CCM, sasa tuangalie mpango wa chakula cha ndani. Tuagizieni mchele wetu wa kitumbo na ile chereko chereko yetu ya Thailand ili kupunguza bei za vyakula.

Kama kweli leo Serikali inaagiza mchele kutoka nje, unafika Dar es Salaam unatakiwa uuzwe kwa Sh. 1,580/=, lakini kutokana na uroho wa wafanyabiashara, unauzwa Sh. 2,000/=, nina imani mchele ukiagizwa kutoka nje mpaka utakapoingia Dar es Salaam hautazidi Sh.1,200/=. Hiyo itasaidia sana wananchi kupunguza angalau mfumuko ule wa bei na chakula angalau vitapatikana kwa urahisi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri ya kuendeleza kilimo tunaikubali mipango yote, lakini kwa wingi wa watu waliopo Dar es Salaam ambao tunakula vyakula vya

Mikoa yote, naona kuna haja ya Serikali kupanga mahsusia pia kuagiza hivi vyakula, lakini pia kusimamia ugawanyikaji wa hivi vyakula.

Mheshimiwa Spika, unaona vyakula vingi vinashuka katika bandari, magodauni yanajaa, lakini hatujui vinakwenda wapi. Ukienda sokoni unakuta mchele ule ule unaotoka Mbeya, unaotoka Rukwa, unaotoka Shinyanga, unakuta unga wetu ule ule. Mahindi tunaambiwa yanakuja msaada, lakini hatutofautishi kipi kimeletwa kwa msaada au kimekuja kwa ajili ya shughuli maalum, na kipi kinauzwa na wafanyabiashara. Naiomba Serikali yangu sikuvi ikalismamie hili suala kwa umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, nitakuja katika eneo lingine la vyanzo vya mapato, hivi vyanzo vya mapato kutegemea sigara, pombe na soda, mimi toka ninakua nasikia vyanzo ni hivi hivi tu. Hebu tubadilike sasa, tuangalie na vyanzo vingine vya mapato. Ninasema hivyo, ninazo sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, vyanzo vya mapato kupatikana kwa soda; soda kwenye miji mikuu siyo kinywaji, bali ni chakula. Ukipita kila ofisi, mashulenii, vyuoni; Vyuo Vikuu Mlimani, Chuo cha Maendeleo ya Jamii na vyuo vyote vilivyojaa watoto wetu wanaponea soda na *chips* dume. Soda moja haitumiki kama kinywaji, lakini sisi wote tunawapa watoto wetu wa Shule za Sekondari za *boarding pocket money*, wanaishia kununulia soda. Madarasani huko hakushiba, anakwenda kujazia tumbo kwa soda na biskuti. Kwa maana hiyo, tukiangalia hiki chanzo tutaua watoto wetu tuangalie na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, ningekuwa nashauri kama mimi, ningesema soda kwa vile ni kinywaji kinachopendwa, kuongeza bei ya kitu, si kufanya kiuzwe sana. Unaweza ukaongeza bei, ukapunguza mauzo, na mapato yasipatikane.

Mara nyingine ukipunguza bei, unaongeza mauzo na mapato yanakuwa makubwa. Hebu tuwe wajasiriamali sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende kwenye eneo la kodi za pikipiki na magari. Naomba Serikali iangalie hawa watu wenye pikipiki na wenye magari. Hawa wenye pikipiki wamejajiri, wametupunguzia vibaka, wale wengine waliokuwa hawana kazi wamejajiri. Kitendo cha kuwaongeza kodi hawa watu, kwa kweli tunawatesa. Tunachotakiwa sasa hivi tuwaambie wajunge hata na Mifuko ya Bima kile kidogo kwa sababu hawa watu wanavunjika mno. Wamejaa kule MOI wamevunjika. Kwa maana hiyo, wanapovunjika, nayo inakuwa ni tatizo kubwa wao kujitibia, badala ya kuwaambia wakatwe kodi. Mimi naomba Serikali tushauriane, tuwaondolee hii kodi ya pikipiki na wenye magari pia.

Mheshimiwa Spika, *tax driver* sasa hivi biashara yao imepungua sana, wanaifanya kwa msimu; mpaka msimu wa kupeleka wanafunzi shulenii ndiyo utakuta *tax driver* wanachangamka na sikukuu. Sasa unapoangalia kodi, kwa wao inakuwa ni tatizo. Lakini naomba niishauri Serikali yangu kwamba, tukikusanya kodi vizuri kwa kuangalia maeneo kama *warehousing bonded*, eneo hili kama litasimamiwa vizuri, na silielewi, hivi *ware housing bounded* ufunguo anakaa nao yule mtu; yule mtu tumemlisha yamini gani sis?

Mheshimiwa Spika, naomba eneo hilo liangaliwe. Lakini kodi za majengo zikikusanywa vizuri tutapata mapato mazuri na kuendeleza Halmashauri. Lakini napenda ziangaliwe hizi *bureau De change*. Hizi wanazi-monitor Benki Kuu, lakini mnaziweza jamani? Mbona kuna za uchochoroni? Hebu tuangalie maeneo haya, badala ya kuangalia tu vyanzo vya soda, bia na maji.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni mimi, soda na maji kwa vijana au kwa nchi yetu hapana, kwa watoto wetu wa shule

kwa kweli ni tatizo kubwa. Ningombwa sana Serikali iangalie maeneo haya. Lakini pia naomba nitoe salamu zangu kabla sijamaliza kwa walimu wenzangu.

Mheshimiwa Spika, walimu wenzangu na mimi nina-declare *interest*, ni mwalimu na mjasiriamali. Naomba mtuamini, tupo Bungeni tumetoka huko huko kwenye hizo chaki, tutawasemea mambo yenu bila uwoga na kwa uwezo wa Serikali yetu sikivu ya CCM, itatekeleza mahitaji yenu bila vurugu.

Mheshimiwa Spika, nawaomba walimu wenzangu msishawishike, tupo hapa kuwawakilisha ninyi na tutawawakilisha mpaka dakika ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, sasa nimwite Dkt. Limbu kama yupo. Okay, hayupo. Mheshimiwa Augustine Massele kama yupo, atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

MHE. AUGUSTINE M. MASELLE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mchana huu bajeti ya Serikali ambayo imewasilishwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia kwa sababu bajeti hii inalo lengo la kutusaidia sisi Watanzania kwa kadri ambavyo tunataka.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali ya CCM kwa kutuanzishia maeneo mapya ya utawala ili kusogezza huduma kwa wananchi. Jimbo langu limetengwa kuwa Jimbo na hatimaye kuwa Wilaya. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, Mbogwe haikuwepo katika ramani ya Tanzania, lakini kwa sasa milele na milele imeandikwa. Hongereni sana Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote ili iweze kwenda mbele inahitaji kuwa na vyanzo vya uhakika vya umeme. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja ya Serikali ya kuimarisha vyanzo vyake vya umeme ikiwemo kuleta gesi ya kutosha pale Dar es Salaam na vile vile kuimarisha chanzo cha umeme kule Mwanza. Kuimarika kwa chanzo cha umeme Mwanza kutahakikisha kwamba umeme unapatikana kwa uhakika Mkoa wa Geita na kwa maana hiyo tutapata umeme wa uhakika Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Serikali, ipo mipango maalum ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha reli ya kat. Katika kuimarika kwa reli ya kat, upo pia mpango wa kujenga reli itakayokwenda nchini Rwanda. Reli hiyo itapita katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Mbogwe. Kwa hiyo, kuwepo kwa reli katika maeneo yetu kutarahisisha usafirishaji. Kwa maana hiyo, kutarahisisha maendeleo ya wananchi wa Jimbo langu na Wilaya yangu ya Mbogwe. Hongereni kwa hilo pia.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia hotuba ya Waziri na niombe kwamba utekelezaji wake uwe wa uhakika, kwa maana ya kwamba katika Jimbo la Mbogwe. Sisi ni wakulima wazuri wa Pamba, ni wakulima wa Mpunga na ni wafugaji pia. Kwa kuwa tuna mifugo ya kutosha, tunao uwezo wa kulima. Serikali imeamua kuwa na Benki ya Wakulima, lakini kuna tatizo moja kuwa, wananchi katika Jimbo letu la Mbogwe wamekuwa makini na wameweza kuwa na utaratibu wa kupata hati za kimila za kumiliki ardhi. Lakini kwa masikitiko makubwa, hati hizi zinakataliwa na Benki ya *Tanzania Investment Bank (TIB)*, wakidai kwamba hati hizi zinaanzishwa kisiasa. Sina uhakika kama kweli maelezo ya watalaam hawa ni sahihi na kama siyo sahihi. Naomba wakati wa majumuisho,

Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa namna gani wakulima na wananchi ambao wanazo hati zao za kimila watazitumia? Kama Serikali inazitambua, basi itoe tamko la kuweza kuzipokea ili kusudi tuweze kuboresha maisha ya wananchi wetu kwa kuwasaidia kuwapa nyenzo za kuweza kufanyia kazi, maana wakipata mikopo wanaweza wakanunua matrekta na wanaweza wakaboresha maisha yao kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara katika nchi yetu ni kweli limepewa kipaumbele, na kwa hakika nchi hii pasingekuwa na mpango kabambe wa Serikali wa kuzijenga barabara kwa kiwango cha lami, nchi hii nadhani tungelikuwa tuko nyuma sana. Maana nakumbuka kuna kipindi mtu aliyekuwa anatoka katika Mikoa ya Mwanza na Kanda ya Ziwa akifika Singida alikuwa hawesi kufika Dar es Salaam, kwa sababu ya kukwama. Wakati ule ililazimika kuzunguka nchi jirani ya Kenya. Lakini kwa sasa Watanzania wanatoka Mwanza na kufika Dar es Salaam siku hiyo hiyo. Haya ni maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa kwamba uimarishaji wa barabara uende sambamba na kuimarishwa kwa reli ya kati. Reli hii ya kati wakati itakapokuwa inafufuliwa na kuanzishwa kuwa katika *standard gage*, naomba Serikali ichukue hatua madhubuti za kuibadilisha kuwa ya umeme ili kusudi usafirishaji wa mizigo na watu kutoka Dar es Salaam na kwenda katika nchi nyingine za jirani uweze kuwa wa uhakika kama ambavyo sasa hivi barabara zinatusaidia.

Mheshimiwa Spika, nina imani kabisa kwamba, reli ikianza kuwa kasi na barabara zetu zikawa katika nafasi nzuri, bidhaa ambazo zinazalishwa katika eneo la Dar es Salaam ambako ndiko kuna viwanda vingi ikiwemo sementi na vitu vingine ambavyo vinaagizwa kutoka nchi za nje, vitafika katika maeneo mbalimbali ya Tanzania kwa bei nafuu, na kwa maana hiyo, upo uwezekano mkubwa wa kupunguza mfumko wa bei katika nchi hii kwa maana ya *inflation*.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* wamefanya kazi nzuri sana. Sasa tunalo tatizo katika barabara za vijijini, na katika Halmashauri, nami niungane na wasemaji wengine walio tangulia kwamba ikiwezekana kuanzishwe na wakala wa barabara za vijijini ili kwa mtindo ule ule ambao tumeweza kufanikisha kwa kuwa na *TANROADS*, basi na barabara za vijijini zipate mlezi ambaye atakuwa anazisimamia na nina uhakika kwamba tukiwa na barabara za uhakika vijijini maisha vile vile yatakuwa katika hali ambayo inaridhisha.

Mheshimiwa Spika, nchi hii imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi. Kuwepo kwa rasilimali hizi kunaifanya Tanzania siku za baadaye kuwa Taifa kubwa. Kinachotakiwa sasa, niwaombe Watanzania wenzangu ambao wameajiriwa katika Sekta ya Umma wabadi like katika mtazamo ili kusudi wawe wazalendo.

Mheshimiwa Spika, hela ambayo tunaipitisha leo katika ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

SPIKA: Kengele ya pili. Ahsante.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu Subhanah-wa-taallah kwa ajili ya uzima na afya njema kwa ajili ya kuchangia bajeti hii mwaka 2012/2013. Nikiwa hai na uzima katika mwezi huu Mtukufu katika dini ya Kiislam, naomba Waislam wote popote pale walipo angalau wafunge siku moja kwa uwezo wa Allah.

Baada ya kusema hayo machache, nianze kwa kusema kwamba, bajeti hii ambayo haikuzingatia usalama wa wananchi wake katika wanaoishi katika mwambao wa Bahari ya Hindi, bajeti ambayo haikuangalia usalama wa wananchi wanaoishi katika maziwa mbalimbali, bajeti ambayo haikuzingatia wananchi wake wanaoishi katika mito mbalimbali, basi kwangu mimi ni bajeti ya kiini macho; kwangu

mimi naona kitendawili na bajeti ya funika kombe mwanaharamu apite. Siungi mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu, ukiangalia kwenye ukurasa wa 47 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amegusia kuboresha barabara, nakubali; reli, treni, usafiri wa anga na viwanja vya ndege. Pia akazungumzia namna gani ya kuendeleza kujenga gati katika Ziwa Tanganyika, nakubali. Lakini inapofikia wakati ukasahau wananchi, wapigakura ambao wanaendelea kufa, ajali zimeongezeka katika mwambao wa bahari ya Hindi, wanaishi katika visiwa, katika maziwa mbalimbali, kwa kweli hatujawatendea haki wananchi wa maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haijachukua muda mrefu Serikali ilikuja Zanzibar pale baada ya kutokea maafa makubwa. Tunapozungumzia jambo hili unaambiwa kwamba lile ni la Zanzibar. *TRA* ni taasisi moja inakusanya mapato. Kwa msingi huo, ikiwa hali ya usalama wa wananchi wanaotoka Pemba kuja Unguja, wanaotoka Dar es Salaam kwenda Mafia wanaotoka Dar es Salaam kuelekea Mtwara kuitia kwenye maji, wanaotoka katika Ziwa Victoria hawakupewa vyombo vinavyostahili meli za uhakika na boti za uhakika, hili ni tatizo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, ajali ambazo zimekuwa zikitokea hivi sasa, inaonekana meli zetu zimechakaa na boti zetu zimechakaa. Leo hii Serikali nikiuliza mna mkakati gani wa kuandaa mazingira, kupatikana kwa meli ya uhakika ambayo itaondoka Dar es Salaam kuelekea kwenye Kisiwa cha Mafia, hakuna. Ni maneno yale yale ya siku zote! Serikali ina mkakati gani wa kupatikana kwa meli ya uhakika na boti za uhakika ambapo katika Ziwa Victoria Boti zilizopo zimechoka kupita kiasi?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia M.V. Victoria, imechoka; M.V. Serengeti, M.V. Clauras nazo zimechoka. Usalama wa

wananchi katika maeneo haya uko wapi? Kwenye Ziwa Tanganyika M.V. Liemba ni ya zamani nayo imechoka, M.V. Songea, M.V. Iringa kwenye Ziwa Nyasa imechoka. Serikali imekuwa bingwa wa kupeleka salaam za rambirambi na ubani, watu wamechoka!

Mmекуwa mабingwa wa risala baada ya vifo kutokea. Salaam za rambirambi mpaka lini? Wananchi wanateseka, tumesema mara nyingi, lakini kila tunaposema, mnasema mko katika michakato, mipango kabambe mmeandaa, kupatika kwa boti nzuri na meli za uhakika, lakini hakuna kilichofanyika. Ni mara ngapi wananchi wanaoishi katika Bonde la Mto Rufiji wamekufa? Lakini hakuna utaratibu wa kupelekewa boti za uhakika katika maeneo haya. Tatizo ni nini? Mmebagua wananchi katika maeneo haya, tatizo ni nini? Mnabagua wananchi katika maeneo haya, mkiri na mkubali.

Mheshimiwa Spika, tunapokosoa, tunaipa Serikali nguvu angalau iandae mazingira mazuri ya kuweza kuwasaidia wananchi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atueleze, awafahamishe wananchi ambao wako katika maeneo niliyoyataja, Serikali ina mkakati gani wa ziada? Katika ukurasa huu ukiangalia ambao mmeeleza katika ukurasa wa 47, hamna mkakati ambao mmegusia waziwazi. Je, maeneo niliyoyataja ili kupunguza vifo hivi na ajali zinazotokea: Je, mna mkakati gani wa kuweza kuwasaidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa kusema kwamba katika hali ambayo siyo ya kawaida, kitabu hiki ukurasa wa 25 inaelezea habari ya MKUKUTA. Ukurasa wa 49 maendeleo ya viwanda, ukurasa wa 55 kupanua fursa za ajira. Pia kwenye ukurasa wa 49 wameelezea namna ya kuendeleza viwanda vilivyopo nchini na wametenga Shilingi bilioni 128.4.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali haikusema na wala haijaaeleza wazi wazi kuwaambia Watanzania ni jinsi gani hivi viwanda ambavyo vilikufa mmeviua mtavifufua? Sasa mnaboresha je maisha ya wananchi kupidia mkakati wa MKUKUTA kuongeza ajira kwa vijana, lakini kuna viwanda ambavyo mlivirithi na miliwa navyo, lakini mkaviua, lakini hadi leo hamjavifufua? Serikali ituambie mkakati wake wa kuweza kufufua viwanda vya Korosho Kusini. Uko wapi mkakati na bajeti wa kufufua Viwanda vya Korosho vya Lindi Mjini, viwanda vya Nachingwe, Mtama, Tunduru na maeneo mengine ya Kusini?

Mkakati uko wapi? Hakuna mkakati wowote kwa Serikali, ninyi mnasema MKUKUTA. Baya zaidi, kila mnapopita katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu wanasema: "Tumethubutu, Tumeweza", mmethubutu na mmeweza kuua viwanda ambavyo hamwezi kurudisha? Tatizo ni nini? Tumethubutu, tumeweza tunasonga mbele. Mnasonga mbele kuua viwanda vingine? Andaeni mazingira mengine, Serikali mkubali mkakati ni upi, tuambieni kwa dhati kabisa mna mkakati gani wa kuweza kufufua viwanda vya nguo ambavyo havipo. Magunia Moshi iko wapi? Mkakati upi ambao mnao wa kufufua Kiwanda cha Magunia kule Moshi?

Mtuambie kule Mang'ula Morogoro mna mkakati gani Serikali? Mnazungumzia ajira kwa vijana, lakini kumbe mipango yenu ni ya mdomoni, haina udhati wa maneno na vitendo, mtuambie hali halisi ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inatia uchungu sana kuona kwamba siku zote Serikali ina mabango kwenye barabara, "Tumethubutu, Tumeweza." Mtuambie namna gani mnaweza kuboresha maisha ya wastaafu. Wastaafu mmewasahau kabisa! Leo wastaafu wanaondoka Dar es Salaam kuja Dodoma Bungeni kwa sababu mmewasahau, umaskini umezidi na hakuna mkakati wa dhati ambao unaonekana katika kitabu hiki cha kuboresha maisha ya wastaafu. Pensheni yao ni

ile ile hata mafao yao wanayopata siku zote wanapunjwa. Unaambiwa ni tatizo la kukokotoa. Majalada yao siku zote ambazo wanachukuliwa, unaambiwa kwamba wastaifu wamepunjwa. Tatizo nini? Kukokotoa! Watalaam hamna! Si aibu! Serikali hamwoni haya. Tatizo ni nini? Serikali ijirekebishe. Yale ambayo sisi Wabunge tunasema hatupigi kelele na kwa sababu leo ni mwezi Mtukufu huu wa Rajab, sisemi sana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme kwamba muandae mazingira, yale mambo ambayo sisi tunaleta kwenu mzingatie. Sisi tuna akili zetu timamu, tunawasemea wananchi katika maeneo wanayopata shida. Leo unapompa mstaifu Sh. 50,000/= apate nini? Leo hii unapokaa na ukaangalia kwamba majalada yaliyochukuliwa yangeliwa pungufu, Shilingi milioni 400 na zaidi, tatizo ni nini? Ndiyo siku zote tu. Unapohoji mambo haya kwamba tatizo ni kukokotoa, mbona hamzidishii walio wengi wastaifu? Wako njiani wanakuja. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nakuomba wakifika hapa tuwapokee kwa utaratibu, waeleze yao waliyonayo, wako taabani, wamekuwa maskini, wastaifu watoto wao maskini, hawana uwezo wa kusomesha. Kumbe kuwa mstaifu katika eneo hili au katika wakati huu sijui ni jambo gani? Lakini jambo baya sana ambalo Serikali inafanya...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii. (Makof)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naona muda wetu hauwezi kutosha, dakika tano mtu kuweza kuchangia hautoshi. Hapa nimeletewa nitangaze jambo moja kwamba yuko Kapteni ambaye ni Nahodha Injinia Ramo Makani, halafu yupo na Kapteni Msaidizi, lakini anasema ni wa muda;

Mheshimiwa Charles Kitwanga Mawe Matatu, anaomba niwatangazie Wabunge wachezaji na wapenzi wa mchezo wa mpira wa kikapu (*Basket Ball*) wajiorodheshe kwa kupitia hawa niliowataja, Mheshimiwa Injinia Ramo Makani na Mawe Matatu.

Walifikiri kwamba ili tuweze kuanzisha mchezo huu na kuongeza idadi ya michezo kwa *Bunge Sports Club*, kwa hiyo, kama kuna watu watakuwa wanapenda kujiunga katika mchezo huu wa mpira wa kikapu, basi Kapteni na Msaidizi wake mnaweza kujiandikisha kwao.

Halafu lingine wakati Mheshimiwa Mbunge mmoja anazungumza, alisema nashangaa kabisa wajibu wa Wabunge kuisemea Serikali. Bunge ni mahali pa *dialogue*, siyo mahali pa mapambano. Wakati wa Chama Kimoja ndiyo kulikuwa na upande mmoja wanasema *front bench* na kwingine Wabunge. Lakini hapa ni *dialogue*. Tunachotakiwa kwa uhakika kabisa tuseme ukweli kwa wananchi kwamba hiki kinatendeka, hiki hakitendeki. Tukifanya hivyo, tunawasaidia wananchi kuelewa nini kipo na nini hakipo. Lakini kama ni kutupa mawe tu wakati wote, hilo siyo Bunge. Bunge ni *dialogue* kwa wote wanaofanya kazi ya kuzungumza.

Nawashukuru sana, kwa leo mmejitahidi vizuri sana kuongea bila kurushiana matonge, na matope yasiyokuwa na maana na wananchi wanalalamika. Tuendelee na utaratibu huu kusudi tuweze kutoa faida kwa wenzetu wanaopenda kusikiliza kipindi chetu, waone hapa pamezungumzwa jambo la muhimu. Tunajua akili ni nywele, kila mtu ana zake. Lakini kutukana hapa, hii ni makusudi. Kwa hiyo, naomba tuwe makini. Hakuna tangazo lingine.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.58 jioni Bunge lillahirishwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, asubuhi Mheshimiwa Spika alitaja watakaokuwa wanachangia kwa kuanzia jioni ya leo. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Anastazia Wambura na atafuatiwa na Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji. Mheshimiwa Wambura, dakika kumi.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kukata utepe jioni hii, maana yake nimekuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii. Kwanza kabisa, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amatulinda salama hadi kufikia siku ya leo. Nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuzindua Mpango wa Kuboresha Elimu ya Msingi Mkoani Mtwara tarehe 15 mwezi wa sita mwaka huu, na hizo ndizo kazi za Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutuonyesha katika bajeti hii kwamba mwaka huu ndiyo inaanza rasmi kutekeleza mpango wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano. Naipongeza sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Pamoja na kazi nzuri iliyofanyika katika kuandaa bajeti hii, nina wasiwasi mmoja mdogo kwa upande wa bajeti ya maendeleo na ni katika lile suala la kupunguza bajeti kutoka asilimia 37 mpaka asilimia 30. Kwa kweli nina wasiwasi mkubwa kwamba kama tutakwenda na mtindo huu, tunaweza tusiweze kufikia dira yetu ya Taifa mwaka 2025 hapo utakapofikia mwaka. Labda kama tutakuwa kila tunapopunguza, kwa sababu sijui kama mwisho wetu ndiyo hapa kupunguza au pengine mwakani tena tukiona kwamba hatukutimiza malengo, tutapunguza zaidi na

kama tutakwenda kwa mtindo huu, basi nadhani tunaweza tukajinyima fursa ya kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wangu, nilikuwa naomba tuendelee kuwa na malengo ya juu ili kusudi tuweze kuchota fursa tulizonazo za utajiri wetu na hapo tunaweza tukafikia vizuri malengo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu nimnukuu mwanafalsafa mmoja anaitwa Less Brown ambaye anasema kwamba: "*Most people fear not, because they aim the highest and miss; it is because they aim the lowest and get.*" Kwa mtindo huu, basi niseme, tutakapokuwa na malengo ya juu katika bajeti yetu ya maendeleo, kwa ujumla mimi nadhani itakuwa inatupa changamoto ya kujitahidi kufanya vizuri na vizuri zaidi na itatuwezesha sasa kuziishi zile ndoto zetu ambazo tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mchache, ningependa nishauri mambo mengi, lakini sasa labda nichukue tu maeneo machache ambayo naweza nikashauri kidogo kuhusiana na jinsi gani ambavyo tunaweza tukatumia fursa zetu kwa ukamilifu, fursa zile za utajiri tulionao ili kuweza kufikia ndoto zetu. Labda nianzie kwa upande wa madini. Upande wa madini, mimi nina wasiwasi sana kama kweli tunapata tunachostahilli kukipata. Tunasema, angalau tumeongeza mrabaha, sijui wanaita mrabaha au mrahaba tunapata sasa hivi 4%. Lakini nani ana uhakika kwamba hii ni 4% ya ile 1% ya msingi ya ukokotoaji wa huu mrabaha? Pengine tunakuwa tunapata 4% ya 10% au tunapata 4% ya 5%.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, katika eneo hili, Serikali ihakikishe kwamba inakuwa na mkakati wa uhakika wa kuhakikisha kwamba hicho tunachokipata ni kweli kinatokana na ule msingi wa ukokotoaji. Kwa sababu kumekuwepo na malalamiko siku nyingi tu kwamba kule kwenye maeneo ya madini hakuna wanaoruhusiwa kuingia, taasisi nyingi kwa

mfano *TRA* au watu wengine, vyombo vingi ambavyo vinaweza vikadhibiti yale mapato. Siyo rahisi kuingia, sijui kama sasa hivi kuna mabadiliko yoyote. Lakini kimsingi, nilichokuwa naomba ni kwamba ufanyike ufuatiliaji wa kuhakikisha kwamba hii 4% ni ya 1% ya msingi wa ukokotoaji na siyo vinginevyo, na ni afadhali tukapata 1% kutoka 100%, kuliko tukapata 4% kutoka 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni lile la mafuta. Sasa hivi tuna utafiti wa mafuta. Unafanyika maeneo ya Mtwara na kwingineko na kuna kampuni moja kubwa tu ambayo iko kilometa 200 baharini kutoka Pwani ya Mtwara na hawa wanafanya utafiti wa mafuta na sijui kama kweli Serikali yetu ina uhakika kwamba ni lini utafiti huu utakamilika, sijui. Lakini hata hivyo, sijui kama kuna ulinzi wowote unaofanyika, na sijui, sina uhakika kama kweli tunajua kwamba kinachofanyika pale ni utafiti tu na siyo biashara nyingine. Kwa maneno mengine, sijui kama tunaamini kwamba hakuna kunachoibiwa kutokana na utafiti huu wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe tu mfano, wakati gesi imevumbuliwa Mtwara kabla ya wawekezaji hawa wa *ARTUMAS* ilivumbuliwa kule Mtwara na baadaye ikawa inakuja meli kule Pwani ya Mnazi Bay na Serikali ilipoona hivyo, ikapiga marufuku ile meli isiwe inakuja na ikaweka ulinzi mkali sana. Sasa sijui kwa upande wetu wa mafuta tunafanyaje. Hilo ni eneo la kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la bei za mazao kwa wakulima limezungumziwa sana. Nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu ambao wametangulia kutoa mapendekezo kwamba ufumbuzi pekee wa mgogoro wa bei za mazao kwa wakulima, bei ya korosho, bei ya pamba ni kwa njia ya kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spiaka, nawaomba wafanyabiashara wa nchi hii, wafanyabiashara wenyewe uwezo, waige mfano wa Bakhresa ambaye mara ya kwanza tulipiga kelele sana hapa Bungeni kuhusiana na suala la kusindika matunda katika nchi yetu. Matunda yalikuwa yanaharibika sana, lakini yeye *al-respond*. Sasa ameinua sana sana bei ya matunda katika nchi yetu. Kabla ya kuanzisha viwanda vya matunda, tulikuwa tunanunua embe kwa Sh. 50/= Vijijini, lakini sasa hivi ukienda kule Vijijini utapata Sh. 300/= hadi Sh. 500, na juu ya hayo pia ameongeza ajira. Vijana wetu wamepata ajira na ukienda mashambani hutakuta matunda yanaharibika au yanaozea shambani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuiomba Serikali sasa iwatambue wafanyabiashara wa aina hii, ikiwezekana iwake tuze na wao wenyewe wajisikie kwamba wana mchango muhimu katika Taifa hili. Lakini vile vile, iangalie suala la kodi, sasa ili kusudi iweze kuwapa nguvu, waendeshe viwanda hivi vizuri kwa manufaa ya wakulima wetu na kwa manufaa ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niachie hapo kwa upande wa mazao, labda tu kuhusiana na mkopo, deni la Taifa. Kuna mbunge mmoja hapa asubuhi amezungumza vizuri sana kuhusiana na ustahimilivu wa deni la Taifa. Mimi namuunga mkono Mbunge huyu. Lakini pia nichukue nafasi hii kuiunga mkono Serikali kwamba ni vizuri sasa ikafikiria suala la kukopa kiasi cha fedha kinachotosha kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo la kwanza ambalo ningependa kushauri kwamba Serikali ielekeze mkopo huu, ni katika kuhakikisha kwamba vitambulisho vya Kitaifa vinapatikana haraka ili kusudi kuiwezesha Serikali kupata kodi na mapato zaidi kutoka kwenye ile sekta isiyo binafsi kama walivyokuwa wame-suggest katika kitabu cha bajeti. Hili ni

eneo muhimu. Lakini upande mwingine, mkopo huu upelekwe pia kwenye kuboresha miundombinu ya barabara za kiuchumi; hili limo katika kitabu cha bajeti; miundombinu ya kiuchumi na nina imani kabisa kwamba barabara ya Mtwara- Tandahimba - Mewala – Masasi haitasahaaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umekwisha. Nichukue fursa hii kusema, naunga mkono hoja na nimalizie kwa kusema, *we have to live our dreams*. Ahsante sana. (*Makof!*)

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi kuzungumzia bajeti ya mwaka 2012/2013. Napenda moja kwa moja nimpongeze Dkt. Augustao Mgimwa - Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu Waziri Sada Salum na Janet Mbene. Napenda kusema kwamba naunga hoja mkono. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia mambo mawili. Kama kutakuwa na muda, nitazungumzia zaidi ya mawili. Kwanza kabisa ni juu ya deni la Taifa na pili, suala la mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la deni la Taifa limezungumzwa sana na napenda kwanza kabisa labda nizungumzle juu ya dhana nzima ya deni la Taifa. Kwa sababu wengi wamezungumza, wakasema deni la Taifa limekua kutoka Shilingi trillioni 17 mpaka Shilingi trillioni 20 ni kama vile jambo baya ambalo Serikali ya Tanzania imefanya. Kwanza kabisa, napenda kuzungumzia juu ya dhana nzima ya deni la Taifa. Sasa deni la Taifa ni kitu gani? Deni la Taifa ni mkopo wa nchi, sasa katika deni la Taifa unaweza kugawanya sehemu mbili. Kuna deni la nje na deni la ndani. Sasa suala zima nafikiri kwamba kukopa siyo jambo baya, lakini hapa tunapozungumza ni kama vile tunasema kwamba hapana jambo ambalo Serikali imefanya ni baya, imekopa. Nasema siyo jambo baya kwa sababu inategemea aina ya mkopo,

inategemea mkopo ule utatumika namna gani na pia inategemea matokeo ya ule mkopo. (*Makofi*)

Hapa tunapozungumzia Shilingi triliioni 17 kwenda Shilingi triliioni 20, inawekwa kama vile hizi Shilingi triliioni 20 zimekopwa jana au juzi au mwaka jana au mwaka juzi na kwamba zinapaswa kulipwa haraka. Lakini katika deni la nje, kuna utaratibu utaratibu wa kulipa kwamba, ni wakati gani fedha hizi au deni hili linalipwa. (*Makofi*)

Kwa mfano, mikopo mingi iliyokopwa ya Benki ya Dunia, nitakuja kueleza. *Africa Development Bank, Kuwait Fund* na kadhalika ni mikopo ya miaka kama 40 mpaka 50. Ni deni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na unapewa *grace period*, yaani muda ambao unaweza kujiardaa. Kwa hiyo, miaka kumi, *grace period*, kwa maana hiyo, kama ni mkopo wa maendeleo wa kuleta mabadiliko katika jamii, katika nchi, *definetly* katika muda huo wa miaka 40 unakuwa umesharudisha deni na mmepata faida zaidi katika *structure* za hapa mbalimbali. Kwa hiyo, nataka kuweka wazi kwamba tusije tukaelewa kwamba hili deni la Shilingi triliioni 20 limepatikana mwaka jana, 2011, mwaka juzi, 2010 na kwamba zinapaswa kulipwa haraka na kadhalika. Hasa hili nimeona kwamba niliweke wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia la pili, kama nilivyosema awali, ni kwamba kukopa ni jambo zuri na unapokopa, unakopeshwa pale ambapo unakopesheka. Kama hukopesheki hawezи mtu kukukopesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika mambo ya kawaida tu, binadamu, kama mtu anakuja kukukopa unamwangalia, unasema mh, huyu kwa kweli hatanilipa, humkopeshi. Mara nyingine hata mtu akija kukopa nyumbani unawaambia watoto mwambieni sipo, kwa sababu unajua

kwamba hawezi kukulipa. Watu wanasema kama unataka kugombana na rafiki, basi mkopeshe rafiki yule ambaye hawezi kulipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kusema na kusisitiza kwamba kukopa siyo jambo baya, linafanyika. Tukiangalia nchi, kwa mfano, nchi ya Marekani hii leo, tunasema ndiyo nchi tajiri kuliko zote. Nchi ya Marekani yenye *treasury bond* kutoka China. Huo ni mkopo ambao nchi ya Marekani imechukua. Hii leo, China ikiamua ku-*recall back* ile *treasury bond* yake, Marekani kiuchumi inaweza kuanguka na kutetereka. Ndugu zangu, hiyo ni Marekani, sembuse Tanzania! Sembuse Tanzania! (*Makof*)

Kwa hiyo, lazima tujue kwamba nchi kadhaa ambazo ndizo zinatoa msaada kwa Taifa letu, zinakopa na zimekopa na kama nilivyosema awali, ni jinsi gani ambavyo mikopo hii iweze kutumika? Kwa mfano, ukichukua pato la Taifa la mkopo kwa nchi mbalimbali, unakuta Canada asilimia 85, Uingereza asilimia 82.7, Marekani asilimia 102, Japani asilimia 229, Tanzania sisi ni asilimia 44.3. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kwenda haraka haraka, muda wenyewe ni mdogo sana. Kwa hiyo, Tanzania inakopa na inakopesheka. Kuna wakati mtakumbuka kwamba Tanzania ilikuwa haikopesheki, tulikuwa katika *HIPC, Highly Indebted Poor Countries*, lakini Tanzania hivi sasa inakopesheka. Niwaambie kwamba katika kukopa, kwa kweli kuna mambo kadhaa. Kwa mfano, kama ni *World Bank*, lazima Bodi ikae na iamue kama nchi inakopesheka au vipi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni *ADD*, lazima Bodi ikae na kusema nchi hii inakopesheka au vipi, lakini pia *watchdog*, yule ambaye anaangalia na kumwambia kama ni Marekani, kama ni *World Bank* kwamba hapana Tanzania haikopesheki, ni *IMF*, Shirika la Fedha la Ulimwengu la Dunia. Hili ndilo linasema kwamba nchi hii ipigiwe taa nyekundu, *stop*. Huwezi

kukopa! Nchi hii ipigiwe taa ya kijani, inaweza kukopa na nchi hii taa ya njano, inawezekana. Kwa Tanzania, ina taa ya kijani, kwa hiyo, inaweza kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ni kwamba fedha hizi za mkopo zinatumikaje? Huu tunaouzungumzia ni mkopo wa nje. Sote tunajua na kama nilivyoeleza, ni kwamba kwa miaka kadhaa, kwa mfano *Africa Development Bank* imetoa mikopo ya barabara kwa Tanzania. Mikopo hii ya barabara tunazungumzia tunataka barabara *Africa Development Bank*, kwa hiyo, Tanzania imebidi kukopa kwenye *Africa Development Bank*. *World Bank* imetoa mikopo ya kilimo kwa Tanzania, lakini pia kuna mikopo ya umeme, kuna mikopo ya mkongo wa Taifa, yote hii ni mikopo ambayo Tanzania imechukua ili kuweza kuendeleza na mikopo kama nilivyosema, yaani inaiva katika muda wa miaka 40 na *grace period* ya miaka kumi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kama hatutokopa, halafu mtakuja kuulizana kwa sababu kuna sehemu ya fedha kutokana na fuel levy ambayo inatumika kwa ajili ya barabara, lakini kuna sehemu ambayo inatolewa kwa ajili ya mkopo wa *ADB*. Kwa mfano, barabara hii ya *USA River* mpaka Namanga, *Arusha USA River*-Namanga, huu ni mkopo wa *Africa Development Bank*. Sasa kama tunasema tusikope, itamaanisha kwamba hatuwezi kuendelea, lakini kama nilivyoonyesha, kwa kweli nchi zote ulimwenguni zinakopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kuzungumzia juu ya mikopo.

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha*)

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti yetu hii ya mwaka 2012/2013. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uratibu na Mahusiano, kwa kuwasilisha bajeti zao vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiunga mkono hoja ya bajeti hii kutoka mwanzo lakini katika kuinga mkono napenda nitoe mapendekezo machache kwa nia ya kuiboresha bajeti yetu tuliyonayo. Baada ya kusikiliza majadiliano ya siku mbili na leo hii asubuhi juu ya bajeti hii, imeonekana dhahiri kwamba, matayarisho ya bajeti yanahitaji mchakato wa muda mrefu na mchakato ambao ni shirikishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu, hata kule ambako watu wamehoji, ni kutokana na kwamba, matayarisho ya awali hawakushirikishwa vizuri. Mimi nashauri kwamba, kwa siku zijazo turejee kule nyuma ambako tulikuwa tunakuwa na bajeti ya mwezi wa Februari ambapo Bunge lilikuwa linakaa kama Kamati ya Mipango. Tulikuwa tunashauri vipaumbele na wapi tuelekeze nguvu ya bajeti yetu. Hiyo ingepunguza sana majadiliano ambayo kwa sasa yanaendelea humu na baadhi ya watu kusema bajeti hii hawaiungi mkono; kumbe tungeanza kwa pamoja, mimi nina hakika tungeweza kwenda mbele kwa haraka zaldi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili ni kwamba, bajeti na hasa katika nchi zinazoendelea, lazima ilenge kupunguza umaskini. Inaweza kufanya hivyo kwa kuangalia shughuli za wananchi walio wengi katika maeneo hayo basi tuboreshe na tupeleke msukumo mkubwa, ili kusudi wananchi hao kwa yale wanayoyafanya kwa ajili ya maisha yao, kwa ajili ya uchumi, waweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania, wananchi wanaoishi vijiji zaidi ya 80% ni wakulima. Kwa hiyo,

nategemea kwamba, bajeti hii ingeweka msukumo mkubwa kwa upande wa kilimo, ili kusudi iondoe kero nyingi na kuweza kuwawezesha wananchi waweze kulima kwa tija zaidi. Bajeti iliyopo kwa sasa hivi ni shilingi bilioni 192.2, kusema kweli bajeti hii haitoshi, ilitakiwa iongezwe zaidi kukidhi mahitaji kwa mfano ya mbolea, ruzuku mbalimbali, ili kusudi wananchi wetu waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mipango mizuri kwa Serikali kwamba tutaanzisha benki na kwenye bajeti hii mmetamka, Benki ya Wakulima. Nashukuru kwamba kwa safari hii tayari kuna fedha kidogo zimetengwa, lakini hazitoshi. Tumezungumza kwa muda mrefu sana juu ya kuanzisha kiwanda cha mbolea kule Mtwara ili tusiagize mbolea kutoka nje, hili bado nalo halijafanyika. Viwanda vyta usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao yetu, nalo hili bado, viwanda vingi na wengine wamezungumzia korosho, wamezungumzia pamba, wamezungumzia vitu vingine, haya yote bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na *valid chain* kuanzia uzalishaji, usindikaji na hatimaye tutizame soko la mazao haya, ni muhimu tukawa na mipango mizuri ambayo itawasaidia wakulima wetu, tusiishie nusu. Napenda Serikali ijifunze kutoka Ethiopia ambapo wenzetu wana kitu wanachokiita *Commodity Exchange Market*, ambayo inakuwa kama mnada na kila mtu anakwenda pale, unakuwa *open* na watu wanandi pale kwa kutizama bei ya soko la dunia, halafu wanalinganisha na la kwao na ndio wanafanya mnada pale. Hii tulivoanza na stakabadhi ghalani ni nzuri, lakini sasa tuendelee mbele ili kusudi tuweze kufikia lengo hilo la soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bajeti inayowekwa nimesema kwamba, ni kidogo. Katika mapatano ya Maputo, tulikubaliana kwamba angalau bajeti ya kilimo iende kufikia 10% ya pato ghafi la Taifa, lakini mpaka sasa tuko kwenye 6% ambayo kwa kweli, si sehemu kubwa sana ya pato letu ambalo linawekwa kwenye kilimo ambacho kinaajiri watu

wengi na ndio huko ambako tungeweza kuwa na mapato mazuri zaidi. Lakini kwa kuzalisha zaidi, hasa chakula, hata huu mfumuko wa bei tunaouzungumzia ungeshuka moja kwa moja. Najua kumewekwa mkakati wa kulima katika mabonde kadhaa lakini vilevile ingeongeza ajira. Vijana wetu tunaosema kwamba, hawana ajira vilevile wangenufaika na haya. Kwa hiyo, nashauri kwamba, eneo la kilimo kwa kweli lipewe kipaumbele zaidi na hasa kilimo cha umwagiliaji ili kusudi pato la Taifa liweze kuongezeka zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna viwanda vingi. Kuna viwanda vya kusindika maziwa na wengi wamezungumzia leo juu ya viwanda vya kutengeneza nguo, mimi nafikiri viwanda hivi ni muhimu na hasa ili kupunguza ushindani wa bidhaa zinazoingizwa hapa nchini. Maziwa peke yake tunayoingiza hapa nchini kwa mwaka, ni Dola za Kimarekani takribani milioni 400, lakini tuna maziwa mengi hapa lakini kuanzisha kiwanda cha kusindika maziwa ni tatizo kubwa, viwanda vyetu vya kutengeneza nguo, vingi watu wamezungumza, vingepewa kipaumbele. Nina hakika tungeweza kuwa na msukumo mkubwa zaidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali, kwa kuweka mkakati wa kupunguza kodi ya ongezeko la thamani hadi kufikia kwenye 1% lakini hili limekuwa likisemwa, mpaka sasa halijafikia huko na tunategemea kwamba, katika hali ya kawaida hili litekelezwe ili kusudi wananchi waweze kunufaika zaidi katika maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 66 wa kitabu cha bajeti, aya ya tatu ya Kirumi, inaeleza maeneo ambayo yatapunguziwa kodi ya thamani. Napenda Serikali iangalie zaidi humu na hasa mashirika ya kutoka nje; mathalani ukichukua *USAID* peke yake ina sekta nyingi ambako ina miradi na sekta hizo nikichukua moja tu ya afya, ina mashirika madogomadogo 73. Punguzo la kodi la thamani kwa mwaka, linakwenda zaidi ya shilingi bilioni nne na kuna mashirika

madogomadogo 73. Sasa acha hilo ni shirika moja tu na lina miradi mingi, ukienda JAICA, ukienda NORAD, ukienda SIDA – Canada, SIDA – Sweden, ukienda DANIDA, yako mengi kwa hiyo, ni eneo ambalo ni lazima tulitizame na tuangalie tunanufaika namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la kodi ya *air time*. Napendekeza kwamba badala ya kusema kutanunuliwa sijui mtambo wa kuweza kufuatilia faida wanayopata wanaoendesa mashirika haya ya mawasiliano, tayari kulishakuja hapa pendelezo kwamba, makampuni yote haya yaandikishwe kwenye Dar-es-Salaam Stock Exchange, ndio utajua hasa kitu wanachokipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami napenda kuchukua fursa hii kuchangia bajeti ya hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa salamu za pole kwa familia ya Muasisi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Marehemu Bob Nyanga Makani. Mwenyezi Mungu, ailaze Mahali Pema Peponi Roho yake, Amina. Pili, napenda kutoa salamu hizi kwa Viongozi wa CHADEMA na wanachama na wapenzi popote pale walipo, kwa kufikwa na msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote ambao wamechaguliwa kwa kipindi hiki. Mwanzo mzuri, lakini mna changamoto kubwa katika Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuchangia ajenda ya vijana. Vijana katika nchi hii ni nguvu kazi ya Taifa lakini Serikali, ambapo kuna wenzetu walisema ima-

paralyse, wengine wakasema Serikali hii kama haipo, najiuliza ni kwa nini mpaka hatua hii tatizo la ajira kwa vijana bado ni kubwa wakati nchi yetu ina rasilimali za kutosha? Napenda kuchukua fursa hii kuiuliza Serikali, tatizo ni nini mpaka mnashindwa kutatua ajira kwa vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia bajeti ya Waziri Kivuli wa Kambi ya Upinzani, tunaambiwa changamoto ya ajira kwa vijana, bajeti mbadala imeiwekea mikakati mipana ya kiuchumi kwa kuanzisha miradi mikubwa ya umma itakayomeza vijana waliopo mitaani na kuanzisha kwa makusudi na kwa kasi vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya ufundi wa mafunzo mengine. Tatizo la ajira kwa vijana limekuwa ni tatizo sugu Tanzania. Serikali ituambie mwaka huu mmetenga pesa kwa ajili ya Benki ya Wanawake, hivi vijana wa Tanzania hamuwaoni kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka hapo kwa vijana, naomba nije sasa kuchangia katika suala zima la bajeti yetu kuwa tegemezi. Tukiangalia katika mwaka wa fedha 2012/2013, tunaona takribani trillioni 5.1 ni misaada na mikopo kutoka nje. Napenda leo kuiambia Serikali kwamba, waathirika wa kwanza wa bajeti kama hizi katika nchi yetu ni wanawake. Leo hii tunaona Sera za Marekani zinataka tupitishe mikataba ili tuhalalishe kitendo cha utoaji mimba, huu ni msiba kwa nchi yetu. Kuna Sera zinazochochea wanaume kuoana wao kwa wao; huu ni msiba kwa wanawake wa Tanzania, kama tutaendelea kuwa na bajeti tegemezi ni lazima kadiri siku zinavyoenda itafikia hatua tunakubali masharti ili tuendelee kuhudumiwa. Itafikia hatua nchi hii inapitisha Sheria hapa waoane wanaume kwa wanaume, wanawake soko lao litakuwa liko wapi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni waathirika wa kwanza wa bajeti hii na napenda wanawake wenzangu popote pale walipo...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize vizuri Mheshimiwa Sabreena kwa sababu anatoa hoja mahsus. Mheshimiwa Sabreena, endelea. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie; wanawake wa Tanzania ni waathirika wakubwa wa Sera za Uingereza, wa Sera za Cameron, zinazotaka tusaini baadhi ya mikataba kwamba, wanaume kwa wanaume waoane lakini waathirika wa mikataba hii ni wanawake, watakosa soko. Nani atawaoa? Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe bajeti zetu haziwi tegemezi kwa kiasi hicho. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia leo hii katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, 36% ya bajeti yake ya mwaka 2011/2012 ndio iliyotekelizwa, lakini bado tuna vyanzo vya mapato. Kwa nini nchi hii haiweki umuhimu katika maeneo haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie kwenye suala la miundombinu. Mkoa wa Kigoma tumekuwa nyuma kwa muda mrefu. Barabara zinasuasua na nimeshangaa kuna Wabunge wenzangu hapa wanasi mama mtu badala ya kuzungumzia kahawa, mananasi na ndizi ambazo zinalimwa kule Kalinzi ni jinsi gani zitaweza kutoka kule ziletwe Kahama, ziletwe Nzega na maeneo mengine illi kuuza kwa bei ya juu, tofauti na sasa hivi zinavyouzwa kule 2,000/=, 3,000/= kwa mkungu, watu haya wameyaacha, wanajibu Sera za Upinzani; huu ni msiba kwa Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiishie kwenye barabara, suala la ndege. Tukiangalia katika bajeti ya mwaka huu, kiwanja cha ndege Mkoa wa Kigoma kimetengewa shilingi bilioni 3.5 lakini tukiangalia Songwe, tunaona wana shilingi bilioni nane (8), tukiangalia kiwanja cha ndege cha Mwanza, kina shilingi bilioni nane (8); tukiangalia Mkoa Mpya wa Katavi, una shilingi bilioni tano (5), *what is so special?* Mkoa ambao

hata sidhani kama *Administration Block* imewekwa, unawekewa shilingi bilioni tano (5), Kigoma inawekewa shilingi bilioni 3.5 na bado mnatuambia kwamba Mkoa wa Kigoma ni *strategic Region*, ni Mkoa wa kimkakati, uko mpakani, una *connection* na nchi zaidi ya tatu, hili ni janga kwa Mkoa wetu wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya hapo, kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Arusha, wako *near* na kiwanja cha Kimataifa cha Kilimanjaro lakini leo hii na chenyewe kimetengewa shilingi bilioni 1.5; hii ni *under utilisation* ya kiwanja cha ndege cha *KIA*. Napenda kuiomba Serikali inapokuwa inapanga bajeti zake ama inapogawanya keki ya Taifa, ni lazima waangalie ni Mikoa ipi iliachwa nyuma na huu ni wakati wa kui-*consider*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa haraka haraka niende kwenye sekta ya madini. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda nikushauri kwamba, kuna taasisi kibao zina hela za kutosha, lakini ninyi masikio yenu na akili mmeelekeza kwenye Bodaboda na pombe. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nchi hii haiwezi kuendeshwa na fedha za pombe. Mnaitafutia nchi balaa hii, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, leo hii Manispaa ya Mtwara, haipewi *service levy* ya gesi. Leo hii Halmshauri ya Bagamoyo ilikuwa inauza kokoto zake, madini ya ujenzi kwa wakandarasi takribani 5,000,000 kila mwaka; katoka Mkuu wa Mkoa, kaenda kasitisha zoezi hili, leo Halmashauri hii haipati mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 69 wa kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Fedha, tunaambiwa kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinahimizwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuzingatia fursa zilizopo. Mionganoni mwa fursa zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ni pamoja na uwepo wa madini ya ujenzi, ambayo ni kokoto. Serikali hili hamulioni?

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiishie hapo, twende Mkoa wa Kigoma, eneo la Mgambazi. Kule kuna madini, kuna *copper*, kuna *platinum*, madini haya yamekuwa yakichimbwa zaidi ya miaka 30. Wanayabeba wanayapeleka *South Africa*, tunaambiwa ni utafiti, ripoti ziko wapi? Hatuoni. Huu ni wizi wa kweupe kweupe, Mkoa na Halmashauri ya Wilaya, ingeweza kupata fedha nyingi lakini hakuna kitu ambacho kinalipwa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hii ni sekta ambayo inapoteza pato la Taifa. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia... (*Makofi*)

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia bajeti ya Serikali. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na Wataalamu wake wote na Manaibu wake, kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala limeongelewa, suala la ajira kwa vijana. Hii ni changamoto ya dunia nzima. Suala la ajira kwa vijana ni changamoto ya dunia nzima, lakini sisi kama Wabunge ni wajibu wetu sasa kuishauri Serikali na sio kuwa walalamikaji na wapiga kelele, tuishauri Serikali. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Sawasawa !

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Tuishauri Serikali tufanye nini ili tuweze kusaidia vijana wetu wote. Wale vijana siyo vijana wa Serikali peke yao ni vijana wetu wote, sisi ndiyo wazazi, tushauri Serikali yetu tufanye nini kuboresha huduma kwa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna fununu tumesikia kwamba kesho kuna watu wanajipanga kuikataa hii bajeti lakini mimi nasema kesho kutwa bajeti hii itapita kwa sababu bajeti hii imekidhi mahitaji yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye kuchangia bajeti, naishukuru sana Hazina kwa kutupa bajeti katika Manispaa yetu ya Tabora ya shilingi bilioni 25. Bajeti hii imegawanyika mapato ya ndani ni shilingi bilioni tatu pointi tano, matumizi shilingi bilioni tatu pointi moja sawa na asilimia 13, mishahara shilingi bilioni 14 sawa na asilimia 54. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo ni ndogo sana, tuna asilimia 20 tu, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie sana kuhusu bajeti hizi za maendeleo, mwaka uliopita kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa fedha hizi za maendeleo na fedha hizi za miradi na kuna sehemu nyingine kama sisi Tabora Manispaa hatukupata fedha zote za maendeleo, tulipata asilimia 67 ya fedha zote za bajeti kati ya shilingi bilioni 22 tukapata shilingi bilioni 15 tu. Tunaiomba sasa Serikali kwa kutaka kuiboresha bajeti hii iwe nzuri ihakikishe kwamba fedha zote zilizoandikwa kwenye bajeti zimefika kwa walengwa, zimefika ndani ya Halmashauri kwa wakati mufaka. Hii itatusaidia sana kupeleka maendeleo yetu mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011, sisi Tabora Manispaa tulipangiwa shilingi bilioni 5.8 lakini tulipata shilingi bilioni tatu tu na hii inatufanya kutokuwa waaminifu kwa wananchi kwa sababu tunakwenda kule tunaahidi miradi ya bilioni 5.8. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nchi yetu imeendelea, mitandao ya kijamii imekuwa mingi, watu wanazisoma hizi bajeti kwenye mitandao, lazima wanapoona bajeti ya shilingi bilioni tano ya maendeleo, lakini maendeleo hayafiki, matokeo yake inaonekana kwamba Halmashauri imechakachua fedha hizi, lakini fedha hizi hazikufika kwa wakati, hazikufika kwa

asilimia mia moja. Kwa hiyo nimwombe sana Waziri wa Fedha sasa hivi kwa kweli tunaomba fedha hizi zifike kwa wakati na zifike kwa asilimia mia moja. Hili pia ni tatizo kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna bajeti zinawekwa za wafadhili labda na Hazina, kwa mfano kwetu Tabora Manispaa tulikuwa na bajeti ya elimu *MMES*, bajeti hii ilikuwa ya shilingi bilioni moja pointi moja hatukuipata kabisa na tulikuwa tumeshaitangaza kwa hiyo inaonekana sisi siyo wa kweli, tunaomba sana hivi vitu viwe vya uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tulikuwa na bajeti ya *capital development grants* ya shilingi milioni 829 tulipata shilingi milioni 400 tu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunaomba safari hii ujitalahidi, bajeti yako ni nzuri uitekeleze mpaka mwisho kwa kufuata taratibu zilizopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee habari ya Tabora. Tabora kwa kweli ni Wilaya kubwa sana, napendekeza ziundwe Halmashauri mbili, sijipingii debe ya kupata Jimbo, lakini napendekeza ziundwe Halmashauri mbili. Nasema hivi kwa nini? Mjini tuna Kata kumi na tatu, vijijini tuna Kata kumi na mbili. Kata kumi na mbili za vijijini zina wakazi zaidi 50,000, Wilaya ya Pangani ina wakazi 48,000, fedha za maendeleo Tabora Manispaa tunapata shillingi milioni 100. Fedha za kilimo tunapata shilingi milioni 100, Pangani kwenye wakazi 48,000, wanapata fedha za kilimo shilingi milioni 500 au zaidi. Kwa kweli mnatuonea, kwa kweli mnakwamisha maendeleo yetu, yamekwama siku zote lakini Serikali mnachangia kutukwamisha. Tunaomba mtugawie hizi Halmashauri ziwe; Halmashauri ya Vijijini na Halmashauri ya Mjini ili kazi ifanyike kwa ufasaha. Hata Mbunge wa Jimbo aliyeleo anapata shida sana kuitembelea Wilaya yote kila siku atakuwa analaumiwa tu. Kwa hiyo, naomba sanasana mtusaidie hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata maji sisi tunapata maji ya TUWASA, TUWASA imekosa nguvu, Wilaya ni kubwa sana, Kata ni nyingi mno, sasa hivi kuna Kata ya Itetemia, Kata ya Talikwa, Kata chungu nzima hazina maji kabisa, wakienda Halmashauri, Halmashauri hakuna pesa, wakienda TUWASA, TUWASA hakuna pesa, wamehanganya kwa muda mrefu sana. Tunaomba tupate mradi wa maji vijijini, kuwe na mradi wa maji vijijini kama ulivyo kwenye Halmashauri za vijijini na sisi Tabora tunataka kwa sababu tuna vijiji vingi. Kwa kweli huu mtizamo wa Wilaya moja ina sura mbili, ni mtizamo mgumu sana, mimi naomba Serikali uufanyie kazi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze *World Bank*, *World Bank* imetuahidi kutupatia shilingi bilioni 23 kwa ajili ya miradi ya soko, barabara za lami kilometra 15 pamoja na madarasa pamoja na *bus terminal*. Kwa kweli yote hii ni jitihada nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, napongeza sana na naipongeza sana Serikali yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sisi watu wa Tabora tuko nyuma, tukipata *bus terminal* ya kisasa, tukapata barabara za lami za mjini, siongelei ambazo ziliahidhiwa na Mheshimiwa Rais, tunaongelea za katikati za Manispaa, tunaongelea soko la kisasa, kwa kweli Serikali yetu itakuwa imetukomboa sana na kuhakikisha tunaendelea kushika dola pale Tabora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee haraka haraka kuhudu *TRA*. Pale Tabora kwa kweli wanatuchonganisha sana na wananchi, nimeangalia bajeti ya Serikali kipindi kilichopita madereva wetu wa bodaboda na pipipiki wamelipishwa shilingi 291,000 kwa mwaka kodi ya mapato, tukalalamika, tukaenda kwa Mkuu wa Mkoa ikashindikana, tunaishukuru sana Serikali nikaenda kwa Naibu Waziri akapiga simu tukashushiwa bei wakawekewa shilingi 90,000 kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huwezi kuamini baada ya miezi kadhaa, meneja wa *TRA* alirudisha kiwango cha shili 291,000 kwa madereva wa bodaboda na pikipiki. Kwa kweli hiki kitu kinatuchonganisha sana Serikali na wananchi hasa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nauliza, hawa Mameneja wa *TRA* wanakaguliwa na nani? Hivi meneja wa *TRA* amekuwa Mungu mtu hivi, vitu si viko kisheria? Kama kwenye sheria imeandikwa 90, lakini meneja wa *TRA* anasema 291,000 na hawa watu lazima walipe vinginevyo atawapa *notes* atawakamata, atawa-*harass*, kwa nini sasa isifike Mkurugenzi wa *TRA*, Ndugu Kitilya sijui wakaunda timu ndogo ikapita Mikoani ikaangalia kama kodi wanazotoza zinastahili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Meneja wa *TRA* mfanyakazi mkubwa ambaye hamtaki, kila siku anamjazia *arrears*, kuna wafanyabiashara kule *arrears* kila siku, wamelipa kodi vizuri lakini unaongezewa *arrears* na kuna mwingine halipi kodi vizuri na hana tatizo lolote kwa sababu tu yeye ni meneja wa *TRA*, hii siyo na hii inatugombanisha na Watanzania. Mimi naomba kabisa sasa hivi imefikia wakati tufute kabisa kodi za pikipiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kingine, hivi unatoka wapi uhalisia wa dereva tax wa Dar es Salaam aliye shilingi 90,000 kwa mwaka dereva taxi wa Tabora, Mkoa maskini aliye shilingi 291,000 hivi hii ni haki? Madereva wangu wa taxi wa Tabora wanalipa shilingi 291,000, tumelalamika Bunge liliopita, nimewachukua viongozi wote nikaja nao kwa Waziri wa Fedha hapa, mara ya pili hiyo, mara kwanza walishushiwa baadaye wakapandisha, mara ya pili akawaandikia barua, hivi hii ni haki? Mimi naomba meneja wa *TRA*, wamepangiwa kifungu...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda!

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Naunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Munde. Kama nilivyosema sasa ni zamu ya Mheshimiwa Selemani Nchambi atafuatiwa na Dkt. Mfutakamba.

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaomba nikimbie sana katika maeneo ya Jimbo langu, kwa sababu Jimbo langu ndiyo Jimbo linaloongoza kwa ubadhirifu na miradi mibovu na shughuli za maendeleo ziko duni. Kwa hiyo, nikiishiwa na muda nisichangie kuhusu uwezekano wa namna gani tutaongeza kipato katika bajeti hii usinilaumu wacha kwanza nianze na wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika mambo haya yote tuwekane sawa, maji ya ziwa Victoria tuhakikishe kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi mwaka jana ungeanza, mwaka huu uanze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, visima virefu vichembwe kwenye maeneo ambayo maji hayo hayatafika. Akinamama wa Kishapu wanahitaji kupendeza nywele zao kama alivyo Sara Msafiri hapa lakini hawawezi, wanabeba maji kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama wa Kishapu wanachoka hata jioni migongo, viuno, vinauma kwa kubeba maji umbali mrefu. Kwa hiyo, naomba sana maji ya Ziwa Victoria, Waziri wa Fedha yuko hapa, ndiye anayemsaidia Rais kwenye mambo haya, ahakikishe fedha zinatengwa na tayari tumeshakamilisha michoro. Mabwawa, marambo, *scheme* za umwagiliaji hatuna hata asilimia moja, tutazalisha vipi, tutaongeza vipi kipato wakati watu hawazalishi ? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali ya Wilaya, nimeingia katika Jimbo la Kishapu hakuna hospitali ya Wilaya, akina mama hawa wanapata taabu, wakitaka kujifungua kwa operesheni vituo vya afya tunavyo vinne, havikidhi wala havitoshelezi mahitaji. Wanapotaka kujifungua wanakwenda kilomita 125 kutoka Magarata kwenda Shinyanga mjini, hii siyo haki na mimi sikubaliani na hili. Kwa hiyo, iangaliwe uwezekano, tumeleta *special request* zaidi ya mara tatu inarudi, je, umuhimu wa afya za wananchi wa Kishapu haupo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia bajeti nzima ya afya, sisi Kishapu tunahitaji zaidi ya shilingi bilioni 6.5 tuna zahanati 47 zinazokidhi kiwango, 17 katika zahanati 117 za vijiji vyangu. Vituo vya afya tunahitaji 20 tunavyo vinne, lakini kimoja ndiyo *at least* kinaweza kikaitwa kituo cha afya. Mgao wa dawa wa kituo cha afya tunaoupata kwa Jimbo la Kishapu ni 348,281, hizi dawa zingine wananchi wanapata wapi? Pamba yenyewe itauzwa shilingi 460, dawa wajinunulie, *ambulance* hakuna *network* haipatikana, *ambulance* ziko tatu, wauze ng'ombe wakodishe gari la wagonjwa kukimbia Shinyanga Mjini, mimi sikubaliani na mambo haya, naomba kwa kweli marekebisho yafanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu Kishapu hatuna mochwari, mtu anapofariki anawekwa *store* kama mchele ama pamba, mimi sikubaliani na haya, ninaomba *special request* iliyokuja ya hospitali yetu ikamilike. Sikubaliani na akinamama kupata taabu, wazee wangu kupata taabu wakiugua na viongozi wakuu wa Kiserikali wanapokuja Kishapu wakiugua wasipelekwe India kama Shemeji yangu Zitto, watibiwe palepale kwenye zahanati zetu za Kishapu waonje machungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha *production* ya nchi hii, barabara ya lami ya kutoka Kolandoto kwenda Meatu, naomba iingie kwenye mpango na ipatiwe fedha. Tunalima sana, tuna mifugo mingi, tuna mambo mengi sana, naomba

sana barabara ya lami hiyo iingie kwenye mpango, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine katika miji yangu mitatu ya Ukenyenge, Maganzo na Muhuze, hatuna hata kipande cha lami au kwa sababu sisi ni Wasukuma hatutakiwi kuwa na lami katika miji yetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji daraja la Karitu, Manonga, tunahitaji daraja Kiloleli kwenda Idisa, tunahitaji daraja la kwenda Shinyanga Itirima, kunakolimwa mpunga, Itirima tunalima mpunga mwangi sana lakini usafirishaji ni wa bodaboda, gunia linabebwa kwa bodaboda, naomba sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye elimu, fedha zangu zimefanyiwa ubadhirifu, kwenye elimu mimi wanafunzi wanakaa chini, Walimu nyumba hakuna, tunakwenda kwenye madarasa hayatoshelezi, fedha za MMEM zimeliwa, tunakwenda kwenye maabara zimeliwa, hostel wanafunzi wangu hawana watoto wa kike wanapanga kwenye nyumba vijijini, mimba zimeongezeka. Kishapu nataka nikueleze watoto wa kike baadaye kama akinamama Anna Kilango hapa hatutakuja kupata watetezi kama utaratibu ni huu, lazima fedha ije. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu siyo wa kutosha, chakula shulenii, tumeanza na shule 20 katika shule 126 na watoto hawa wanatembea kilomita nyingi, naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye kilimo pamba...

(*Hapa Mheshimiwa Mbunge aliongea Kisukuma*)

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Nimewaambia kwa lugha ya nyumbani kabisa kama hakuna elfu pamba wakae nayo kwanza. Watu wamehangwaika, wamepigwa juu,

wamekwenda kwenye tope, wamevuna, wamepiga dawa, dawa zimechakachuliwa wamepewa maji lakini bado bei tunaambiwa shilingi mia tano.

(Hapa Mheshimiwa Mbunge aliongea Kisukuma)

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, pamba inaendelea kushuka kila mwaka, leo Geita, *mining turnover* ya mwaka mmoja ni zaidi ya shilingi bilioni 400 mafuta unayotumia kwa mwezi mmoja ni lita milioni moja na nusu, milioni mbili lakini bajeti ya afya, ni shilingi milioni 576 *turnover* ya mgodi mmoja, inasogelea bajeti ya Wizara moja, mimi sikubaliani na hili. Shinyanga sisi, naomba nianze kukuhesabia neema tulizonazo, tuna pamba nyingi, tuna dhahabu nyingi, almasi nyingi, tuna mifugo mingi, tuna tumbaku nyingi, tuna *population* kubwa kabla ya kugawa Simuyi, *4.2 million people* Mkoa wa Shinyanga. Tuna vyanzo vingi via maji na tuna mpunga mwangi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nianze kukuhesabia matatizo ya Mkoa wa Shinyanga, kiwanja cha ndege mvua ikinyesha ndege hazishuki, Mheshimiwa Rais zaidi ya mara mbili anataka kushuka kiwanja kimejaa maji, hospitali ya rufaa hatuna, watu milioni 4,200,000, kwa neema zote hizi, hatuna chuo kikuu chochote, kwa neema zote hizi maji ya Ziwa Victoria tunashukuru sana Serikali ya CCM imeyaleta, lakini Kishapu lazima yafike kwa neema hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nakwenda kwenye matatizo tu, tuna vyanzo via maji lakini maji ni haba, akinamama nimelieleza sana, neema ya pamba, Shinyanga inatoa pamba 62% ya pamba ya nchi hii, huo ni Mkoa mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna kiwanda chochote, leo nashangaa mashirika yetu ya Serikali ya NSSF wanajenga maghorofa ya shilingi bilioni 100 Dar es Salaam, yamewaaajiri

Watanzania 30, wanashindwa ku-*invest* kwenye viwanda vya nyuzi na nguo ambako wataajiri Watanzania milioni 14, pamba inaajiri Watanzania milioni 14 wakulima wa pamba wakiamua Serikali gani ikae madarakani inakuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima sasa Serikali ifanye yafuatayo kwenye pamba isiwe ni agenda za kuongea. Bodi ya pamba imeonekana imeshindwa kusimamia pamba, pamba tumeanza kulima kabla ya uhuru, ivunjwe, iundwe bodi mpya. Uingereza kabla ya kuanzishwa bodi, wajumbe wanakwenda kusomea namna ya kuendesha bodi, sisi hawasomei, imekuwa kama ni takrima, wewe utakuwa Mkurugenzi wa Bodi, haiwezekani awaburuze watu milioni 14, kikao kinakaa kwa ajili tu ya kupanga bei ya pamba, hakikai kwa ajili ya mikakati ya kuimarisha zao la pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifute kodi zote kwenye zao la pamba, Serikali itoe dhamana kwa matajiri wawekezaji, Watanzania wanaotaka kuwekeza kwenye mazao ya pamba, itoe *guarantee* kwa viwanja hivyo. Serikali gani isiyosikia Watanzania milioni 14 wanalia, sasa wamefika 16, NSSF wanajenga maghorofa yanapangisha watu 40, 50 badala ya kwenda ku-*invest* kwenye ajira ambako wataajiriwa Watanzania milioni 16, fedha za nje zitakuja madola kwa madola tutaacha hata kwenda kukopa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nataka niwatahadharishe na kuwaomba, kama tunawadharau Watanzania milioni 16 wanaolima pamba tutakuja kukumbuka maneno yangu. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M.N. SULEIMAN: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini sisi Wabunge *form one*, uwe unatuongezea muda. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na pole sana kwa matatizo ya Kishapu, lakini kwa kweli Serikali imekuwa ikipeleka hela kama mtakavyokumbuka Waheshimiwa Wabunge Taarifa ya CAG, tunatumaini Serikali itafuatilia kuona nini kinachoendelea huko Kishapu.

Mheshimiwa anayefuata ni Dkt. Athuman Mfutakamba na baada yake Mheshimiwa Salome Mwambu ajiandae. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Athuman Rashid Mfutakamba.

MHE. DKT. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Nami pia naomba nimpongeza Mheshiiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Manaibu Waziri wawili kwa bajeti ambayo wameweza kuiwasilisha na kuifanya kazi vizuri sana. Nianze tu kwa kutamka kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 300. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwanza kuweza kutuletea barabara ya lami kwenye Jimbo la Igalula, kitu ambacho tangu Jimbo lile liundwe ilikuwa ni barabara ya vumbi lakini hivi sasa tuna kilomita 86 zinawekwa lami kutoka Tabora Mjini mpaka Nyahua, kuna kilomita 82 zinatoka Itigi kuja Chaya. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba kilomita 88 zilizobaki tunaomba nazo ziwekwe lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee pale alipoishia Mheshimiwa Zakia Meghji. Nimekuwa nafuatilia mijadala kwa makini sana kuhusu suala la deni, deni la taifa la ndani na nje, ninaomba nieleze suala la mzigo wa deni yaani *debt burden*. Kitaalamu unaweza kupata uwiano yaani *debt ratio* kwenye *GDP* yaani pato la Taifa. Sasa kwa harakaharaka hapa ninazo

nchi na kiasi cha *ratio* ilivyo. Wenzetu Kenya *GDP ratio* ni 50.9, Uganda 20.4, Afrika Kusini 33, Malaysia 53, Indonesia 1002. Tuangalie sasa wenzetu wa *G8 club*, Japan kama alivyosema Mheshimiwa Meghji 225%, UK 76.5%, Marekani 58.9%. Suala la msingi kama walivyoeleza wajumbe wengine walionitangulia ni fedha hizi tulizokopa tunazitumiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatumia kwa kujenga barabara, tunatumia kwa ajili ya afya na maji, kwa hiyo ni lazima tukope, lakini suala ni *ku-manage* lile deni ili maendeleo yawafikie wananchi na Serikali ya CCM hilo inalifanya kwa hatua kubwa sana. Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge ndiyo inachukua *oversight function* ya kuangalia hizi fedha zinatumikaje. Kwa hiyo, Kamati naamini inafanya kazi nzuri hili lisiwe tatizo kwa ndugu zangu wenye wasiwasi wa ukubwa wa deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya Madiwani ni muhimu kwani Madiwani ndiyo wanatuwakilisha kule na Madiwani ndiyo wako karibu na wananchi. Wilaya ya Uyui kiasi tulichopata mwaka jana kilikuwa hakitoshi kama kilichokuwa *budgeted* kwa hiyo tunaomba kiongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la maji, nina vijiji 51 lakini vijiji vitatu tu ndiyo vina maji na wananchi wa Jimbo la Igalula wanahitaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru suala la mtandao tunaendelea vizuri, lakini bado vijiji kama nane havijapata mtandao. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amesema hayo yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama wa chakula pamoja na mfumuko wa bei, ghamama ya umeme na ghamama ya chakula, mimi nashauri kwamba tuendelee kuongeza bajeti kwenye pembejeo na tusimamie hili kikamilifu ili tukiwa na uwezo wa kuzalisha chakula ndani, mfumuko wa

bei utashuka na bahati nzuri kwa sababu sekta ya madini inakwenda vizuri, naamini kama tutaongeza kodi ya mirahaba isiwe 4% ya *gross*, tuongeze tano au sita kwa sababu gharama za utafutaji yaani *exploration cost* hii nchi yetu karibu kila mahali kuna madini kwa hiyo ule uhatari yaani *risk factor* iko chini. Kwa hiyo, tuzungumze nao, kuwe na *windfall tax*, mtu amepata madini mengi tunam-charge mrahaba mkubwa zaidi, hili nafikiri linawezekana Wizara husika kama zitafuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, 30% ya matumizi ya fedha za maendeleo, kuna pesa nyingine zipo kwenye elimu, kuna pesa nyingine zipo kwenye Tume ya Katiba na kuna pesa nyingine zipo kwenye Sensa, hizi zote tunaomba Waziri wa Fedha azikokotoe kwa sababu ni sehemu ya mpango wa maendeleo. Mimi naamini itafika 40% tu kama tunavyohitaji ili bajeti iweze kupita kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya bodaboda, mimi nashukuru kuondoa hii kodi kwa sababu vijana wangu wengi watapata unafuu na wataweza kupata pato lao na mahitaji yao kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba sasa Igulula na sisi tutapata umeme kama ilivyokuwa imepangwa kwa bajeti hii. Kwa hiyo, mimi nashukuru sana bajeti hii Igulula tutaonekana, Sololo, Goeko, Kigwa pamoja na Imalakasekwa watapata umeme sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la tabianchi. Tabianchi tunaweza kupata fedha za ziada kutoka kwenye mifuko mbalimbali inayoshughulikia masuala ya hewa ukaa. Mimi ninaomba sana, nimeona kwenye Mpango na nimeona pia kwenye bajeti tumezungumzia uhifadhi wa mazingira na tabianchi lakini misitu yetu ya kupanda na misitu ya asili vijiji vyote vinavyotunza hii misitu upo utaratibu, kuna dirisha moja lipo Marekani kwa sababu wao siyo *Kyoto signatories* lakini nchi

nyingine za Ulaya na Asia wanachafua mazingira wanaweza kutulipa kwa sisi kuhifadhi maeneo yetu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa mawasiliano. Kodi yetu ipo chini kwenye kampuni za mawasiliano, Kenya wanapata shilingi bilioni 107 *corporate tax*, Uganda wanapata shilingi billioni 45, Rwanda shilingi bilioni 21 lakini sisi tunapata shilingi billioni 2.5. Naamini mtambo huu ukija na tukiweza ku-*monitor* hizi kampuni zetu zilikuwa zinapata ngapi, tufanye kupiga hesabu kwenda nyuma tangu walipoanza kupata hizi fedha ambazo hawakutulipa yaani *retrospectively* ili tuweze kulipwa fedha hizo na ziweze kwenda vijijini kwenye masuala ya barabara, maji na umeme, itakuwa ni muhimu sana kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la mwisho lakini siyo kwa umuhimu ni kuhusu bandari. Nimeangalia katika vitabu vyote vya Mpango sioni gati 13 na 14 linaelezwaje. Hili ni lango la kufungua uchumi kwa sababu nimeona Gati Na.1-7, Bandari ya Dar es Salaam, sasa utakwenda kina toka mita tisa mpaka kumi na tatu kama hauongezi kina cha lango utapitishaje meli kubwa za *generation* ya nne yaani *fourth generation shipped?* Ni muhimu Mpango uwepo wa kujenga gati namba 13 na 14 haraka iwezekanavyo kwa sababu huyu ni ng'ombe yuko tayari kukamuliwa, tayari ujauzito ameshapata, tutapata fedha nyingi na tutaweza kujenga bandari nyingine kwa haraka zaidi kwa utaratibu ambao *TPA* pamoja na Bodi yake wataona ni sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye teknohama. Zipo nchi kwa mfano Dominican Republic Jamaica, wana utaratibu wa kampuni hizi na ku-*process* masuala mengi kwenye *IT* na kadhalika, tutapata ajira nyingi kama tuki -link na sehemu moja inaitwa Silicon Valley ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja tena asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Athuman Rashid Mfutakamba...

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN M. CHEYO: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Cheyo!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7). Mheshimiwa Mjumbe aliyemaliza kuzungumza, amezungumzia sana juu ya madeni yaliyokopwa yamekwenda wapi na Mheshimiwa Meghji pia amesema hayohayo lakini kitu kinachoshangaza ni kwamba miradi haiendi yaani haina fedha na sisi tunavyoangalia *accounts* za *vote* mbalimbali ndiyo hilo tunaloliona, isingekuwa basi vizuri Waziri wa Fedha kati ya miaka mitatu ambapo deni la taifa lilikuwa trillion tano *point something* na leo ni ishirini *point something*, basi atuletee ndani ya Bunge hili *matching* ikonyesha kwamba fedha hizi zilikopwa na zilikwenda huko na fedha hii ilikopwa imekwenda mradi huu. Basi ubishi huu utakuwa haupo tena, lakini kama hakuna hali kama hiyo ni vigumu sana kukubali hata yale yaliyosemwa na Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza na wale watu wengine wote ambao tunasema kwamba tunapeleka kwa mambo mengine, naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cheyo, kwa kweli hapo hakuna mwongozo ultaka kuchangia tu kuhusiana na walichokuwa wanasema akina Mheshimiwa Meghji na

Mheshimiwa Mfutakamba na kwa hiyo na mimi nisingependa kuingia hapo katikati ya mjadala huo.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Salome Mwambu na atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvestry Koka.

Mheshimiwa Salome Mwambu!

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niongee kuhusu mambo machache kwani mengi wamezungumza Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda nichangie kuhusu fedha za maendeleo. Fedha za maendeleo, nafikiri tukae sasa Wabunge na Wizara ya Fedha tufikirie namna ya ya kupata hizi fedha kuliko kuwategemea wafadhili. Wafadhli wanachangia 70% ambayo haifiki halafu Serikali inachangia 30%, tujifunze nchi nyingine walifanyaaje? Walikuwa hawana wafadhili kama China na Korea? Walikuja kuinukaje kwenye maendeleo? Sasa sisi ifike mahali wafadhili tusiwategemee bali tutafute mbinu katika uchumi wetu wa ndani ili tuone tutaongezaje hii bajeti. Mathalani, mimi nashauri fedha wanazotoa wafadhili tumeona haziji sasa kwa nini bajeti isitengenezwe msamaha wa kodi urudishwe kwa mashirika mbalimbali yanayosamehewa? Zile fedha hata kama watalipa nusu lakini ziongezee huu mfuko wa maendeleo. Ni fedheha kwenye Halmashauri, mnakaa mnapanga bajeti lakini mnakuta hizo fedha zinaweza zikaja shilingi milioni 20 au zisije kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tuliangalie kwani wanateseka sana Madiwani wetu kujibu hoja za miradi mbalimbali za wananchi, kwa nini miradi haiendi? *Solution* ya kwanza ni kuanza na kodi walizosamehewa. Kweli wapo wanaosamehewa wanaofanya huduma za jamii lakini zile huduma za jamii nazo kuwafikia wananchi ni shida. Unaweza

ukakuta kuna vituo, hata hizi dawa za kuongeza maisha kwa waathirika hakuna au hazifiki na mtu kasamehewa aingize bure. Suala hili tuliangalie kwani ni dogo lakini linawaathiri sana wananchi na linatuathiri hata sisi tunaowaongoza wananchi kwa sababu kilio ni hichohicho, watu wamejitokeza kwenda kupimwa mume na mke, wajawazito lakini hakuna madawa ya kupimia. Kwa hiyo, mimi naona jamani tupunguze hii misamaha, waangaliwe kweli watu wanaohitaji kupewa msamaha, wengine walipe kodi ili tuongezee kwenye mfuko wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee suala la viwanda. Duniani kote uende China na kadhalika, viwanda ndivyo vilikuwa *source* ya maendeleo hasa viwanda vyatya nguo yaani *textile industries*. Sasa sisi mbona tunapuuzia hizi *textile* au viwanda vyatya nguo, hatuvijalijali? Viwanda vyatya nguo ndivyo vilivyoleta mapinduzi ya kilimo maana yake na sisi wale wenye uwezo wakisamehewa VAT watasaidia sana kuinua kilimo cha mazao mbalimbali hasa pamba, watasaidia na hakutakuwa tena na watu kuacha kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wangu wa Singida ni mmojawapo unaolima pamba lakini watu walishaweka zana chini kwa sababu pamba haina soko wala haina bei na mnajua kazi ya pamba ni nzito mno mpaka mtu kuvuna kupeleka kwenye soko. Kwa hiyo, mimi ninachoomba ni kwamba watu wapewe motisha, wasamehewe kodi na wenye uwezo wajenge hivyo viwanda vyatya nguo, nguo utaivaa leo kesho imeisha unakwenda kununua tena, ina ajira. Kwa hiyo, ninachoomba hawa watu wenye uwezo wa kuanzisha au kujenga viwanda vyatya nguo watazamwe kwani wanaleta ajira kubwa mno hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine napenda nizungumzie kuhusu umeme. Jamani umeme kila mahali kulingana na teknolojia sasa hivi, umeme ndiyo unaosukuma maendeleo mbele. Sasa mimi kwenye Wilaya yangu ya

Mkarama nina mafuta yako juu ya ardhi, mafuta siyo lazima yawe chini, mafuta ya kula. Wananchi wanalima alizeti na walanguzi wanunua kwa bei mbaya, wanaauza kwa sababu ya shida lakini umeme ungepelekwa, kungekuwa na viwanda vingi vidogovidogo vya kukamua alizeti. Tungeuza nje mafuta ya alizeti na tungedhibiti uingizaji wa mafuta ya kula hapa nchini, kwa hiyo, mkulima angepata motisha na angelima zaidi hili zao la alizeti pamoja na zao la pamba. Ninachoomba umeme uangaliwe jamani siyo suala la mjadala ndiyo kipaumbele cha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, hii bajeti naomba ipitie sana mawasiliano, tumezoea hapa Tanzania tangu uhuru njia za mawasiliano zinazojulikana ni Dar es Salaam – Mwanza na Reli ya Kati na Arusha lakini njia zinaweza zikapasuliwa za kukatisha huu msururu wa magari, magari mengine yakapita labda Dar es Salaam kuitia Mkarama kuelekea Mwanza lakini daraja la Sigit, imekuwa ni wimbo. Hili daraja tunalitaja na kwenye bajeti limetajwa lakini utekelezaji hauonekani. Mimi naomba hilo daraja lipitishwe maana yake litafungua Meatu, Wilaya ya Mkarama mpaka Nairobi. Sasa ubaya uko wapi mpaka mtu azunguke Mwanza aje akate Singida aelekee Arusha, naona masuala mengine yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nitoe shukrani kwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Tunajua kuwa huu ni mwanzo tu lakini kule tunakokwenda watatufikisha. Vilevile nashukuru kupata uongozi katika Wilaya ya Mkarama, nina *DC* na nina watendaji karibu wote wa Halmashauri, ninangoja nipewe kibali tarehe I Julai, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Sylvestry F. Koka, atafuatiwa na Mheshimiwa Rebecca Mngodo. Mheshimiwa Koka!

MHE. SYLVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Yote tunayozungumza hapa kimsingi Watanzania wanataka maendeleo na maendeleo ni mchakato ambao hauna mwisho. Lengo la bajeti hii, ni kujaribu kukidhi na kufanya mchakato wa rasilimali mbalimbali ili ziweze kuwaletea Watanzania maendeleo zikisimamiwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya katika bajeti hii lakini vilevile nitoe ushauri mbalimbali ambao utasaidia Serikali katika kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulimwengu wa sasa hivi umejikita katika uzalishaji, viwanda, biashara na teknoloja. Katika nchi yetu mwajiri mkubwa ni kilimo. Umefika wakati sasa Serikali iweke mkazo zaidi katika kilimo na tulete mapinduzi ya kilimo kwa mapana yake ili tufanye kilimo cha kibiashara *commercial farming*. Tutoe fursa na Serikali kwa makusudi kabisa itenge na kutangaza maeneo makubwa ya mashamba ambayo yatalimwa kibiashara ili kuzalisha kwa wingi. Sioni ni kwa nini Serikali kwa makusudi kabisa isijenge miundombinu kwa ajili ya umwagiliaji kwa kutumia mito na maziwa tuliyonayo na hatimaye kutangaza maeneo haya na kuwafanya wawekezaji na Watanzania wenyе uwezo kulima kilimo kikubwa na hatimaye kuzalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili tuweze kufaidi katika eneo hili na kuleta ajira kwa Watanzania pamoja na wakulima wadogo wadogo, ni lazima tujikite katika viwanda vitakavyokuwa vinaongeza thamani ya mazao haya. Viwanda hivi vitawasaidia wakulima wadogo wadogo kupata soko lao na kwamba mazao wanayolima yatapata soko la uhakika na

bei ya kuridhisha. Vilevile kama nchi, mazao yetu tutakuwa tumeyasindika na tutayaiza kwa thamani kubwa tofauti na ilivyo sasa kwamba mazao yaliyo mengi tunayaiza yakiwa ghafi na hatimaye tunanunua mali zilizopita viwandani kwa thamani kubwa na kwa fedha za kigeni. Nina uhakika kama tutafanya hivyo itatusaidia sana hata kupunguza ule uhafifu wa uwiano kati ya fedha zinazotokana na mauzo ya nje na fedha zinazotumika kwa manunuzi ya ndani (*balance of payment*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa makusudi kabisa ichochee eneo hili kwa kutoa motisha kwa wawekezaji wenye viwanda hivi ili waweze kuwekeza kwa wingi na hakika tutakuwa tumewakomboa Watanzania walio wengi kwani walio wengi wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingi mpaka sasa hivi na hasa vile mama ambavyo vimebinafsishwa havijaweza kuleta tija kwa Watanzania. Mfano mzuri ni kiwanda kilicho katika Jimbo langu la Kibaha Mjini, TANITA ambacho kilikuwa kina-*process* korosho. Kwa zaidi ya miaka kumi (10) sasa hivi kimebinafsishwa, kipo pale kama ghofu, hakijulikani hatima yake. Hata wale wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi pale bado wengine wanadai mafao yao na leo hii wakulima wadogo wadogo utawaona wakibangua korosho kwa kuzikaanga katika makarai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itatupia macho viwanda mbalimbali vilivyobinafsishwa na kuvisimamia na kuhakikisha lengo lililovifanya vikabinafsishwa linatimizwa, ni hakika tutakuwa tumeongeza thamani kubwa katika nchi yetu na tutakuwa sasa tunaelekea katika uzalishaji na kupata thamani ya mwisho ya mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii vilevile kuzungumzia miundombinu na uchukuzi kwa ujumla wake. Tunalo tatizo kubwa la usafiri na usafirishaji. Nizungumzie

kuanzia Dar es Salaam na hususan mpaka katika Jimbo langu la Kibaha Mjini. Hakika hakuna maendeleo kama hakuna *timely movement of goods and services*. Hatuwezi kuendelea kama hatuna namna ya kusafirisha mali pamoja na huduma mbalimbali tena kwa wakati. Leo hii ukitaka kufanya huduma yoyote Dar es Salaam na Kibaha ni wazi kwamba muda mwangi, zaidi ya asilimia 40 ya muda wote utapotea barabarani. Leo hii uwe na mgonjwa kutoka Kibaha unampeleka Dar es Salaam hata mahali pa pembedi kwa ajili ya kupaki ili hiyo *ambulance* ipite hakuna. Ni wazi kwamba, ukifanya mahesabu kila wakati tunarudisha nyuma maendeleo kwa zaidi ya asilimia 40 kwa ajili ya ucheleweshaji wa barabarani katika Dar es Salaam na Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali sasa ifanye makusudi, kwa sababu barabara hii ya Morogoro ndiyo pekee inayotumika kwa zaidi ya asilimia 75 katika usafirishaji na mawasiliano kati ya Jiji la Dar es Salaam na mikoa yote na tumeshuhudia adha kubwa ambayo inafanyika, Serikali sasa katika bajeti hii ichukue hatua za makusudi ili kujenga barabara hii hata kama ni *lines* tatu kila upande kwa maana ya *six lanes* ili tuweze kufanya *movement of goods and services* kwa wakati na tuweze kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nzungumzile sasa wito wangu katika bajeti hii. Wito wangu kwa Watanzania ni kwamba, nawashauri tushirikiane kwa pamoja kwanza kabisa tujitume na kufanya kazi. Tufanye kazi kwa bidii na maarifa. Kama kila Mtanzania jioni kabla hajakwenda nyumbani atajiuliza kwamba, leo nimefanya wajibu gani katika Taifa langu? Nimefika kazini kwa wakati? Nimefanya kazi yangu sawasawa? Sijaitumia ofisi ya Serikali kwa manufaa yangu kwa kazi zangu binafsi? Nimeitumia ofisi ya Serikali kufanya kazi za Serikali na hatimaye nimefanya kwa tija na maarifa? Nina uhakika Taifa hili litasonga mbele. Hii ni pamoja na kusisitiza nidhamu ya matumizi ya fedha hizi kidogo ambayo tunaipeleka katika bajeti hii, itakuwa ni bure hata kama

tutapeleka fedha hizi zote lakini kusiwe na nidhamu ya matumizi yake.

Niwaombe Watanzania, ndugu zangu watumishi wote pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge twende tukasimamie fedha hizi, tuhakikishe inamfikia Mtanzania maskini na kumkomboa kutokana na yale yaliyopangwa katika bajeti hii. Nichukue fursa hii kuipongeza sana Ofisi ya CAG na niseme sasa Serikali iwave nyenzo zaidi na ipanue wigo ili iweze kuhakikisha fedha hii ambayo tunaipigia kelele hapa na tunaigombania hapa inakwenda kweli kwa walengwa ambao ni Watanzania maskini kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa bajeti hii. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makof!*)

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii. Kwanza kabisa napenda kusema kwamba, siiungi mkono bajeti hii kwa sababu sioni ni kwa jinsi gani mwananchi wa pembezoni anaweza kufaidika na bajeti hii. (*Makof!*)

Katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa akitoa hotuba katika kitabu chake anasema kwamba, asilimia 70 ya bajeti ni matumizi ya kawaida na asilimia 30 ni matumizi ya maendeleo. Hivyo basi inamfikiria mwananchi aliye pale Songoro? Mama aliye pale Songoro Kijijini au pale Sakila King'ori anafaidikaje na bajeti hii ambayo asilimia 30 ni kwa ajili ya maendeleo? Kwa hiyo, ina maana mwanamke huyu aliye pale kijijini ataendelea kuteseka na kuumia katika nchi yake ambayo imejaa raslimali nyingi ambazo Mwenyezi Mungu ametubariki nazo na ametusaidia tuweze kumiliki. Napenda kusema kwamba ni muhimu Serikali ikaangalia uwezekano wa kupunguza matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa katika Kamati zetu na katika kuangalia vitabu vya bajeti tunaona fedha nyingi imeelezwa katika posho, kuelimisha watu nchi za nje, starehe, yes kulikuwa na hilo neno starehe. Lakini pia ningependa kusema kwamba ni vema bajeti hii ikaelekezwa katika maendeleo kwa sababu ni jana tu nilikuwa naangalia Televisheni nikamuona mwakilishi mmoja kutoka Ufaransa, mwanamke na alikuwa anaelezea kwamba Balozi wa Tanzania kule Ufaransa alikuwa amewaita wawekezaji wa Kifaransa na kuwaonesha nchi yetu ilivyo na rasilimali wanazoweza kuja kuwekeza.

Nikamsikiliza sana yule mama, alieleza kwamba nchi yetu imesonga mbele na ina rasilimali za kutosha. Kwa sababu hiyo basi kumbe sisi hatuhitaji kuendelea kuwanufaisha zaidi wawekezaji kwa kuwapunguzia misamaha ya kodi kwa sababu wao wenyewe wanakiri kwamba nchi yetu ina rasilimali za kutosha. Kwa hiyo, kumbe zile rasilimali tulizonazo zenyewe zinatosha kabisa kuwa vivutio. Hivyo basi, kumbe na sisi tunaweza tukauringia ule utajiri tulionao na tukawa na msimamo kwamba wawekezaji wa nje nao wasiweze kusamehewa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilichotaka kusema hapa ni kwamba, nimeangalia matumizi katika bajeti hii ni makubwa. Nikaangalia mapato ni madogo. Kwa hiyo, ina maana kodi hatuikusanyi inavyopasa au pengine wale wanaostahili kukusanya kodi wanaendelea labda kumpendelea mtu au kupokea rushwa na kupunguza kodi. Kwa hiyo, kodi iliyo kamili haikusanywi. Naitaka sana Serikali yetu ihakikishe makusanyo ya kodi yanakusanywa inavyopaswa kwa sababu ni kweli watu walioko vijijini wanaendelea kuteseka sana. Kama tutakaa hapa na kuipitisha hii bajeti bila kurudi na kwenda kuiangalia kama imemwangalia na yule mwananchi wa pembezoni mimi nitasikitika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna habari ya MKUKUTA - *Phase II*. Nataka kusema kwamba, sielewi kwa nini wameweka *Phase II* wakati hakuna kitu kinachoendelea? MKUKUTA ni mkakati wa kupunguza umaskini, je, umaskini umepungua au watu wanaendelea kuteseka na umaskini na MKUKUTA unaweka *Phase II*? Kwa hiyo ina maana kwamba, watu wanaendelea kufanya kazi katika zile ofisi ili kujinufaisha wao? Kwa sababu tungetaka kuona katika *Phase I* tathmini imefanyika. Tathmini ingefanyika ikaonesha kwamba, MKUKUTA *Phase I* labda umaskini umepungua kwa kiwango fulani, lakini badala yake tunaona Mtanzania wa kawaida anaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa kijijiini kwangu pale Sakila ambapo mwanamke anakwenda kuchota maji na punda katika karne hii ya sayansi na teknolojia. Punda anakunywa maji kwanza ndipo mama achote maji apeleke nyumbani. Kuanzia asubuhi mpaka jioni yuko anachota maji, ni saa ngapi atafanya kazi za kuzalisha? Ndiyo maana nasema bajeti hii haijamwangalia mwananchi wa pembezoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika elimu tunaambiwa kwamba wanafunzi wanaoijiandikisha katika shule za msingi ni asilimia 94 na asilimia 35 katika shule za sekondari. Nilikuwa naangalia utafiti uliofanywa na Hakielimu na kuonesha kwamba mwanafunzi anayemaliza sekondari sasa hivi hawezi kuandika, hawezi kusoma Kingereza, hata Kiswahili hawezi. Sasa kwa nini mambo kama haya tusiyape kipaumbele? Nilipokuwa nasikiliza taarifa ya habari wenzetu wa Kenya wao elimu wameipa kipaumbele na Kilimo wamekipa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa pia naangalia vitabu vya Kilimo Kwanza tangu mwaka 2009 Benki ya Kilimo ilitakiwa iwe imeanzishwa kwa kutengewa, *I think* nimesahau labda ni dola 500 au milioni 500, lakini mpaka sasa katika Taarifa hii ya

hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna msisitizo kwamba Benki ya Kilimo ianzishwe. Kumbe mpaka leo hiyo benki ambayo ilitakiwa tangu mwaka 2009 ianzishwe haijaanzishwa? Lakini ukisoma taarifa zilizo nzuri utaamini kwamba haya ni mambo ambayo yanakwenda kutokea kesho, lakini kumbe ni mambo ya kuzidi kuwadanganya wananchi. Wananchi wamechoka na huo ndio ukweli na sisi hatupendi amani ipotee katika nchi yetu kwa sababu tuna familia zetu na watoto. Tunaitaka Serikali ihakikishe inamwangalia na yule mwananchi wa pembezoni asiendelee kuteseka kwa bajeti ambayo haimlengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maji. Tunaambiwa kwamba Tanzania ni nchi ya pili Barani Afrika kwa kuwa na vyanzo vingi vya maji; bahari, mito na kadhalika. Tungeweza kuwa na uvunaji wa samaki na tukarudisha viwanda vya kusindika minofu vijana wetu na hata wanawake wakapata ajira. Hivyo tukapata zaidi pato la Taifa kuliko kuendelea kung'ang'ania sigara na pombe. Jamani naomba niwakumbushe kwamba Taifa lolote ambalo linaweka ibada za sanamu mbele haliwezi kuendelea katika mipango yake ya maendeleo kwa sababu limeweka ibada za sanamu mbele. (*Makof*)

Nataka kusema kwamba, kama tutaendelea hivi tutakuwa kila mara tunalaumiana, tunashangaa mbona mambo hayaendelei! Juzi pale Dodoma Hoteli nilishangaa kuona kwamba kumbe tuna wataalam wazuri! Dokta Ngowi alikuwa pale akituelezee jinsi ilivyo muhimu kuondoa kodi ili kuwasaidia wananchi. Lakini tukashangaa huyu mtaalam alikuwa wapi siku zote, hakupewa nafasi na Serikali yake? Ilikuwaje? Lakini ndiyo mambo kama hayo. Kama Taifa limeweka mbele mambo ya kuchuna ngozi, tunasikia kule Mbeya watu wanachunwa ngozi, kule Shinyanga bibi wazee wanauawa na albino wanauawa. Haya ni mambo ambayo hayafai. Tunahitaji kuyaacha na hivyo tutaweza kufanikiwa

katika bajeti hizi ambazo tunazileta na maendeleo mengine pia yanaweza kuonekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hapo. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rebecca. Nikushukuru kwa mchango wako. Sikukuelewa tu mahali uliposema kwamba matumizi ni makubwa kuliko mapato kwa maana ya kwamba bajeti haina mizania. Sina hakika sana.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni jambo lillio bayana humu ndani kila mmoja anajua, maisha ya Watanzania huko nje ni magumu sana. Maisha ya Watanzania huko vijiji ni magumu zaidi. Maisha yanazidi kuwa magumu kadri siku zinavyokwenda. Ni jambo lillio wazi kwamba hivi sasa matumaini ya Watanzania wengi juu ya maisha yao mazuri yanazidi kuyeyuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo lillio wazi kwamba matumaini ya maisha bora kwa kila Mtanzania sasa hivi yamesimama kama mshale wa saa mbovu. Nitafika Ludewa; Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopita wamezungumzia maeneo kadhaa. Mie nina maoni tofauti kwamba, kwa jinsi tulivyo sasa hivi na Serikali yetu hili hata tungeongeza mapato namna gani bado hatuwezi kwenda. Hatuwezi kufika na sababu yetu ni moja tu, hatuna nidhamu kwenye matumizi ya fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai sana turekebishe hilo suala moja na mambo yatakwenda. Tuweke nidhamu kwenye kukusanya fedha. Naiomba sana Serikali yetu iwe na nidhamu kwenye kidogo hiki tunachokipata leo. Kama hiki kidogo tunachokipata leo hatuna nidhamu nacho, tukipata kikubwa tutakitumiae vizuri? Kama leo tunapata raslimali hizi za kwetu tunashindwa kuzitumia vizuri, tunaomba

Mungu wigo wa mapato uongezeke na tunatarajia kukusanya zaidi na zaidi, lakini tutakuwa tumechukua maji tunatia kwenye bakuli inayovuja. Ninachokiona kikubwa sana tuna mifano, Wabunge wengi humu ndani ukiwatazama unaona kabisa wana uoga na uoga huu unatokana na dhana ya bajeti zilizopita ambapo tumeshuhudia, tumeona, tumeahidi hatujatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunesema ndani ya Bunge hili mara kadhaa. Hata mwaka jana kwa mfano, Wizara ya Ujenzi tuliahidi sisi wenyewe humu ndani tuliwaambia Watanzania tukapanga shilingi trillioni 1.5, hata nusu yake hatujatekeleza. Mwaka jana mtakuwa mashahidi tulikaa hapa mbele tukagoma kupitisha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Bajeti ya pili tuliyogoma kupitisha ilikuwa ni ya Wizara ya Uchukuzi. Waziri wetu Mkuu akaja kutusihu Wabunge hapa, "Naombeni mpitishe bajeti hii tutaongeza shilingi bilioni 90". Katika hizo shilingi bilioni sita (6) zilikuwa zinakwenda Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Katika bilioni sita (6) tumepeleka shilingi milioni 200 peke yake mpaka leo ninavyozungumza. Ndiyo maana Wabunge wanakuwa na woga na wasiwasi, tunakuwa wepesi wa kupanga, wepesi wa kuandika mambo vizuri utekelezaji unakuwa ni wa wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kabla hata hatujaomba *TRA* waongeze makusanyo Serikali yetu iwe makini na ijitazame vizuri zaidi kwenye suala la nidhamu ya matumizi ya fedha kidogo zinazopatikana. Waheshimiwa Wabunge kama Serikali yetu haina nidhamu kwenye matumizi ya fedha hatuwezi kwenda. Jimboni kwangu Ludewa mwaka jana tulipitisha katika Bunge kama hili fedha kadhaa lakini mwezi Agosti mwaka jana tulipaswa kupeleka sh. 84,000,000 Serikali ilipeleka sh. 14,000,000 peke yake. Wizara ya Maji Serikali ilipaswa kupeleka sh. 13,000,000 lakini Serikali yetu hii ilipeleka shilingi 500,000 tu. Mwezi uliofuatia Serikali ilipeleka Wizara ya Afya shilingi sifuri, mwezi uliofuatia Serikali yetu hii hii kwenye

ujenzi ilipeleka shilingi sifuri. Fedha tunapitisha, tunapanga lakini utekelezaji hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasihi sana tuisimamie Serikali yetu iwe na nidhamu katika matumizi ya fedha. Kupanga hapa ni suala lingine na utekelezaji ni hatua nyingine. Tatizo tulilonalo sio wigo mdogo wa mapato, sio makusanyo kidogo ya mapato, bali kwa hakika ni matumizi mabovu na tunachokipata na viongozi wetu tuliuwaweka madarakani. Sasa kama Waziri Mkuu anaweza akafika hapa akaomba kwenye kipindi cha maswali Alhamisi akasema tutaleta shilingi bilioni sita, leo usafiri wa maji ni mgumu kule mnapeleka shilingi milioni 200 peke yake. Tunasema nini na tunafanya kitu gani. Waheshimiwa Wabunge nyie wote mna azma njema na nyie wote mna nia njema lakini bila kuwa na nidhamu hatuwezi kufanikiwa. Hili ni suala la *compliance period* kwenye Serikali yetu. *TRA* wamekusanya asilimia 104, *TRA* msiwalaumu, *TRA* fedha mliowapangia kukusanya wamekusanya hao. Zile fedha zote zinakwenda wapi, ndio suala la msingi la kuijuliza hapa Waheshimiwa Wabunge. Ni wepesi wa kupanga, ni wepesi wa kusema hapa ndani, lakini utekelezaji ni duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo rai yangu kwa Serikali yetu ni kwamba, nahisi sana kabla hata hatujaongeza, kabla hatujakwenda kukopa nje tuimarishe nidhamu katika matumizi ya fedha. Fedha tunazopanga hazifiki tunabaki hapa kuwalaumu watendaji wa Halmashauri, tunawaoneshea vidole, wanatafuna fedha lakini si kweli Serikali haipeleki fedha, ni suala la nidhamu. Kwa hiyo, ninachokiona kinasumbua sasa humu ndani ni uongo wetu tuliousema Bungeni mwaka jana, ndio sasa unatusumbua hapa ndani. Tulisema tutafanya hiki hatujafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba turekebishe hiyo sisi wenyewe kwa vitendo vyetu kwa sababu bajeti ambayo haitekelezeki haina manufaa kwa wananchi na wala kwa Watanzania. Maisha ni magumu sana na Watanzania leo hii

ukiwaambia walipe kodi, sioni kama kuna shida. Watumishi sasa hivi wanalia na *PAYE*. Lakini kimsingi walalamike na ile kodi kwa sababu hawaoni kodi yao inakwenda wapi na inafanya kitu gani. Watanzania leo ukiwaambia wakae miaka mitano wajifunge mikanda, watajifunga hawana shida na hilo. Lakini shida *we are fasting for no reason we should fast while we know* hizi fedha tunajinyima tunajifunga kibwebwe, zinakwenda kufanya kitu fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawasihi sana wenzangu na nasema haya kwa uchungu sana kwamba pamoja na rasilimali tulizonazo leo hii Tanzania bado ni nchi omboomba. Maana yake wenyе vipimo vya ulimwengu sasa hivi kwanza inaanza Afghanistan inafuatia Iraq halafu Tanzania kwa kuomba fedha nyingi nje bila sababu ya msingi na hizi fedha zinakwenda wapi. Mwaka 2008 deni la Taifa lilikuwa ni shilingi trillioni tano, mwaka 2011 lilikuwa ni shilingi trillioni 14, leo ni shilingi trillioni 22, fedha zinakwenda wapi? Kukopa sio shida hata kidogo, lakini tukope tuone *replica* yake *on the ground, value for money*, hizi fedha hata kulipa baada ya miaka 50 ni deni kwa Watanzania. Sio sisi, watoto wetu, wajukuu wetu watalipa. Kwa nini tunakopa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunakopa wakati tuna rasilimali zote hizi? Kwa nini tunakuwa omboomba tunafika mahali tunamdhaliisha Rais wetu, kila siku anakwenda nje kuomba. Itafika mahali tutamwambia Rais sasa usisafiri, ubakie hapa hapa ndani usiende kuomba. Kidogo tulichonacho hapa ndani tukitumie vizuri kwa maslahi yetu, hakuna haja ya kwenda kukopa nje ndio hatua tuliyofikia. Rasilimali zote hizi tulizonazo, Tanzania nchi tajiri, wananchi wake ni maskini. Nidhamu kwenye matumizi ya fedha ndio jambo la msingi na kwa kufanya hivyo peke yake naona utakuwa ukombozi na ufumbuzi sahihi wa matatizo yetu. Kila mmoja analalamika kuwa na mgomo wa Madaktari, walimu nao sasa wanakuja, ni suala la kutazama kwa makini sana na sekta zingine tu hazisemi, wazee waliostaifu huko vijijini nao wanataka

kugoma, sasa sijui watamgomea nani! Lakini kimsingi tutengeneze maisha mazuri kwa kila mmoja. Hata sisi itakuja siku moja tutazeeka tu tutakuwa wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupitishe sheria hapa ya pensheni kwa ajili ya wazee, kila mzee anapofika umri fulani na wale wazee wametumia nguvu zao na umri wao mpaka wamestaafu wakilitumikia na kuliendeleza Taifa hili. Nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge tupitishe sheria hii wazee wote wapewe pensheni asilimia 25, aidha alikuwa mwajiriwa au sio mwajiriwa kwa sababu na sisi itakuja kuwa wazee. Kwa hiyo sheria yetu hii pia itatusaidia na sisi huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele imegongwa. Ahsante kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu bajeti ya kipindi hiki cha mwaka 2012/2013 katika kuongelea mambo mbalimbali yanayohusu Taifa letu. Kwanza kabisa nisije nikassahau kwa sababu nitakuwa nimemwonea Waziri wa Fedha ambapo ni juzi tu ndio amekabidhiwa mzigo huu, wakati anakabidhiwa ndio na bajeti tunatarajia kuianza, tukikataa bajeti yake nadhani tutakuwa hatukumtendea haki. Kwa hiyo, naunga mkono bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa kuanzia hapo alipoishia ndugu yangu, mtoto wangu Filikunjombe, napenda niseme kwamba, aliyojasema ni ya kweli kwamba matumizi ndilo tatizo. Sasa basi nipende kutoa ushauri kwamba ifike mahali sasa nakumbuka wakati Waziri mwenyewe wa sasa wa fedha tukiwa naye *bench* huku tena alikuwa mbele yangu tu hapa alikuwa ni mzuri na mpaka tukajua kwamba ni Mchumi aliyebolea, akawa anatoa michango yake humu ndani ya Bunge. Alikuwa anatoa michango kweli ya kuweza kushauriana, nadhani ndio maana alionekana na kuchaguliwa

kuwa Waziri wa Fedha. Lakini alichokuwa akisema ni kwamba, hebu ifike mahali kama nadhani nitamsingizia anisahihishe siku akijibu. Alikuwa anatoa kauli nzuri kabisa ya kutia moyo kwamba, jamani katika masuala mazima haya ya bajeti au ya matumizi ya mapato yetu tufike mahali tuwe tunakaa aidha *quarterly* au kwa nusu mwaka kufanya tathmini ya *trend* ya mapato yetu na matumizi yetu, hapo ndipo tutajua kudhibiti fedha za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kabisa alikuwa ana picha ya namna hiyo. Sasa na mimi niombe kurudia kauli yake. Fedha itatoka kuanzia Julai unaonaje Desemba tuone kama kweli fedha hiyo ya mapato yetu inakwendaje kutoka katika matumizi na hapo ndipo tutajua kweli wewe ni Mchumi na kwamba unaibana Wizara yako na kwamba unakwenda vizuri. Ushauri huo naurudia kabisa kwamba tufike mahali tutafute mfumo huo tuufanyie kazi, labda hapo tutaona hivi ni Wizara ipi iko kazini na Wizara ipi iko *idle* ipo ipo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda niongelee kuhusu suala zima la miradi yetu hii ambayo tunaitumia katika matumizi ya fedha zetu. Miradi mingine ndiyo inayotusababisha hata uchumi wa nchi yetu urudi nyuma. Miradi ya malambo, visima kwa mfano, tuseme miradi yote hii ya maji unakuta hawa wakulima wazuri kwa mfano kabilia la Wasukuma, ni wakulima wazuri sana. Lakini walime lini pamba, walime lini mahindi, chakula au mazao yoyote, wanabaki wanazunguka kwa sababu ya kukosa kuwekewa miradi ya huduma katika maeneo yao. Miradi inakwenda kutekelezwa visivyo, unakuta malambo yanakwenda kuchimbwa kusiko na mifugo unategemea nini wale wanaopelekewa hayo malambo hawawezi kuyatunza, hawana uchungu nayo badala ya kuwapelekea wale wanaoyahitaji wajue kabisa kwamba huu mradi umeletwa kwetu, tukae tutulie sasa tuzalishe, tuinue uchumi wa nchi hii, wanakuwa wazururaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali tuwe waangalifu kabisa katika kutoa miradi mbalimbali katika maeneo ya nchi yetu. Tunapeleka miradi pasipo matokeo yake, wananchi hawafanyi kazi ipasavyo. Utasema nini kama ndio hali halisi iko hivyo uje uwaambie uchumi utakuwa je, utakuwa kwa kuzurura? Utakuwa kwa kutafuta huduma za nchi hii, haiwezekani! Naomba kabisa miradi hii tunayoipeleka katika maeneo tena nishauri kuweko na uchunguzi. Ukienda kuwatafuta wale wanaozurura na mifuko utawajua tu wanatoka wapi. Sasa kwa nini tusiwapelekee hiyo miradi. Nilikuwa na ushauri huo katika mazungumzo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimesoma katika kitabu cha mpango, anasema Serikali iko tayari kununua mahitaji ya chakula nje na sukari na vitu vingine. Tatizo la nchi yetu ni usambazaji wa vifaa hivi. Wakulima hawa wa Songea kwa maana ya Ruvuma, Rukwa na huko Kigoma wanabaki na vyakula, Kilombero wanabaki na sukari, sisi huko ambako tunahitaji hatuoni matokeo haya. Mtasema uchumi ukue, ukue kwa kukaa na vitu ndani, hautakua hata kidogo. Niwaambie ukweli, tufike mahali sasa tuweze kufanya *distribution* ya vitu hivi ipasavyo kwa haraka tunapozungumza katika Bunge hili mwandike myajue haya, tengeni fedha kutokana na bajeti. Nilishawahi kuuliza safari moja, Waziri mmoja katika hili akaniambia Mama Hewa hakuna fedha, hebu ona hayo. Hakuna fedha wakati wananchi wa Mikoa ya Kusini wanataka kuza mahindi yao wapate fedha mnawakataza. Wakisema sasa pelekeni basi humu humu nchini hakuna fedha, tunapata jibu lipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe katika hili wahusika waweze kuliona na kulifanyia kazi ili tusije tukawa manamba wa kuombaomba vyakula nje kumbe na mazao mengine tunayo na yanaoza humu humu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa vile kengele ya kwanza imegongwa nipende kuongelea suala ambapo watu

wanakataa kuunga mkono hoja ya bajeti. Jamani ungeni mkono miradi yenu kwa mfano hata wa Kigoma mnatengenezewa barabara, mnatengenezewa sijui daraja la Malagalasi, hii fedha inasubiriwa, mnasema hapana. Naomba waunge mkono bajeti hii ili kusudi nchi hii miradi yake itekelezeke vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nasema, jamani tunaongelea kufufua viwanda vya pamba tutavifufua na nini. Naomba suala la pamba liwekewe umuhimu wa kwanza kabisa. Wasukuma wamelima huko pamba na kabilia zingine zinazolima pamba wamelima jamani, wanachosubiri ni msimu. Mapema iwezekanavyo tutawakomboaje hawa watu waliojitoso mapema hivi. Mnazungumzia kufufua viwanda, mnatafuta ajira za vijana, ajira ndizo zimo humo katika viwanda, vikifufuliwa kutokana na uuzaji wa pamba humu humu nchini. Niwaombe ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge Serikali yetu ni sikivu, sikieni hili, nyanyukeni mpeane zamu hata kama ndio unapaswa kukaa humu, mwingine anyanyuke aende akaone na msimu uanze mara moja kwa bei ambayo ni stahili. Wenzangu wamezungumza humu shilingi elfu isishuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja hii na nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Maria Hewa hii elfu ni kwa biashara gani?

MHE. MARIA I. HEWA: Jamani ni kwa hilo msije mkasema mambo, nisitamke Kigogo. Samahani.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mengi yameshazungumzwa kuhusu bajeti hii na michango mingi imeshatoka na nashukuru kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa yale ambayo nayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianzie na suala zima la mfumko wa bei. Watanzania walitegemea sana kwamba bajeti hii itawapa matumaini, bajeti hii angalau itamawaliza kiu yao hata japo nusu yake na walitegemea kwamba yale matatizo makubwa ambayo yanawakabili kimaisha basi yanaweza kupatiwa ufumbuzi na bajeti hii. Matokeo yake tumekuja kujikuta kwamba bajeti hii imeendelea kuonyesha namna gani mfumko wa bei umezidi kuwaandama na kuwaathiri wananchi wetu. Mwaka jana tulikuwa na asilimia takribani sita pointi za mfumko wa bei, safari hii tuko katika asilimia 17 pointi hii ni sawa sawa na kusema maisha yamepanda kwa asilimia 120. Ni hatari kwa watawala, lazima tukae tuangalie namna gani tunaboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kitu ambacho kiko dhahiri, hili linaathiri hata suala zima la uzazi wa mpangilio. Linaathiri watoto wetu waliozaliwa, linaathiri na linasababisha uongezekaji wa vifo vyta akinamama wajawazito. Nataka niache kidogo niende katika kitabu cha bajeti. Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba pato la Mtanzania limekua kutoka shilingi 600,000/= kwa mwaka hadi kufikia shilingi 700,000/= mwaka huu na *most indicators* sasa sijui hapa kama alikuwa anakejeli au kama ni *indicators*, ndiyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema kwamba Watanzania sasa hivi wanamiliki baiskeli, wanamiliki pikipiki, Watanzania wanamiliki simu za mkononi. Jamani mmechoka kuongoza? Baya zaidi ni kwamba sasa hivi Serikali inataka kuongeza malipo zaidi katika *airtime*. *Indicator* moja waliyoieleza ni kwamba Watanzania wanamiliki simu za mkononi, lakini wakati huo huo wana mpango wa kutaka kuzidisha gharama za utumiaji wa simu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu upo, hivi hawa Watanzania wamewakosea nini? Hebu tuambieni au uzuri unakuwa wakati wa kuomba kura tu unapofika wakati wa Bajeti hawana tena

thamani? Hivi leo unavyopandisha *airtime* umekusudia nini na wakati moja katika *indicator* yako inaonesha kwamba pato la Taifa limekuwa ni kumiliki simu ya mkononi. Leo simu ile ile unakwenda kumpandishia tena gharama za upigaji wa simu. Baya zaidi ni kwamba waathirika wakubwa ni sisi Wabunge vile vile. Hakuna Mbunge ambaye hatumii zaidi ya milioni moja hapa kupiga simu kwa mwezi. Leo hii *airtime* itakapopandishwa itakuwaje jamani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna njia nyingi ambazo nafikiri Serikali ingetafuta kufidia hii kuliko hii *indicator* moja kutaka kurudi tena kuwapokonya hawa wananchi. Kwa mfano, katika ukurasa wa 63(4) kuanzisha kodi itokanayo na uuzaaji wa rasilimali *capital gain tax* kwenye uuzaaji wa hisa za kampuni za ndani unaofanywa na kampuni mama ya nje ya nchi. Hapa huu ni mwanya ambao fedha zinapotea. Hii mifano inaonekana zaidi katika makampuni ya simu. Nataka nichukue mfano wa Kampuni moja ya Simu, *Celtel* ambayo ilikuwa ni kampuni ya Netherland iliiza hisa zake kwa *Celtel* Tanzania ambao walishirikiana pamoja na *TTCL* baadaye wakauza tena kwa *Zain* na *Zain* imeuza tena kwa *Bat Airtel*, hawa wote wanauziana hisa tu, lakini hawauziani pamoja na vitu vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri watakapouza pamoja na vile wanavyovimiliki hapa tutaongeza pato la Taifa. Lakini kuwaachia tu kwamba wenyewe wauziane huko kwa huko kwa kweli hapa tunapoteza. Leo tunakuja kumkamua huyu ambaye anapiga simu kumpigia mtoto wake, tunataka kumkamua huyu kweli wakati watu wanafanya biashara kubwakubwa na hatuwafanyi chochote! Hii sio halali na wala halikubaliki. Waoneeni huruma wananchi wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na bajeti hii ilivyo hapa ndani tumekuta wengi wamejiita wachumi, wachumi. Kama kuna kipengele ambacho kitaniruhusu kesho katika *Order Paper* ikiwezekana turuhusiwe kuleta bajeti yetu rasmi ya

Chama cha CUF. Kwa sababu Bajeti zenyewe hapa hazikubaliki. Bajeti ya Upinzani sio, Bajeti ya Chama Tawala sio, sasa za nini. Sisi tuna mchumi ambaye anakubalika Kimataifa na nyote mnafahamu Profesa Lipumba na Bajeti yake mbadala ipo tayari. Kama naruhusiwa naomba tupewe hiyo nafasi ili tuwasilishe Bajeti ambayo itakuwa ni mkombozi wa Mtanzania. Hili sisi hatuna masihara nalo na wananchi wajue na wameona mifano ambayo inatokea humu ndani ya Bunge. Chama Tawala na Chama Kikuu cha Upinzani badala ya kujadili Bajeti mnajadili mambo ambayo hayaeleweki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka kuongea suala la deni la Taifa. Deni la Taifa *speed* yake ya ukuaji ni kubwa sana. Kazungumza mama yangu mmoja hapa anasema halina tatizo, lakini sisi tunasema deni ni deni. Hata kama unadaiwa senti tano ni deni. Liwe linahimilika liwe halihimiliki hilo ni deni na unapochukua deni usijifananishe wewe na Marekani. Uchumi wa Marekani na Tanzania ni tofauti. Huwezi kumwambia Mtanzania wa kawaida kwa sababu Marekani inakopa na sisi tuna uwezo wa kukopa. Katika akili ya kawaida haiingii. Marekani ni nchi kubwa, uchumi wake mkubwa na akiona unamurai unamkera anaweza hata kukupiga. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tukubali kwamba, hii bajeti haimsaidii mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, siungi mkono hoja hii mpaka pale pengine nitakamposikia Waziri kaondoa suala la kuongeza kodi katika matumizi ya simu za kawaida. Nashukuru. (*Makof*)

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu na afya ili tuweze kuzungumza na kujadili Bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kutuletea Bajeti ambayo nitaijadili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajadili vipaumbele vya Serikali halafu mwishoni nitakuja kuishauri Serikali. Tukiangalia katika mwaka huu wa fedha tunaomalizia sasa vipaumbele vya Serikali vilikuwa sita. Ambavyo ni miundombinu, kilimo, maji, maliasili, viwanda na maendeleo ya rasilimali watu. Ukiangalia katika kitabu cha mpango utaona katika ukurasa wa 20 kuna changamoto kama 11 zimeanishwa pale.

Changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha, kuongezeka kwa mfumko wa bei, kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, upatikanaji wa fedha toka kwa wafadhili, uhaba wa wataalam na kadhalika. Ukitathimini vipaumbele vya mwaka huu tunaomalizia utaona kabisa kwamba utekelezaji wake haukuwa mzuri. Lakini ukiangalia sasa vipaumbele hivyo na utekelezaji wake pamoja na changamoto ambazo zimeanishwa katika kitabu hicho cha mpango nilikuwa nafikiri kwamba, hii ingepelekea Serikali kuja na vipaumbele vingine tofauti na vipaumbele vya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuja na vipaumbele vilevile. Katika ufahamu wangu nafikiri kwamba, maana ya maneno vipaumbele ni kwamba unakuwa na vitu vingi lakini unachagua kati ya vitu hivyo vingi kuwa na vitu vichache ambavyo sasa utaelekeza nguvu yako zaidi. Kwa hiyo, nilitegemea kwamba Serikali sasa ije na vipaumbele ambavyo ni vichache ili sasa Serikali iweze kuzitumia zile rasilimali fedha kwa kuelekeza katika vipaumbele hivyo muhimu ili kuifanya Serikali isitegemee sana zile fedha ambazo zinatoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuja na vipaumbele vichache kungeweza kusaidia sana Taifa kama Taifa kuimba wimbo mmoja wa kuwa na vipaumbele vichache ambavyo kwanza tungekuwa na uhakika wa kuvisimamia vizuri zaidi, lakini pia mwishoni tungeweza kuja kutathimini na kuona ni

wapi tumekosea na kwa sababu gani. Vilevile ingeweza ikawapa hata wafadhali wale wazuri ambao wanetusaidia kuweza kuwa na moyo wa kutusaidia na kuelekeza nguvu zao katika vipaumbele vichache hivyo ambavyo tungekuja navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilihakikishie Bunge hili, Watanzania na Serikali kwamba tukienda kiujumla jumla hivi kwa kuleta vipaumbele vilevile kila mwaka na vingi kwa kiasi hiki, sioni ni namna gani tutaliondoa Taifa hili mahali ambapo lipo kwa sasa. Kwa maana hiyo basi, nataka sana niishauri Serikali, ije na vipaumbele vichache ambavyo vitatufanya sisi kama Taifa tuweze kuelekeza nguvu huko, kwa mfano, Serikali ingekubali kuja na vipaumbele vitatu tu ambavyo ni miundombinu, viwanda pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipaumbele cha miundombinu pale tunaona kwamba tuna nishati, barabara, reli, bandari na mawasiliano. Tukivitengeneza vizuri hivi vitu ambavyo nimevitaja hapa ambavyo vipo katika kipaumbele cha miundombinu hakuna jinsi ambavyo tutakwepa kutatua tatizo la ajira, tatizo la bei, tatizo la pato la Taifa na hata kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye suala la kilimo; kilimo kinaweza kikaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania. Kwa kufanya hivyo basi, tungeweza kabisa kuhakikisha kwamba, suala la ajira tumelipatia suluhisho. Lakini pia tungeweza tukazalisha bidhaa ambazo zingeweza kutusaidia sana kupunguza bei ya vitu lakini tukapata pia fedha za kigeni. Lakini pia tungeweza tukaelekeza nguvu kwenye eneo la uvuvi ambalo liko katika kilimo hicho hicho, tungeweza tukahakikisha kwamba wavuvi wanavua samaki wengi ili Watanzania waweze kupata samaki kwa bei rahisi wangeweza kuwa na afya njema na kuchapa kazi kwa nguvu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ingetuwezesha kuhakikisha kwamba, hatuagizi samaki kutoka katika nchi nyingine kama

Japan na kadhalika. Ingetuwezesha pia kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inaangaliwa kwa ukaribu. Lakini inatengewa fedha nyingi zaidi ambazo zingesaidia sana kufufua vile Viwanda vya Kusindika Nyama ambavyo vingetusaidia sana kwenye ajira na mambo mengine. Katika eneo la viwanda tungeweza tukahakikisha kwamba madini yetu yanaangaliwa vizuri, lakini tunaweza pia kuhakikisha mikataba ya kwenye madini inapewa umuhimu wa kutosha. Kwa kufanya hivyo, katika sekta hii tungeweza kupata fedha za kigeni ambazo zingesaidia kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa na vipaumbele vichache nafikiri ingesaidia sana Serikali kuhakikisha kwamba matatizo ya Watanzania yanakwisha. Lakini pamoja na vipaumbele hivyo vitatu nilivyovitaja ni lazima Serikali ihakikishe kwamba inasimamia vizuri ukusanyaji wa kodi, kusimamia watendaji ambao ni wafanyakazi wa Serikali ili wawze kuchapa kazi badala ya kuingia ofisini na kusaini na kuondoka au kukaa tu. Punguza matumizi ya Serikali yasiyo ya muhimu, kuangalia upya Sheria ya misamaha ya kodi iweze kushuka kuanzia asilimia 0.5 mpaka asilimia moja, lakini pia Serikali kuwa makini na mikataba ya madini na mikataba mingine ambayo inasainiwa nchini. Kila Mtanzania atakiwe kufanya kazi na Serikali ifike mahali sasa iwaeleze Watanzania kwamba nchi hii sio ya kijamaa kwa asilimia mia moja na kwamba mtu hawezi kula bila kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali ikija na vipaumbele vichache na ikaweza kusimamia mambo haya niliyoyataja, mimi sina wasiwasi kabisa wa kuliondoa Taifa hili mahali liliipo na likaweza kufika mahali pengine ambapo Watanzania watakuwa wanapata mahitaji yao ya muhimu kwa bei nzuri zaidi. Nasema kwamba tukiendelea hivi ndiyo hapo chuki kwa wananchi itaendelea kwa sababu tunagusa hapa, tunagusa pale na mwisho wa siku wananchi wanasema hawaoni kitu kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwa mwaka mzima wa fedha, Jimbo la Ukonga limetengenezewa barabara ya lami nusu kilomita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mie kidogo nizungumzie namna gani tunaweza tukajikwamua kiuchumi. Nawauliza Wabunge wenzangu kwa mfano, tungerekodiwa mwaka jana kwenye Bajeti namna tulivyochangia, halafu *record* ile ikawa inatiwa kwenye vyombo vyahabari siku baada ya siku wananchi wangetofautisha tuliyozungumza mwaka jana na mwaka huu? Wasingeweza kutofautisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini? Kwa sababu kila tunapokuja hapa tunazungumzia matatizo yale yale. Nafikiri tungeyapa mambo au Wizara *priorities* ili zikazalisha kwanza, tukatoa ajira kwa vijana halafu tukaona pato la nchi linakua namna gani. Tuna dhahabu, almasi, *tanzanite*, gesi, makaa ya mawe, kesho kutwa *uranium* lakini bado tunasuasua palepale na matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi ukiwa mbovu na watu wakajenga tamaa zao za ublnafsi Serikali yoyote haiwezi ikaendesha mipango yake kwa maslahi ya walio wengi. Mwaka jana tulitaka Mlima Kilimanjaro uingie katika *Seven Wonders of the World* nafikiri sasa hivi wakati umefika tuiingize kwenye *Guinness World Record* kwamba ni nchi ya kwanza duniani kuwa na *national carrier* yenye ndege moja. Ndiyo, Rwanda wana ndege sita, wana mipango ya kuongeza ndege mbili zaidi nchi ndogo kama ile ya Rwanda. Lakini sisi tunasuasua kwa ndege moja. Dar es salaam, Arusha, Kilimanjaro *finito*. Tutakwenda kweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natoa mapendekezo yangu. Kwanza ieleweke kwamba asilimia 50 ya makusanyo ya mapato ya kodi inasemekana hupotea kwa njia ya rushwa. hatuna uzalendo. Ule uzalendo uliokuwepo miaka ya 60 na 70 haupo tena. Kila mtu anapowekwa anataka kuchukua chake mapema. Tunakuja humu kwa ushindani wa kisiasa, sio wa kiuchumi wa kujenga nchi kuwakomboa wale waliokuwa wanyonge. Leo nimemkuta mama mmoja wakati nakwenda kununua dawa hapa mjini Dodoma ana bakuli juu lina aina nne, tano za matunda yanayoanza kuoza anatembeza hayana mnunuzi. Tunamfikiraje mama yule? Ana watoto wangapi nyumbani, anaishije, ana matumaini gani ya kesho?

Kama sisi viongozi, kama sisi Wabunge tunakuja humu na kulumbana bila ya kujenga imani ya kuwa pamoja kujenga uchumi imara kuwaondoshea matatizo walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wala hutajenga uchumi hata siku moja kwa kuzidisha kiwango cha kodi kwa sigara na bia. Hatuko Cuba sisi. Niletii mtu mmoja tu Tanzania anayevuta sigara nakupa zawadi na kesho mtatuletea kwamba mtapandisha kodi ya *pipe*, nani anavuta *pipe* hapa Tanzania? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tujaribu kuangalia hili shirikisho la Afrika Mashariki litatusaidiaje kiuchumi, tuende na hili jambo dogo tu. Tanzania ni nchi pekee katika Afrika Mashariki inayopakana na nchi zote za Afrika Mashariki yaani hizi *East African Community*, Tanzania inapakana na Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi lakini tumetumiaje mipaka hii kusafirisha bidhaa zetu, tumechangamshaje masoko yaliyo karibu na mipaka kuwaruhusu wa jirani kuingia nchini mwetu na kununua bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi kubwa ukishindanisha hizi nchi, Tanzania ukiichukulia kwa Kilomita za

mraba watu wa Tanzania 47 kwa kila kilomita moja za mraba, wakati Kenya ni watu 70, Uganda 139, Burundi 301, Rwanda 403. Hatuoni tuna kila sababu ya kuitumia ardhi yetu tukavuna uchumi wa nchi jirani, tukainua maslahi ya watu wanaoishi vijijini na mipakani, hatulioni hilo? Tukainua uchumi kwa njia ya bidhaa, kwa njia ya kilimo, kwa njia ya utalii, tukashirikiana na hizi nchi za Afrika Mashariki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii gesi ambayo tunasema tunataka kuzalisha, hii hii tunaweza tukafua umeme na tukazizua nchi zote ambazo zimepakana na sisi, lakini ni nani anafikiria mambo hayo, kila mmoja anafikiria kuingia mikataba na watu wanaochimba madini, watu wanaokuja na mikataba mibovu ili apate, ukishakupata itakusaidia mali mbovu!

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wote walioifanyia ubadhirifu nchi hii kwa njia ambazo si halali *Wallah* zitawatokea puanı pesa zile, kwa sababu *majority* ya watu ni maskini, watu wanazaliwa hawawezi kununua dawa, hawana Hospitali za kisasa, hawana nguo bora, hawana chochote kinachowasaidia. Sisi leo tumebaki tunadai mishahara minono kwa viongozi wa Serikali pamoja na sisi kwa nini tufiche, kwa nini tusiwatetee wale walio wengi, waliotuchagua wakatuleta hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pamba hii hapa utakapomwambia mtu yejote kwamba pamba inazalishwa Tanzania lakini Tanzania hawa-*produce* vitambaa ni jambo la ajabu. Mauritius hawana pamba wanasafirisha nguo kupeleka Italy, kupeleka Ureno, kupeleka Spain na kupeleka nchi nyingine za Ulaya. Pia hutaskia wala hujaskia watu wa Sychelles, Mauritius, kufanya maandamano ya kupinga Serikali kwa jambo lolote kwa sababu wana uchumi imara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo viwanda viwo nchini hatuwasaidii wenye viwanda tuka-*subside* wakazalisha pamba wakatengeneza nyuzi, wakatengeneza majora ya vitambaa,

wakatengeneza vitambaa vikatumika nchini, matokeo yake zinaingizwa nguo kutoka Pakistani, Bangladesh, China, India kwa mlango wa nyuma bila ya kulipiwa ushuru halali wakaua viwanda vyta ndani kwa nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, piga marufuku mara moja bandarini pale, *TRA* itafute watalaam watakaoweka *database* ya kuona namna gani nguo zinazalishwa nje na bei gani na zinaletwa vipi ndani na zinalipiwa ushuru kiasi gani ili tulinde viwanda vyta ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiinyanyua pamba utai-save pamba, umem-save mkulima, ume-save mtu aliyeajiriwa kwenye kiwanda, umei-save nchi inapoagizia kwa kutumia pesa za kigeni nchi ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wetu wanavaa nguo kutoka nje, Wanajeshi wetu wanavaa nguo kutoka nje, JKT wanavaa nguo kutoka nje ya nchi, pamba tunayo ndani, si aibu!

MBUNGE FULANI: Aibu!

MHE. IBRAHIM MOHAMMED SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, *we eat what we don't produce and we produce what we don't eat.* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwe na viwanda vyta kisasa vikazalisha nguo tukawapa Polisi wetu tuka-save pesa ya kigeni, kwenye bajeti tukapunguza matumizi. Kwa nini tuisitengeneze nguo za Kijeshi, Polisi, JKT, Mablanketi ya hospitali na nguo za wanafunzi wetu?

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hata Tanzania mwaka huu mzima imesafirisha bidhaa za dola bilioni mia nne Kenya, lakini Kenya na udogo wake wametuuzia dola mia tatu na tisini na tatu, tofauti iliyopo ni dola milioni 21, wakikazana

kidogo tu wale Wakenya kule watatushinda kiuchumi na watasafirisha bidhaa zao nyingi zaidi. Turejeshe siasa ya Ujamaa katika nchi ya Tanzania, ndiyo *solution* yetu, ubepari umetushinda na hii kazi tunayokwenda nayo tutawakandamiza kiuchumi wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mohammed Sanya, Mheshimiwa Faith Mitambo Mbunge wa Liwale atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Salim Turkey.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpa pongezi Waziri wa Fedha Dokta Mgimwa kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Fedha. Mchango wangu nitautoa katika kilimo, viwanda pamoja na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo tunafahamu kwamba kinachukua ajira ipatayo asilimia sabini na tano, asilimia sabini na tano ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo. Kilimo kina sekta nyingi, kina sekta za umwagiliaji, kilimo kina sekta ya mazao ya kawaida kama korosho, pamba na kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia sana kwenye zao la korosho. Tunapozungumza kwamba, mwaka jana tulifail/katika mazao ya bishara kwa sababu ya kukosa pembejeo, tatizo hili tena linajitokeza mwaka huu, mwaka jana tulilalamika sana kuhusu suala la pembejeo na matokeo yake zao la korosho halikuwa kama vile tulivyotegemea. Tatizo hili tena limetokea mwaka huu, mpaka sasa hivi tunavyozungumzia wananchi hawajapata pembejeo za kutosha.

(Hapa umeme ulikatika)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Endelea.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipaumbele ambavyo Serikali imevitoa ni pamoja na kilimo, lakini kinakuwa ni kipaumbele gani kinatolewa wakati suala la pembejeo linakosekana. Hili ni suala la kusikitisha, wakulima wangu toka natoka Jimboni mpaka nafika hapa hawana pembejeo hata moja, lakini bado katika bajeti hii tumezungumzia mambo ya kilimo na tumetoa kipaumbele katika mambo ya kilimo. Naomba kumwuuliza Waziri wa Kilimo, wakulima wale tunawafanyaje kama mpaka kufikia sasa hivi hawajapata pembejeo na hapo hapo tunasisitiza masuala ya kilimo na kilimo kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Kilimo achukue hatua za haraka kwa ajili ya wakulima wa Mtwara na Lindi kwa ajili ya kupeleka pembejeo za *sulphur*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia nizungumzie suala la Viwanda vya Korosho. Viwanda vya korosho katika miaka ya 1978/79 katika Mikoa ya Mtwara na Lindi wakati vinafanyakazi, vilisaidia sana katika kuleta ajira kwa vijana wetu.

Vile vile vilisaidia kuleta bei nzuri kwa zao la korosho kwa sababu tulikuwa hatuuzi tena *raw materials*. Lakini viwanda vile viliuzwa na waliouziwa viwanda vile hawakuweza kufanya kazi ambayo inatakiwa, viwanda vimegeuka kuwa magodauni na kuwa magilio. Naiomba Serikali waturudishie Viwanda vya Korosho, wavirudishe ndani ya mikono ya Serikali, aidha, Serikali yenyewe isimamie wanunuzi wale walionunua Viwanda vile vya Korosho waanze kazi ya kubangua korosho ili waweze kuajiri vijana wetu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, tunazungumzia suala la ajira la vijana wakati huo huo Mikoa ya Mtwara na Lindi wakati huo ilikuwa inaajiri watu wengi mno na viwanda vingefanya kazi kwa sasa vingeweza kuajiri vijana wengi. Naiomba Serikali tena kwa mara nyingine waturudishie viwanda vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuishukuru Serikali kwa ajili ya vijana wetu wa bodaboda kuwapunguzia ushuru na kwa kweli nashukuru mno wamefanya jambo la busara. Wiki mbili tatu zilizopita nilikuwa nipo Jimboni, niliweza kukaa na vijana wa bodaboda kama 80 na nikawasilikiliza matatizo yao. Katika matatizo ambayo waliyatoa ni pamoja na hili wakilalamikia kodi na bughudha mbalimbali na mambo mengine ambayo yalikuwa yanawasumbua. Nichukue nafasi hii kuishuru sana Serikali, kwa ajili ya kuwapunguzia kodi vijana hawa. Kwa kweli wengi walikiri walisema sisi wengine tulikuwa wezi, wengine tulikuwa majambazi, wengine tulikuwa wazururaji, lakini sasa hii kazi ya bodaboda ndiyo inayotufanya tuishi, tunaiomba sana Serikali ituone. Sasa Serikali imewaona na vijana wa bodaboda mmesikia huko mliko, Serikali imewaona, fanyeni kazi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee sekta ya madini. Katika Jimbo langu sekta ya madini bado inanipa shida, vijana wachimbaji wadogo wadogo bado wanapata matatizo ya kunyanyaswa na wachimbaji wakubwa, nilishaliongelea hili mara nyingi, naomba Serikali ilifikirie kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza ifikirie kuweka ofisi ya madini katika Wilaya ya Liwale kwa sababu Wilaya ya Liwale ndiyo Wilaya ambayo inatoa madini mengi kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi lakini ofisi ya Madini iko Mtwara. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni jinsi gani wananchi wa Wilaya hii wanapata shida kwa ajili ya kushughulikia masuala haya ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naomba pia sheria za madini ziangaliwe upya kwa sababu zinakandamiza sana wachimbaji wadogo wadogo, nilishalizungumzia hili na leo nalizungumzia tena. Mchimbaji mdogo anapokuwa amechimba mahali, anapokuja mchimbaji mkubwa, mchimbaji mdogo hana haki. Naomba sana tuangalie tena hizi Sheria za Madini na umilikaji wa madini jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa hayo. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa nampa nafasi ya mwisho Mheshimiwa Turkey.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana, nami nimshukuru *Allah Subhanah Wataallah* kwa kutujalia fursa hii kubwa leo ya kuweza kuchangia bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwapongeza wale wote walioteuliwa kwa kushika nyadhifa zao mpya hizi na Mwenyezi Mungu awajalie na awaongoze katika kufanya kazi hili kwa kheri kubwa na subira kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kueleza machache kidogo ambayo kwa kweli katika Bunge letu yanaleta picha mbaya sana kwa nchi yetu. Naamini kabisa hakuna Bunge lolote linalotawala likakosa Upinzani na hakuna wema hata mmoja utakaofanya wewe mtawala Mpinzani akausifu, hilo haliwezekani, lakini jamani tujaribu kujifundisha, ikiwa mtu kama hawezi kumshukuru mzazi basi hata Mwenyezi Mungu hawezi akamshukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka tusitake tulionmo humu wote asilimia kubwa ni matunda ya Chama Tawala, kwa hivyo haifai kabisa tukikaa hapa tukaanza kutukanana na kusemana

vibaya, natoa nasaha kwetu sote tunapoongea basi tuongee mada zinazotuhusu na uchumi wetu na namna ya kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka yote bajeti inapangwa hapa na mwaka jana bajeti imepangwa, hivi jamani tumesikia wapi watu wamekufa kwa njaa, wameuana kuna hali ya hatari nchini, lakini unapoingia katika Bunge hili Watanzania wenyewe tunavyozungumza utafikiri katika Tanzania hii watu hawaishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani Tanzania yetu ni nchi tulivu sana, tunaishi vizuri, kwa hivyo inafaa kabisa tukikaa tuisifu Tanzania yetu, tukosoane pale tunapoteleza lakini jamani haifai, mpaka sasa hivi naona hakuna aliyeanguka kuna kuteleza, kama tukitazama nchi za wenzetu mambo yanayotokea basi jamani Tanzania amani na utulivu hakuna sehemu inapatikana isipokuwa kwenye Chama Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania vijana ni wengi sana, wasomi wapo kiasi, lakini watu waliopo katika elimu ya kati na chini tupo wengi sana. Mimi sitoichambua bajeti kwa kina, lakini kuna mada moja ambayo inanihu na mimi ni mdau mkubwa, nina *interest* kubwa sana nayo ni biashara ya sukari na mchele. Kwa hivyo na-declare *interest*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana katika Bunge hili watu wanaposimama wakasema kwamba Serikali kwa kuondoa ushuru haijawasaidia Watanzania, jamani tunamdaganya nani, wakati vibali vyatukarishwa vinaolewa nchini bei za sukari ilikuwa ni dola 920 mpaka 960, bei ya *exchange rate* ilikuwa ni elfu moja mia nane na hamsini, kwa maana hiyo mfuko mmoja wa sukari pale bila ya ushuru unakugharimu shilingi tisini elfu ni sawa na shilingi elfu moja na mia saba kwa kilo hamsini bila ya ushuru. Leo kama utalipa ushuru kilo moja ya sukari ile Mtanzania utanunua kwa shilingi 3400. Sasa leo Tanzania hii hebu tutazame kweli Watanzania

walikuwa wakinunua sukari kwa shilingi elfu mbili na elfu mbili mia nne na ndiyo sababu kubwa leo nchi jirani zote zikawa zinachukua sukari Tanzania, kwa sababu Tanzania katika *East Africa* nzima ndiyo sukari iliuzwa bei rahisi. Kwa hivyo, badala ya kupotosha wananchi kwamba kushushwa kwa bei ya sukari ile Watanzania hawajasaidiwa, hilo ni uwongo tunawapotosha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia suala la mchele, mchele haujapata kusamehewa ushuru Tanzania mpaka leo, hakuna mchele uliosamehewa ushuru na badala yake Wafanyabiashara wa mchele tulikuwa tukihangaika na kusema kwamba jamani umefika wakati sasa hivi pia ushuru uondoshwe katika mchele ili uweze kuuzwa kwa urahisi, kwa sababu bei ya mchele sasa hivi imefika karibu shilingi 2500. Naamini kama tukiondisha ushuru basi mchele huu unaweza ukawa rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, nawaomba sana ndugu zangu wanapoongea mada hizi waongee *with facts*. Leo sukari ilishashuka bei, sasa hivi sukari inauzwa dola mia saba na sitini na bei ya dola imekuwa 1600, sasa tuangalieni bei ya sukari sasa hivi inauzwa bei gani? Ni shilingi 76,000. Sasa ni nini kimetokea, soko la dunia nzima liliipanda juu, sasa usitegemee Tanzania watu watauza bidhaa rahisi, hilo haliwezekani, sisi tunaendeshwa na nguvu za ulimwengu. Kwa hivyo, wakati watu wanaposema kwamba, Tanzania bei zinapanda kiholela siyo sahihi, ikiwa kama vitu tunavyonunua kutoka nje vimepanda sisi tutauza rahisi kwa misingi ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kusositiza ni kwa Waziri wa Fedha pamoja na Mawaziri wengine wanaohusika na mambo ya Viwanda. Tanzania inabidi tuangalie sana uzalishaji wa viwanda vyetu na humo pia nina-declare interest kwamba tunavyo viwanda vyetu, sasa hivi katika bajeti hii kuna kitu kinaitwa *LABSA* kimeondoshwa ushuru.

LABSA ni *raw material* inayokuja katika *liquid form* inatoka nchi za nje. Miaka yote sabuni haiwezi kutengenezwa bila *raw material* hiyo na ilikuwa ikiagizwa kutoka nje, leo hapa Tanzania kuna kiwanda kikubwa sana kimewekwa kinazalisha tani mbili kwa saa na kitakuwa na tani 48 kwa siku maana yake viwanda vya ndani hapa vyote ukivijumlisha basi *demand* yao *hardly* ni tani ishirini mpaka ishirini na tano kwa siku, kwa maana hiyo tuna *surplus* ya *quantity*. Leo unaposema kwamba unaondoa ushuru kwenye sabuni ile na naamini kabisa kwenye *raw material* zile, wafanyabiashara ndiyo sisi, ushuru ukiondolewa bei ya sabuni haitoshuka itabaki pale pale. Sasa hivi kelele yetu ni kwamba, tuongeze vipato vyetu vya ndani. Kwa maana hiyo naomba sana viwanda vilindwe na kusamehewa kwa ushuru ule hakuna mtu ambaye anaathirika zaidi ya mwananchi kuumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo naomba ushuru ule nafikiri katika kutengeneza bajeti ile kuna mahali tume-*overlook* tukaona kwamba labda viwanda vya aina hiyo havipo au taarifa hazijakwenda vizuri lakini kiwanda kipo tena kikubwa na cha pili kipo katika ujenzi *in another six seven month* kitaanza pia uzalishaji. Kwa maana hiyo, naishauri Serikali ambayo ni sikivu sana na naamini kwamba tutaweza kuona wapi tuliteleza ili tuweze kurekebisha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisite hapo, niwashukuru watu wote waliochangia, nazidi kutoa nasaha zangu za kuhakikisha kwamba tuangalieni jamani, tusije tukatoa utamu wa Bunge hili kwa kulumbana bila ya kuwa na hoja nzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Turkey nakushukuru sana kwa mchango wako umetusaidia sana. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wale wote

ambao mmechangia kwa siku ya leo, kwa kweli tumekwenda vizuri sana na naamini kabisa kwamba kwa mwendo huu tutafika. Niwataarifu tu kwamba wachangiaji wangu karibu wanakwisha na nimefunga kupokea maombi mapya. Kwa hiyo yejote katika waliokuwa wamejiandikisha ambaye atapata fursa ya kuchangia, mwisho itakuwa ni kesho na sana sana ni kesho asubuhi. Kwa hiyo baada ya hapo itakuwa ni mambo mengine. Kwa hiyo, yejote ambaye katika orodha yangu ameomba kuchangia basi ajilande kuchangia na hasa kesho asubuhi kwa sababu baada ya hapo huenda tukawa tumeshafunga kila kitu hapa kufuatana na orodha niliyonayo.

Waheshimiwa Wabunge, niwataje wale wa mwanzo kesho: Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Aliko Kibona, atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono na wengine watafuata. Niendelee kusisitiza siyo wengi uwezekano mkubwa sana tutamaliza kabla ya saa saba. Baada ya uchangiaji huo ratiba nyingine au utaratibu utakaofuata atauelezea Spika baada ya kipindi cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa leo katika *Order Paper* yetu zimekamilika, basi kwa hatua hii naomba Kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.45 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi
Tarehe 21 Juni, 2012 Saa Tatu Asubuhi*)